

# **UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA**

## **Mwongozo wa Mafunzo**



**WIZARA YA HAKI, UWIANO WA KITAIFA  
NA MASWALA YA KIKATIBA**

**Novemba 2012**



# UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

## Mwongozo wa Mafunzo



WIZARA YA HAKI, UWIANO WA  
KITAIFA NA MASWALA YA  
KIKATIBA



gíz



I(kenya (·)

**Umechapishwa na:**

Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba pamoja na Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.

**Umehaririwa na:**

Kilian Nyambu  
Musambai Arthur  
Nyongesa Wafula  
Sellah King'oro  
Jane Muthura  
Jonathan Maranya

**Umetafsiriwa na:**

Nuhu Bakari  
Prof. Clara Momanyi

**© WIZARA YA HAKI, UWIANO WA KITAIFA NA MASWALA YA KIKATIBA**

S.L.P. 56057 - 00200

Nairobi, Kenya

Simu: 02224029 / 337

Kipepesi: 02031317

Simu ya Mkono: 0728970604 / 0733241111

Barua- pepe: [info@justice.go.ke](mailto:info@justice.go.ke)

Wavuti: [www.justice.go.ke](http://www.justice.go.ke)

ISBN No. 001

**Usanifu na Mpangilio**

Musambai A. Djanana

Barua-pepe: [amsambai@yahoo.com](mailto:amsambai@yahoo.com)

**WIMBO WA TAIFA**

Ee Mungu nguvu yetu  
 Ilete baraka kwetu  
 Haki iwe ngao na mlinzi  
 Na tukae na undugu  
 Amani na uhuru  
 Raha tupate na ustawi.

Amkeni ndugu zetu  
 Tufanye sote bidii  
 Nasi tujitoe kwa nguvu  
 Nchi yetu ya Kenya  
 Tunayoipenda  
 Tuwe tayari kuilinda.

Na tujenge taifa letu  
 Ee ndio wajibu wetu  
 Kenya istahili heshima  
 Tuungane mikono  
 Pamoja kazini  
 Kila siku tuwe na shukrani.

O God of all creation  
 Bless this our land and nation  
 Justice be our shield and defender  
 May we dwell in unity  
 Peace and liberty  
 Plenty be found within our borders.

Let one and all arise  
 With hearts both strong and true  
 Service be our earnest endeavor  
 And our homeland of Kenya  
 Heritage of splendor  
 Firm may we stand to defend.

Let all with one accord  
 In common bond united  
 Build this our nation together  
 And the glory of Kenya  
 The fruit of our labour  
 Fill every heart with thanksgiving.

**YALIYOMO****UKURASA**

<b>WIMBO WA TAIFA .....</b>	iii
<b>ORODHA YA PICHA .....</b>	viii
<b>ORODHA YA MICHORO .....</b>	viii
<b>ORODHA YA JEDWALI .....</b>	viii
<b>AKRONIMU/VIFUPI VYA MANENO .....</b>	x
<b>DIBAJI .....</b>	xi
<b>UTANGULIZI .....</b>	xiii
<b>TAARIFA KUTOKA KWA MWENYEKITI, TUME YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA (NCIC) .....</b>	xiv
<b>TAARIFA KUTOKA KWA KATIBU, UWIANO WA KITAIFA .....</b>	xv
<b>SHUKRANI .....</b>	xvi
<b>MUHTASARI WA YALIYOMO .....</b>	xviii
<b>MAELEZO YA MWONGOZO WA MAFUNZO KUHUSU UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....</b>	xxi
Utangulizi .....	xxi
Rajua .....	xxii
Azimio .....	xxii
Lengo Kuu la Mwongozo wa Mafunzo .....	xxii
Malengo Maalum ya Mwongozo huu wa Mafunzo .....	xxii
Harakati.....	xxiii
Utekelezwaji wa Mwongozo wa Mafunzo .....	xxiii
Makundi Lengwa katika Uhamasishaji na Ufundishaji.....	xxiii
Mwongozo wa Waelekezi .....	xxiv
<b>SOMO LA 1: UTANGULIZI WA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....</b>	1
MADA 1: DHANA ZA UWIANO NA UTANGAMANO NA MANENO MENGINE HUSIKA .....	1
MADA 2: VIONYESHI VYA UWIANO WA JAMII .....	6
MADA 3: MANUFAA YA TAIFA LENYE UWIANO NA UTANGAMANO .....	8

MADA 4: CHANGAMOTO KWA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....	9
MADA 5: MIENENDO YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....	11
<b>SOMO LA 2: HALI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....</b>	<b>16</b>
MADA 1: JITIHADA ZILIZOFANYWA ILI KUPATIKANA KWA UWIANO NAUTANGAMANO WA KITAIFA TOKEA UHURU (1963) HADI MWAKA 2007 .....	16
MADA 2: CHANGAMOTO KATIKA KUFANIKISHA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA NCHINI KENYA .....	18
MADA 3: JUHUDI ZA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....	20
<b>SOMO LA 3: MIKAKATI YA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....</b>	<b>23</b>
MADA 1: MKAKATI .....	23
MADA 2: MIKAKATI YA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....	25
MADA 3: WAHUSIKA KATIKA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....	30
<b>SOMO LA 4: MUUNDO WA KISERA, KISHERIA NA KIASASI KWA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....</b>	<b>35</b>
MADA 1: UFAFANUZI WA MANENO “SERA, MUUNDO WA KISHERIA NA KIASASI” .....	35
MADA 2: SERA ZINAZOENDELEZA UPATIKANAJI WA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA	37
MADA 3: VIPENGELE VIKUU VYA KIKATIBA VINAVYOWEZESHA.....	38
UPATIKANAJI WA UWIANO WA KITAIFA.....	38
MADA 4: VYOMBO VYA KISHERIA VINAVYOWEZESHA KUPATIKANA .....	40
KWA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....	40
MADA 5: ASASI MUHIMU ZINAZOWAJIBIKIA UENDELEZAJI WA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....	49
<b>SOMO LA 5: MIFUMO YA TAHADHARI NA MIITIKO YA MAPEMA - MBINU ZA UPATIKANAJI WA UWIANO .....</b>	<b>53</b>
MADA 1: DHANA YA TAHADHARI NA MIITIKO YA MAPEMA .....	53
MADA 2: MANUFAA YA TAHADHARI NA MIITIKO YA MAPEMA .....	55
MADA 3: UTAMBUZI WA ISHARA ZA TAHADHARI ZA MAPEMA.....	57
MADA 4: HATUA ZA KUZUKA KWA MAFARAKANO/ MIGOGORO .....	58
MADA 5: MASWALA YA MAADILI KATIKA UTARATIBU WA TAHADHARI ZA MAPEMA.....	60

MADA 6: MBINU ZA KUPUNGUZA MIGOGORO KWA KUTUMIA MIFUMO YA TAHADHARI ZA MAPEMA NA MIITIKO .....	62
<b>SOMO LA 6: MAWASILIANO KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....</b>	<b>65</b>
MADA 1: MAWASILIANO SHIRIKISHI.....	65
MADA 3: UMUHIMU WA MAWASILIANO KATIKA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....	72
MADA 4: VIZUIZI KATIKA MAWASILIANO SHIRIKISHI.....	73
MADA 5: JUKUMU LA SERIKALI KATIKA MAWASILIANO SHIRIKISHI .....	75
<b>SOMO LA 7: UDHIBITI NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA KUIMARISHA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....</b>	<b>77</b>
MADA 1: UFAFANUZI WA MAANA YA MANENO MGOGORO, UDHIBITI WA MGOGORO NA MANENO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYA.....	77
MADA 2: SURA YA MIGOGORO NA VISABABISHI VYAKE .....	79
MADA 3: MIKAKATI YA UDHIBITI WA MIGOGORO .....	81
MADA 4: MANUFAA YA UDHIBITI WA MIGOGORO .....	89
<b>SOMO LA 8: UTARATIBU WA MAPATANO NA MARIDHIANO KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....</b>	<b>92</b>
MADA 1: SWALA LA MAPATANO NA MARIDHIANO .....	92
MADA 2: UTARATIBU WA MAPATANO NA MARIDHIANO .....	94
MADA3: MANUFAA NA CHANGAMOTO ZA MAPATANO NA MARIDHIANO.....	96
<b>SOMO LA 9: MFANO WA KUIGWA KATIKA UIMARISHAJI WA TAIFA LENYE UWIANO .....</b>	<b>98</b>
MADA 1: DHANA KAMILI YA MFANO WA KUIGWA NA MABINGWA WA UWIANO .....	98
MADA 2: MANUFAA YA MABINGWA WA UWIANO KATIKA JAMII .....	100
<b>SOMO LA 10: KUIWEZESHA JAMII KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....</b>	<b>102</b>
MADA 1: KUIWEZESHA JAMII.....	102
MADA 2: UTARATIBU NA WAJIBU WA KUIWEZESHA JAMII KUPATA UWIANO WA KITAIFA.....	104
MADA 3: AINA ZA UWEZESHAJI WA JAMII.....	106
MADA 4: UMUHIMU WA UWEZESHAJI.....	108

MADA 5: MIKAKATI ENDELEVU YA KUIWEZESHA JAMII .....	109
<b>SOMO 11: USAWA NA UHUSISHWAJI KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....</b>	<b>111</b>
MADA 1: USAWA NA UHUSISHWAJI .....	111
MADA 2: VISABABISHI NA AINA ZA UTENGWAJI NA UTELEKEZWAJI.....	114
MADA 3: HATUA ZA KUENDELEZA USAWA NA UHUSISHWAJI .....	117
MADA 4: MANUFAA YA USAWA NA UHUSISHWAJI.....	118
<b>SOMO 12: UDHIBITI WA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI .....</b>	<b>120</b>
MADA 1: MAANA YA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI .....	120
MADA 2 : CHANGAMOTO KATIKA KUDHIBITI UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI. ....	123
MADA 3 : MIKAKATI YA KUENDELEZA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI.....	124
MADA 4 : UMUHIMU WA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI.....	125
<b>SOMO 13: NAFASI YA MAADILI NA KANUNI ZA UTAWALA KATIKA UWIANO WA KITAIFA.....</b>	<b>128</b>
MADA 1: MAADILI, KANUNI ZA UTAWALA NA MANENO MENGINE .....	128
MADA 2: MAADILI YA KITAIFA NA KANUNI ZA UTAWALA KAMA ZILIVYO KATIKA KATIBA.....	130
MADA 3: CHANGAMOTO ZINAZOSHUGHULIKIWA NA MAADILI NA KANUNI ZA UTAWALA.....	136
MADA 4: MIKAKATI INAYOSHIRIKISHA MAADILI YA KITAIFA NA KANUNI ZA UTAWALA.....	137
MADA 5: NAFASI YA MAADILI NA KANUNI ZA UTAWALA KATIKA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .....	138
<b>SOMO 14: UKAGUZI NA UTATHMINI WA MIRADI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA.....</b>	<b>141</b>
MADA 1: TOFAUTI KATI YA UKAGUZI NA UTATHMINI .....	141
MADA 2: UTARATIBU WA UKAGUZI NA UTATHMINI.....	143
MADA 3: UMUHIMU WA UKAGUZI NA UTATHMINI.....	145
MADA 4: MBINU NA ZANA ZA UKAGUZI NA UTATHMINI .....	147

## ORODHA YA PICHA

Picha 1	Shughuli za Uwiano wa Kitaifa .....	Ukurasa wa 5
Picha 2	Jamii yenye uwiano na maendeleo ya kiuchumi.....	Ukurasa wa 7
Picha 3	Kutafakari kuhusu jamii isiyo na uwiano.....	Ukurasa wa 10
Picha 4	Madhimisho ya kitaifa.....	Ukurasa wa 17
Picha 5	Changamoto za kufanikisha uwiano na utangamano wa kitaifa nchini Kenya.....	Ukurasa wa 19
Picha 6	Jitihada za kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.....	Ukurasa wa 21
Picha 7	Stakabadhi za Kisheria na sera za Uwiano na Utangamano.....	Ukurasa wa 36
Picha 8	Hali zinazoathiri ufanisi katika maridhiano.....	Ukurasa wa 95
Picha 9	Watu ambao ni Mifano ya Kuigwa ya Uwiano.....	Ukurasa wa 101
Picha 10	Jamii inayozingatia uhusishwaji.....	Ukurasa wa 113
Picha 11	watu waliohamasishwa	Ukurasa wa 118
Picha 12	Uanuai wa kitamaduni mionganoni mwa jamii za Kenya.	Ukurasa wa 122

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1	Mfumo wa Mawasiliano .....	Ukurasa wa 66
Mchoro 2	Utaratibu wa Mawasiliano .....	Ukurasa wa 71
Mchoro 3	Jinsi ya kudumisha mawasiliano shirikishi.....	Ukurasa wa 74
Mchoro 4	Mikakati ya kudhibiti Migogoro.....	Ukurasa wa 82
Mchoro 5	Mwelekeo wa Ukaguzi na Utathmini unaozingatia Matokeo.....	Ukurasa wa 149

## ORODHA YA JEDWALI

Jedwali 1	Tofauti kadha baina ya Nchi na Taifa .....	Ukurasa wa 13
Jedwali 2	Taswira ya Uwiano na Utangamano.....	Ukurasa wa 13
Jedwali 3	Wahusika katika Kuendeleza Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.....	Ukurasa wa 33
Jedwali 4	Vyombo vyta kisheria vinavyoendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.....	Ukurasa wa 48
Jedwali 5	Taasisi muhimu zilizowezeshwa kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa .....	Ukurasa wa 51
Jedwali 6	Hatua za Kuenea kwa Mafarakano ama Migogoro...	Ukurasa wa 59
Jedwali 7	Maswala ya Kimaadili katika Tahadhari za Mapema.	Ukurasa wa 61

Jedwali 8	Mikakati ya Kupunguza Migogoro.....	Ukurasa wa 63
Jedwali 9	Aina ya Mawasiliano Shirikishi.....	Ukurasa wa 68
Jedwali 10	Kuelezea Mitindo ya Migogoro.....	Ukurasa wa 83
Jedwali 11	Mitindo ya usuluhishaji wa migogoro.....	Ukurasa wa 88
Jedwali 12	Baadhi ya maadili ya kitaifa na kanuni za utawala..	Ukurasa wa 129
Jedwali 13	Tofauti kati ya Ukaguzi na Utathmini.....	Ukurasa wa 142
Jedwali 14a	Kupima utendakazi wa mradi.....	Ukurasa wa 148
Jedwali 14b	Kupima utendakazi wa mradi.....	Ukurasa wa 148
Jedwali 15	Mfano wa muundo wa ukaguzi na utathmini.....	Ukurasa wa 149

## AKRONIMU/VIFUPI VYA MANENO

AEC	African Economic Community
APPER	Africa's Priority Programme for Economic Recovery
AU	African Union
CDF	Constituency Development Fund
CSO	Civil Society Organizations
DNC	Department of National Cohesion
EACC	Ethics and Anti-Corruption Commission
ECOSOC	Economic and Social Council
ICC	International Criminal Court
ICERD	International Convention on Elimination of all forms of Racial Discrimination
KNCHR	Kenya National Commission on Human Rights
KNDR	Kenya National Dialogue and Reconciliation
LATF	Local Authority Transfer Fund
LPA	Lagos Plan of Action
MoJNCCA	Ministry of Justice, National Cohesion and Constitutional Affairs
MTP	Medium Term Programme
NCCK	National Council of Churches of Kenya
NCIC	National Cohesion and Integration Commission
NEPAD	New Partnership for Africa's Development
NGO	Non-Governmental Organizations
NSC	National Steering Committee on Peace Building and Conflict Management
REC	Regional Economic Commission
RRI	Rapid Results Initiative
TJRC	Truth, Justice and Reconciliation Commission
UN	United Nations
UNDP	United Nations Development Programme
UNEP	United Nations Environment Programme
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
UNHCR	United Nations High Commission for Refugees

## DIBAJI

---

Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (*National Cohesion and Integration*) unahusisha umoja, usawa, uhuru, demokrasia, kutokuwa na vita, amani ya haki, haki ya kijamii na kuzingatia kanuni za sheria. Hali hii husaidia katika kukuza ushirikiano wa kimaadili, changamoto na kuandaa nafasi za kimaisha. Kuzuka kwa ghasia za baada ya uchaguzi nchini Kenya hasa baada ya matokeo ya kura za urais kuliashiria kuwepo kwa farakano la muda ambalo halikuwa limeshughulikiwa kwa muda mrefu. Mambo haya ndiyo yaliyosababisha ghasia ambazo zilirudisha nyuma maendeleo ya Kenya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Kutokana na hili, mamlaka ya Wizara ya Haki na Maswala ya Kikatiba wakati huo yalipanuliwa ili kuhusisha uwiano wa kitaifa. Hii ilikuwa mojawapo ya sehemu nne zilizohitaji kuzingatiwa chini ya Ajenda ya nne (4) inayohusisha uimarishaji wa Uwiano na Umoja wa Kitaifa. Idara ya Uwiano wa Kitaifa (*Department of National Cohesion*) ilianzishwa mnemo Septemba 2009 ili kushughulikia jukumu lilioongezwa. Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (Disemba, 2008) ndiyo iliyosababisha kuundwa kwa Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (*National Cohesion and Integration Commission*) ili kukomesha namna zote za ubaguzi, kujenga uvumilivu na uelewano, na kuzuia kauli za uchochezi. Ili kufanikisha mamlaka yake ya kuelimisha na kuhamasisha wakenya juu ya mambo yanayohusu uwiano wa kitaifa na yale yaliyomo katika Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa, 2008, Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Masuala ya Kikatiba pamoja na Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa zimetayarisha Mwongozo wa Mafunzo ya Uwiano na Utangamo wa Kitaifa, mbali na mengine.

Upatikanaji wa uwiano wa kitaifa ni mojawapo ya malengo ya Rajua ya 2030 ya Kenya chini ya Nguzo ya Kisiasa kuhusu mkakati wa Usalama, Ujenzi wa Amani na Udhibiti wa Mafarakano. Ili kufanikisha mambo haya, mkakati huo unaeleza, "(iii) kuendeleza taratibu zinazohusu kuwepo kwa mazungumzo mionganii mwa jamii ili kujenga amani kwa makundi ya kikabilii, kirangi na makundi mengine; (iv) kuendeleza ujenzi wa amani na mapatano ili kuboresha udhibiti wa mafarakano na kuhakikisha kuwepo kwa amani ya kudumu nchini; na (v) kuimarisha desturi ya kuheshimu thamani ya maisha ya binadamu ambayo haitaruhusu vurugu kama chombo cha kutatua mitafaruku ya kibinafsi na kijamii. Haya yanahitaji kuanzia katika familia, shuleni, kanisani na katika taasisi zote za umma."

Kwa hivyo Mwongozo wa Mafunzo ni kifaa cha kutumiwa na wahusika mbalimbali katika vikao mbalimbali vya mafunzo na uhamasishaji kote nchini katika kuwapa wananchi ujuzi, habari na maarifa muhimu. Mwisho, ningependa kutoa mwito kwa wadau wote wanaohusika katika mambo ya uwiano na utangamano wa kitaifa, kuchukua nafasi ya mwongozo huu wa mafunzo ili kuona kwamba wakenya wote

wamefahamu yote yaliyomo. Hili litachangia kujenga taifa lenye umoja na maendeleo chini ya msingi wa maadili ya kitaifa na kanuni za uongozi kama inavyoelezwa katika Ibara ya 10 ya Katiba ya Kenya, 2010.



**MHE. MUTULA KILONZO, E.G.H., SC, M.P.,  
WAZIRI WA HAKI, UWIANO WA KITAIFA NA MASWALA YA KIKATIBA.**

## UTANGULIZI

Shughuli kubwa ya serikali katika kuendeleza uwiano na utangamano inatekelezwa kuitia kwa Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba (*MoJ/MCCA*) ambayo jukumu lake, mbali na majukumu mengine, ni kusaidia katika kuwaelimisha na kuwahamasisha wakenya juu ya mambo yanayohusiana na uwiano wa kitaifa na yale yaliyomo katika Sheria ya mwaka wa 2008, kuhusu Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.

Mwongozo wa Mafunzo unanuia kuendeleza jukumu hilo la Wizara kuhusu utekelezaji wa elimu ya uraia na uhamasishaji wa wakenya juu ya uwiano wa kitaifa. Katika kusawazisha zoezi hili, mwongozo huu unawasilisha muundo mahususi katika kutekeleza mafunzo hayo, pamoja na upana wa mambo yanayopaswa kufunzwa na shughuli za kufanywa kwa wanaoshiriki mafunzo.

Ijapokuwa miradi na shughuli nyingi zimevahi kufanywa katika kufunza na kuhamasisha juu ya uwiano wa kitaifa, mapengo kadha yametambuliwa. Haya ni pamoja na ufinyu wa yale yanayopaswa kufunzwa, ukosefu wa mipango mizuri ya uwasilishaji na ukosefu wa vifaa vya kufunza yaliyomo. Mapungufu haya yameathiri juhudi za serikali kwa sababu ya kupungua kwa kasi ya utekelezaji wa mradi huo.

Kuitia kwa mwongozo huu wa mafunzo, serikali itaendelea kujitahidi kuzidisha idadi ya walimu wa kutoa mafunzo ya uwiano na utangamano wa kitaifa nchini. Mwongozo huu pia utahakikisha kuwepo kwa ubora, mfanano na usawazishaji wa mambo ya kufunzwa pamoja na utekelezwaji wake katika Wizara, Idara, Mashirika, Wahusika na Wadau wote wanaohusika katika kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.



Gichira Kibara, EBS

KATIBU MKUU MSHIKILIZI,

WIZARA YA HAKI, UWIANO WA KITAIFA NA MASWALA YA KIKATIBA

## TAARIFA KUTOKA KWA MWENYEKITI, TUME YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA (NCIC)


Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (*NCIC*) ilianzishwa chini ya Sheria Na. 12 ya 2008 ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa. Ni mojawapo ya Tume za Ajenda ya Nne (4) zilizobuniwa kutohana na Makubaliano ya Amani ya Kitaifa. Jukumu kuu la Tume ni kuchangia katika kuendeleza usawa wa nafasi, mahusiano mema, upatanifu na kuishi kwa amani pamoja mionganoni mwa watu wa makabila na rangi mbalimbali nchini Kenya, mbali na kuishauri serikali, yakiwemo mapendekezo na uwezekano wa kuingilia kati ili kurekebisha hali.

Mwongozo huu wa mafunzo ni matokeo ya utafiti wa kina, mashauriano, semina na warsha zilizofanywa na wadau mbalimbali nchini. Tuhuma na chuki za kikabila zimekuwepo kama matatizo sugu ya muda mrefu nchini. Azma ya kufikia jamii yenye uwiano na utangamano itahitaji shabaha mbalimbali ili kushawishi watu wa tabaka mbalimbali katika jamii ya Kenya.

Ni kupitia kwa utambuzi huu ambapo *NCIC* imeanzisha harakati za kuwahamasisha wana jamii kuhusu jinsi watakavyojukumika zaidi. Kwa mfano, Tume inashirikiana na Wanawake wa Umoja wa Mataifa (*UN Women*) katika kutoa mafunzo kwa wanawake na vijana ili kukuza maarifa na ujuzi wao katika udhibiti na kupunguza mafarakano. Kadhalika, Tume pia inajihusisha katika warsha za kutoa mafunzo kwa wanahabari, kikosi cha polisi na mahakama kuhusu kauli ya uchochezi na athari mbaya za kauli hiyo kwa jamii.

Taratibu za elimu ya uraia na umma katika Tume hii zimehusisha kuhamasisha jamii mbalimbali juu ya kanuni za uwiano na utangamano, mikakati ya kuimarisha uwiano wa kijamii pamoja na uchunguzi wa vielelezo vyta mabingwa wa uwiano katika jamii yetu.

Hata baada ya juhudini hizi zote, ilibainika kwamba kulikuwa na haja ya kuwa na mpangilio ulioratibiwa na kuongozwa vyema katika shughuli za kutoa mafunzo na uhamasishaji. Mwongozo huu ambao ulitayarishwa kupitia kwa ushauri mbalimbali wa wadau unatarajia kuziba hili pengo ili kushughulikia mahitaji ya kuwa na utaratibu ulio sawa wa yale yaliyomo, utoaji wa habari juu ya uwiano na utangamano, pamoja na masharti ya kuwepo kwa vifaa vyta marejeleo mbali na mengine.



Mzalendo N. Kibunjia, Ph.D., EBS

**MWENYEKITI, TUME YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA**

## TAARIFA KUTOKA KWA KATIBU, UWIANO WA KITAIFA

Mamlaka ya Idara ya Uwiano wa Kitaifa ni kuongoza katika ujenzi wa jamii inayoashiria upatanifu na usawa kuititia kwa upatanishi wa kitaifa, kumaliza ugomvi, uwiano na utangamano. Ili kutekeleza mamlaka haya, mojawapo ya mikakati ambayo idara imeteua ni kuhamasisha wananchi wa Kenya kuhusu uwiano na utangamano wa kitaifa. Kutokana na hili basi, kumekuwa na haja ya kuwa na mpangilio mahususi wa mafunzo katika mambo haya. Jambo hili muhimu limesababisha kutayarishwa kwa mwongozo wa mafunzo ili kuiwezesha Wizara na wadau wengine kutekeleza mamlaka haya kwa matokeo bora na yenye kufaa.

Kwa hakika, kuna watu wengi wanaohamasisha wakenya katika mambo yanayohusu uwiano na utangamano wa kitaifa. Hata hivyo, hakuna mipangilio mizuri iliyoko katika kuratibu shughuli hizi nchini. Kwa hivyo, mwongozo huu unatoa njia ya kuyashughulikia na kuhakikisha ulinganifu wa mafunzo na uhamasishaji.

Mwongozo huu wa mafunzo unahakikisha kuwepo kwa ulinganifu wa yaliyomo na habari nyingine zinazohusu uwiano na utangamano wa kitaifa. Habari hizi zinasambazwa kwa umma kuititia mikutano mbalimbali nchini na wafanyakazi wa Wizara na waelekezi wengine ambao tayari wamefunzwa. Hili linahakikisha kwamba wakenya wamepata habari zisizo na utata na zisizofaa. Kwa hivyo, mwongozo huu jumuishi wa mafunzo unawasilisha mambo kwa njia ya kitaaluma katika vikao mbalimbali vya uwiano na utangamano wa kitaifa. Hali hii inahakikisha kwamba dhana sawa za kimsingi, mipangilio na njia za ufundishaji zinatumwiwa kwa ukadiriaji na kutegemea hali mbalimbali zilizoko katika maeneo au vikao. Mwongozo huu basi utakuwa kifaa muhimu cha kutumiwa hata na wale wasiohusika na mambo ya kiserikali na yeote yule anayehusika katika kuwashamasisha wakenya juu ya uwiano wa kitaifa.

Mwongozo wa mafunzo unatoa utaratibu elekezi ambamo ujumbe wa uwiano wa kitaifa unapitishwa. Kuititia kwa njia hii, mwongozo huu unaweka msingi wa kutambua umuhimu wa uwiano na utangamano wa kitaifa nchini Kenya.



Michael M. Ndung'u, HSC  
**KATIBU, UWIANO WA KITAIFA**

## SHUKRANI

---

Utayarishaji wa Mwongozo huu wa Mafunzo Jumuishi ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa umefanikiwa kupitia kwa michango na juhudzi za watu na taasisi mbalimbali. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa hao wote.

Kwanza kabisa, natoa shukrani kwa Waziri wa Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Masuala ya Kikatiba (*MoJ/NCCA*), Mhe. Mutula Kilonzo, kwa maelekezo yake kuhusu sera katika utayarishaji wa mwongozo huu. Ningependa pia kutoa shukrani kwa usaidizi na msukumo tulipata hasa katika hatua za awali za utayarishaji wa mradi huu kutoka kwa aliyekuwa Katibu Mkuu, Balozi Amina Mohamed. Tunampongeza kwa kujitwika jukumu la kutayarisha mwongozo huu kama Utaratibu wa Matokeo ya Haraka (*RR*) ambao ungekamilika katika siku 100 kwenye mwaka wa Kandarasi ya Utendakazi 2011/2012 (*2011/2012 Performance Contract*). Msingi ambao aliuanzisha uliendelezwa vizuri na Katibu Mkuu Mshkilizi, Gichira Kibara ambaye kila mara akituhimiza kuendelea na mradi huu. Tunashukuru kwa ukarimu, uongozi na usaidizi wa taratibu katika shughuli zote za utayarishaji wa mwongozo huu.


Naishukuru Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (*NCIO*) kwa kuwa mshiriki mwema katika utayarishaji wa mwongozo huu. Sote tumetembea kila hatua ya safari hii pamoja. Asante kwa kutumia rasilmali yenu na kuwahusisha maafisa wenu wenye ujuzi kuwa sehemu ya timu iliyoongoza utaratibu wote hadi mwisho wenye mafanikio. Tunatoa shukrani kwa wakurugenzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Utawala Kenya (*KIA*) pamoja na Taasisi ya Elimu Kenya (*KIE*) kwa usaidizi wenu maalumu wa kuteua maafisa walio na ujuzi ili kusaidia katika utayarishaji wa mwongozo huu. Tunatambua maarifa ya thamani na tajriba katika uchapishaji na uchoraji ambao ultajirisha sana mwongozo huu.

Ninatambua kwa shukrani mchango wa wadau mbalimbali tokea Mashirika ya Kiraia (*Civil Society Organizations*), Mashirika ya Kidini (*Faith Based Organizations*) yaliyoongozwa na Baraza la Makundi ya Kidini la Kenya (*Inter-Religious Council of Kenya*), Mashirika ya Kijamii (*Community Based Organizations*), vyombo vyta habari, vyuo vikuu na watafiti kwa ajili ya utafiti mpana na mchango wao katika utayarishaji wa mwongozo huu. Shukrani zetu pia zinaziendea wizara mbalimbali za Serikali, idara na mashirika ambayo kwa namna fulani yalitekeleza majukumu muhimu katika utaratibu wote. Wizara hizo ni pamoja na Wizara za Elimu, Wizara ya Serikali kuhusu Mipango na Rajua 2030, Baraza la Kiuchumi na Kijamii la Kitaifa (*National Economic and Social Council*) pamoja na Kamati ya Malalamiko ya Umma (*Public Complaints Standing Committee*). Shukrani maalumu ziliendee jopo la Kandarasi ya Utendakazi chini ya Afisi ya Waziri Mkuu, kwa kutambua umuhimu wa kutayarisha mwongozo

huu kama matokeo muhimu katika ya Rajua 2030 na utaratibu wa kandarasi ya utendakazi.

Ningependa kutoa shukrani za kipekee kwa washiriki wetu katika maendeleo, Mradi wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*United Nations Development Programme*), na *Gesellschaft fur Internationale Zusammenarbeit (GIZ)* kwa usaidizi mkubwa wa kifedha na kimpangilio. Asanteni kwa kuwa wenyiji na kushiriki kikamilifu katika utayarishaji na majadiliano katika utaratibu wa kuanda mwongozo huu.

Mwisho bali si akali, shukrani zangu ziwaendee wafanyikazi wa Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Masuala ya Kikatiba (*MoJNCCA*), hasa Idara ya Uwiano wa Kitaifa. Asanteni kwa ubunifu na fikra zenu katika kutoa muswada wa kwanza ambao ulikuwa msingi wa kazi hii kubwa.



F. O. Owino



**MKURUGENZI, UWIANO WA KITAIFA  
WIZARA YA HAKI, UWIANO WA KITAIFA NA MASUALA YA KIKATIBA**

## MUHTASARI WA YALIYOMO

---

Mwongozo huu wa mafunzo ya uwiano na utangamano wa kitaifa ni matokeo ya jitihada za washikadau mbali mbali walioletwa pamoja na Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya kikatiba kwa ushirikiano wa Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa. Mwongozo huu uliundwa kama chombo na hazina muhimu kwa waelekezi, wahusika na washiriki kwenye nyanja za elimu na uhamasishaji wa maswala ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

Katika utayarishaji wa mwongozo huu, utaratibu bora wa kiushauri na kiutafiti ulitumika. Jitihada za awali za kuwaelimisha na kuuhamasisha umma kuitia kwa Wizara, Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC) na washikadau wengine zilisababisha kuandaliwa kwa mwongozo kutokana na viwango finyu, kina cha maswala, muktadha na hali kadhalika ukosefu wa usawa katika utendakazi wa washikadau hao. Hojaji iliandaliwa na kukabidhiwa washikadau wote ili kuipitia na kupendekezwa maelezo yanayofaa. Baada ya hapo, wahusika walifanya vikao ili kushauriana na kuwashirikisha wahusika wakuu, wakiwa ni pamoja na: wakereketwa, wasomi na hata wananchi ili kujadili kwa lengo la kuandaa matini muhimu ya mwongozo huo.

Zao la utaratibu huo wa kiushauri lilikuwa ni stakabadhi hii ambayo ni mwongozo maalum wa waelekezi na kadhalika ni marejeleo muhimu kwa wasomaji. Mwongozo huu unahusisha mada mbali mbali kuhusu uwiano wa kitaifa kama vile ufanuzi wa maneno muhimu, uthibiti wa mafarakano, wajibu wa mawasiliano katika uimarishaji wa uwiano, usimamizi wa tofauti za kikabila na nafasi ya maadili katika upatikanaji wa uwiano na utangamano kati ya mambo mengine mengi. Mwongozo huu pia unapendekeza mbinu maalum za kutoa mafunzo katika kila mada husika, vifaa maalum na mifumo shirikishi ya kutoa mafunzo kwa makundi tofauti tofauti ya watu. Michoro ya ubunifu inayopatikana katika kila mfumo hurahisisha na kuufanya usomaji wa mwongozo huu kuwa mwelesi zaidi na hali kadhalika kufurahisha. Marejeleo yaliyotolewa huwawezesha waelekezi kuimarisha mafunzo yao kuitia kwa mawanda mapana ya usomaji.

Hivyo basi, mwongozo huu unakuwa kama chombo cha kimsingi cha kuongeza idadi ya wahusika wanaojishughulisha katika kupigia debe uwiano wa kitaifa. Kwa sasa, washikadau wengi wanaweza kujishirikisha katika harakati za kutangaza uwiano kwa usaidizi wa mwongozo huu. Kadhalika, sasa itawezekana kuhakikisha kuwepo kwa viwango vya ubora na jitihada za pamoja kutoka kwa wahusika wote. Hali hii itasababisha kuwepo kwa matumizi thabiti na faafu ya rasilimali zilizopo. Mwongozo huu unatoa fursa muafaka ya kusimamia shughuli za washikadau wote waliohusishwa katika harakati za kuendeleza uwiano wa kitaifa.

Kwa ujumla, mwongozo huu kama ulivyowasilishwa unayashughulikia maswala mbalimbali yanayohusisha uwiano na utangamano. Kadhalika yanahusisha maswala yanayoambatana na pia huandaa maelezo kamilifu kuhusu mwongozo wa mafunzo. Kisha inafuatiwa na harakati zilizojaribiwa tokea enzi za uhuru hadi kufikia mwaka wa 2007 za kuimarisha uwiano na utangamano humu nchini, hasa katika sehemu ya pili. Kadhalika, mwongozo huu umeelezea kwa kina kuhusu changamoto zilizopatikana na jitihada za suluhi zilizofanywa ili kuunda uwiano na utangamano. Hali kadhalika, mwongozo huu umejadili umuhimu wa washiriki kufurahia mazingira ambayo yametangaza ama kuchangia pakubwa kukosekana kwa ushirikiano baina ya jamii mbali mbali, hali ambayo inaweza kuathiri maisha yao ya baadaye.

Somo la tatu linaelezea maana halisi ya mkakati mzima. Linajadili mikakati mbali mbali ya kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa na pia kuyafafanua majukumu ya wahusika walioshirikishwa. Kadhalika, linaelezea mbinu na shughuli zinazoweza kutumika katika kuendeleza uwiano wa kitaifa. Somo hili linafuatiwa na somo la vyombo vyanya kisheria vinavyotoa mfumo mzima unaotumiwa na wanajamii ili kuhakikisha wana mahusiano mema. Vyombo hivi ni pamoja na: Katiba, Sheria za Bunge, Sera, Mikataba, Maazimio, na Makubaliano. Ni kuitia kwa vyombo hivi ambapo taasisi na mashirika mbali mbali yanapopata majukumu na kanuni zao za utendakazi ili kuhakikisha uwepo wa taifa lenye uwiano na utangamano. Hivyo basi, somo hili hutilia mkazo kuwepo kwa ushirikiano wa karibu kati ya Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba, Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano na wizara nyinginezo pamoja na idara za kiserikali, zote zikiwa na majukumu yanayokaribiana.

Somo la tano limejadili kwa kina umuhimu wa tahadhari hizi za mapema na kuwepo kwa taratibu za kutafuta suluhi katika upatikanaji wa jamii inayoshirikiana kikamilifu. Katika njia za kusifu ubora wa somo hili, taratibu muafaka za uzuiaji wa migogoro unafaa kupewa kipaumbele. Somo la sita linaelezea mawasiliano shirikishi na kufafanua utaratibu wa mawasiliano. Inagusia umuhimu wa mawasiliano bora katika harakati za kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa na pia kuielezea wazi vizingiti inayoathiri pakubwa mawasiliano bora. Kadhalika, majukumu ya washiriki mbali mbali wanaoshughulikia mawasiliano bora yamejadiliwa.

Somo la saba linatoa mafunzo ya kimsingi ya jinsi ya kushughulikia udhibiti na usuluhishaji wa migogoro. Somo hili pia linashughulikia mbinu mbali mbali za kutatua na kutafuta suluhi kwa migogoro. Somo linalofuatia linaelezea njia za kuponyesha donda-ndugu na upatikanaji wa suluhi ya migogoro. Linafafanua utaratibu wa kusameheana na kuwaleta pamoja waathiriwa huku likiweka wazi manufaa na changamoto ya utaratibu huo pamoja na mikakati ya mshikamano huo.

Mabingwa wa uwiano na walio kama kielelezo katika jamii wameelezwa vyema

katika somo la tisa. Somo hili pia linagusia majukumu ya mabingwa hao wa uwiano katika jamii. Somo linalofuatia linatoa mafafanuzi ya kina kwa washirika kuhusu maswala mbali mbali ya utoaji wa mamlaka kwa wanajamii ili kuimarisha uwiano na utangamano wa kijamii. Somo linalofuata linatoa taarifa muhimu kuhusu haki na ushirikishwaji. Fauka ya hayo, somo hili linaelezea kwa kina kuhusu mahusiano yaliyopo kati ya haki na ushirikishwaji na uwiano na utangamano wa kitaifa.

Maadili ya kikatiba yanachangia kuwepo kwa somo linalopendekeza kuundwa kwa Sheria ya Bunge itakayoidhinisha Ibara ya 4 (2) na ile ya 10 ya Katiba. Hii ni kwa lengo la kurasimisha kanuni za maadili ya kitaifa na kuunda asasi itakayosimamia utoaji wa ushauri na kuwaelekeza washikadau kwa lengo la kusimamia kanuni hizo za maadili ya kitaifa hasa kwa kila mkenya. Hii ni kwa sababu ya kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa. Somo la mwisho linafafanua maana halisi ya usimamizi na utathmini na hali kadhalika linachanganua utaratibu unaofaa kutumiwa katika kuendesha shughuli za usimamizi na utathmini huo ili kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa. Umuhimu wa usimamizi na utathmini huo umefafanuliwa kwa kutumia mbinu na zana mahususi.

## **MAELEZO YA MWONGOZO WA MAFUNZO KUHUSU UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA**

### **Utangulizi**

Serikali huimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa kwa kuhakikisha kuwepo kwa udhibiti wa masuala ya siasa, kijamii na kiuchumi. Ni jukumu la serikali kuunda mazingira mwafaka na yanayotabirika kwa raia ili kuwawezesha kuyashughulikia maazimio na mahitaji yao maishani. Serikali ya Kenya imetumia mikakati mbalimbali kuimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa. Mojawapo ya mikakati iliyotumiwa na Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba ni uelimishaji na ufundishaji kwa lengo la kutoa msingi thabit kwa mabadiliko ya kijamii. Mwongozo huu wa ufundishaji unasaidia kuweka pamoja jitihada hizo kwa ajili ya kuendeleza uwiano na utangamano.

Mwongozo huu wa ufundishaji umeundwa ili kuwesha kila mhusika wa maswala ya uwiano na utangamano wa kitaifa kutekeleza jukumu la kufundisha raia wa Kenya kuhusu masuala yanayohusiana na uwiano na utangamano wa kitaifa. Kwa hivyo, mwongozo huu unatoa mpangilio na hali kadhalika kuhakikisha kwamba pana mfanano katika ufundishaji.

Lengo kuu la mwongozo huu wa ufundishaji limetokana na ukweli kwamba uwiano na utangamano wa kitaifa siyo fani huru za kielimu katika asasi za masomo za humu nchini. Hii inamaanisha kwamba mtu hawezi kupata vitabu ama marejeleo muhimu yanayohusiana na fani hizi za elimu moja kwa moja. Kwa hivyo, mwongozo huu wa uhamasishaji sio kwamba tu unatoa vitabu vilivyoundwa mahususi kwa ajili ya mazingira halisi ya taifa la Kenya lakini pia husaidia mno katika utafiti kwa wenyeji na wageni. Hali hii huandaa msingi wa utafiti wa siku zijazo hasa kuhusu masuala fulani yanayolandana na mazingira ya taifa la Kenya.

Kama ilivyotajwa hapo awali, mwongozo huu wa mafunzo ya uhamasishaji wa kiutangamano huhakikisha kwamba kuna mfanano wa mambo yaliyomo na data nyinginezo za uwiano na utangamano wa kitaifa zinazosambazwa na wafanyakazi wa Wizara pamoja na waelekezi wengine waliofunzwa ili kuusaidia umma katika makongamano mbali mbali kote nchini Kenya. Kwa hivyo, Wakenya watapokea taarifa sawa na hizo zitakazopitishwa kwenye makongamano yatakayokuwa yanaeleweka vyema na ambayo hayatahusisha masuala yasiyoeleweka. Kwa ujumla, mwongozo huu wa mafunzo ya uhamasishaji wa kiutangamano hutoa maelekezo ya kitaalamu katika makongamano mbali mbali yanayoshughulikia uwiano na utangamano wa kitaifa. Kimsingi, hali hii inahakikisha kuwepo kwa matumizi ya dhana kuu zinazofanana; mielekeo na njia zenye mabadiliko katika mtazamo fulani ili kuingiliana na muktadha wa maeneo fulani ama makongamano.

## Rajua, Azimio na Malengo ya Mwongozo wa Mafunzo

Mwongozo wa Pamoja wa Uhamasishaji kuhusu Uwiano na Utangamano wa Kitaifa unaongozwa na maswala yafuatayo: Rajua, Azimio na Malengo.

### Rajua

Chombo kikuu cha mafunzo ya uendelezaji wa uwiano na utangamano wa kitaifa.

### Azimio

Kutoa mafunzo yaliyo sawa na yanayoambatana na uwiano na utangamano wa kitaifa kupitia kwa uhamasishaji bora na miradi ya kuwezeshana.

### Lengo Kuu la Mwongozo wa Mafunzo

Lengo Kuu la mwongozo huu ni kutoa mpangilio wa mbinu za kufundisha na kuhamasisha kuhusu uwiano na utangamano wa kitaifa nchini.

Zifuatazo ndizo sababu kuu za nyaraka hii:

- Kutaalamisha ufundishaji na uhamasishaji kuhusu uwiano na utangamano wa kitaifa humu nchini;
- Kuimarisha usimamizi wa ufundishaji na uhamasishaji kuhusu uwiano na utangamano wa kitaifa;
- Kuhakikisha kuwa kuna usawa katika uhamasishaji/ufundishaji wa uwiano na utangamano wa kitaifa; na
- Kutoa habari, maarifa na ujuzi katika uendelezaji wa uwiano na utangamano wa kitaifa.

### Malengo Maalum ya Mwongozo huu wa Mafunzo

Mwongozo wa Uhamasishaji wa Kiutangamano wa Kitaifa una malengo maalum yafuatayo:

- Kutoa habari muhimu na zinazostahili kuhusu uwiano na utangamano kwa waelekezaji;
- Kutoa msingi wa utafiti utakaotumiwa na waelekezaji ili kufanya utafiti zaidi kabla ya kurejelea kikamilifu zoezi lenyewe la uhamasishaji;
- Kutoa mbinu mbali mbali za majoribio na zile za ushirikishi ili kuhamasisha katika makongamano tofauti tofauti.
- Kuhakikisha kuwepo kwa usawa na ushikamano katika ujumbe uliotolewa kwenye makongamano ya uhamasishaji kote nchini.
- Kuwapa waelekezi mwongozo kuhusu malengo ya kijumla na maalum ya kila somo la uhamasishaji na hivyo kuhakikisha kuwa wanabakia waaminifu kwa ajenda ya uwiano na utangamano wa kitaifa;
- Kuongoza waelekezi katika uzingatiaji wa muda katika nyakati za makongamano ya uhamasishaji ili kuhakikisha kwamba yote yaliyopangwa hayatimizwi tu katika muda uliotarajiwa lakini pia vyema; na

- g. Kuwapa waelekezi mwongozo kuhusu shughuli na vifaa wanavyootarajia kutumia katika utekelezaji mzuri wa kazi yao ya kuwezesha hafla ya uhamasishaji kuhusiana na uwiano na utangamano wa kitaifa.

## **Harakati**

Uandaaji wa mwongozo huu wa mafunzo ulishirikisha washikadau wengi. Ulihusisha wahusika wafuatao:

- a. Wizara za Serikali, Idara na Mashirika mbali mbali (MDAs);
- b. Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya kikatiba;
- c. Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC);
- d. Mashirika ya Kijamii (CSOs)
- e. Washirika wa Kimaendeleo;
- f. Mashirika ya Kidini (FBOs);
- g. Vyombo vya Habari;
- h. Sekta ya Kibinagsi;
- i. Miungano ya Mashirika ya Kibashara;
- j. Mabaraza ya Wazee; na
- k. Vyuo Vikuu vya Umma na Vya Kibinagsi.

## **Utekelezwaji wa Mwongozo wa Mafunzo**

Utekelezwaji wa mwongozo wa mafunzo utashughulikiwa na Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya kikatiba pamoja na washikadau wanaohusika kwenye uhamasishaji na ufundishaji ili kupata uwiano na utangamano wa kitaifa. Wahusika wengine watakaoshirikishwa katika uhamasishaji/ufundishaji wa vipengee vilivyomo katika mwongozo wa pamoja utawahusisha: Wizara, Idara na Mashirika (MDAs), Mashirika ya Kijamii (CBOs), Mashirika ya Kidini (FBOs) na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (NGOs) yakiwa na majukumu ya kuimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa.

## **Makundi Lengwa katika Uhamasishaji na Ufundishaji**

Makundi yafuatayo ya jamii ya Kenya yatalengwa katika uhamasishaji na/au ufundishaji kuhusu vipengee vya mwongozo huu. Makundi haya yanahusisha lakini hayafungiwi kwa:

- a. Vijana;
- b. Makundi ya wanawake;
- c. Watu walio na mahitaji maalum;
- d. Vyombo vya habari;
- e. Wazee wa Kijamii;
- f. Viongozi wa kisiasa;
- g. Viongozi wa kidini katika Mashirika ya Kidini;
- h. Mashirika ya Kijamii (CBOs);
- i. Watumishi wa Umma;

- j. Waundaji sera;
- k. Walinda usalama na Majeshi;
- l. Shule na vyuo;
- m. Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (NGOs); na
- n. Wawakilishi wasiokuwa wa Kiserikali (NSAs).

### **Mwongozo wa Waelekezi**

Majukumu ya mwelekezi ni muhimu sana wakati wa majadiliano au kongamano. Vifuatavyo ni vipengee vya kutumia mwongozo huu:

- a. Kutoegemea upande wowote na kuongoza majadiliano ya washiriki bila kulazimisha maoni au mambo muhimu kwako;
- b. Kuwa na mtazamo chanya (mzuri) na kuhakikisha kwamba wanaoshiriki wanahisi huru na kuhimizwa kushiriki;
- c. Kukumbuka malengo ya ufundishaji ili kuzingatia hoja muhimu pekee;
- d. Kuwapa wanaoshiriki nafasi sawa;
- e. Kila mara hakikisha kufupisha majadiliano;
- f. Kusikiliza kwa makini mchango wowote unaotolewa na washiriki;
- g. Kutumia maneno ya kuchangamsha na kusisimua ili kudumisha mvuto na umakini katika mazungumzo;
- h. Kuzingatia ishara za mwili na uso ili kuwezesha ushirika wa dhati;
- i. Kuwa mbunifu na mcheshi katika kushughulikia maoni tofauti tofauti ya washiriki; na
- j. Kuwa m'wazi ili kupokea majibu kutoka kwa wanaoshiriki.

## SOMO LA 1: UTANGULIZI WA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanafaa kuwa wamepata maarifa, ujuzi na mitazamo ambayo itawawezesha kuimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa.

### UTANGULIZI

Somo hili linaangazia dhana za uwiano na utangamano, maneno yanayohusiana nazo na linatoa msingi wa mwongozo mzima wa mafundisho.

### MADA 1: DHANA ZA UWIANO NA UTANGAMANO NA MANENO MENGINE HUSIKA

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za maelezo.

**Mbinu:** Chemsha bongo, hadithi na somo kifani.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anaorodhesha maneno na kuwaongoza washiriki ili kutoa **maana** za maneno hayo.
- Washiriki wanatoa maana za maneno yaliyoorodheshwa.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa mukhtasari maoni ya washiriki.



### Maneno Muhimu

1. Taifa, 2. Utaifa, 3. Upendo wa Utaifa, 4. Nchi, 5. Nchi Huru, 6. Uhuru wa nchi, 7. Serikali, 8. Jamii, 9. Washikadau, 10. Utangamano, 11. Uwiano, 12. Uwiano wa Kijamii, 13. Uwiano wa Kisiasa, 14. Uwiano wa Kiuchumi, 15. Uwiano wa Kitaifa, 16. Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.

### Vidokezo Muhimu

#### Maana ya Maneno

##### 1. Taifa

Taifa ni kundi la watu walio katika himaya moja ya ardhi, na wanaotumia rasilmali, maadili, utamaduni, matamanio, ishara za pamoja kama vile lugha,

bendera, wimbo wa kitaifa na Nembo ya Serikali, historia na serikali moja. Katika utangulizi wa Katiba, watu wa Kenya wamejitolea kutunza na kulinda maslahi ya raia, familia, jamii na taifa.

## 2. Utaifa

Hii ni harakati ya uundaji na udumishaji wa umoja wa nchi kuitia mashirika na asasi za kijamii, kiuchumi au kisiasa.

## 3. Upendo kwa Taifa

Ni utambuzi wa dhati wa kundi la watu wenyewe mfumo wa kisiasa unaoweza kufasiriwa kama taifa na unaouna sura ya kitaifa. Pia inaweza kuhusisha imani kuwa taifa lina umuhimu wa kimsingi, au imani kuwa nchi yao kiasili ni muhimu kuliko nyinginezo zote. Pia inatumika kufafanua kundi linalowania kulinda nchi yao.

## 4. Nchi

Nchi ni kundi la kisiasa lililoundwa kwa mipaka ya kimataifa. Linahusisha raia, kama watu binafsi au jamii.

### Sifa za Nchi

Sifa hizi zinaweza kuwekwa katika makundi mawili makuu:

- a. Mahali nchi ilipo
  - i. Inaundwa na watu/idadi inayobainika ya watu; na
  - ii. Eneo linalotambulika: ardhi, maji na anga.
- b. Msingi wa kisiasa wa nchi
  - i. Serikali inayofanya kazi; na
  - ii. Iliyo huru, inayojitawala yenyewe.

### Jedwali la 1: Tofauti kadha baina ya Nchi na Taifa

<b>Namba</b>	<b>NCHI</b>	<b>TAIFA</b>
1.	Ni chombo cha kisheria na cha kisiasa	Ni la kijamii/kitamaduni
2.	Watu waliopangwa kwenye eneo linalotambulika	Watu waliounganishwa kisaikolojia wakiwa na nia moja ya kuishi pamoja "manufaa ya jumla"
3.	Nchi lazima iwe na uhuru wa kujitawala	Watu huendelea kubaki kama Taifa hata kama hawana uwezo wa kujitawala

**5. Nchi Huru**

Ni eneo la kisasa linalohusisha Nchi huru kama vile Kenya, Uganda na Tanzania iliyo na watu wenyewe sifa fulani na wenyewe utamaduni, historia na/au lugha moja.

**6. Uhuru wa Nchi**

Jukumu moja kuu la serikali ni kuimarisha utaifa kwa kufanya nchi hiyo kuwavutia raia wake. Hali hii hupatikana kuitia kwa kuendeleza maswala ya haki, usawa na uchukuaji hatua sawazishi. Kwa hali hii, Nchi huwahitaji raia na jamii kulipatia Nchi hiyo uwezo na uhuru wake wa kisasa, kuchangisha pesa za kuendesha shughuli za Nchi, na hali kadhalika kubakia kuwa wazalendo panapozuka mavamizi kutoka nje. Uimarishaji wa umoja wa nchi hufanyika kuitia ishara za umoja kama vile: Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa na Azimio la Uaminifu, rangi za taifa, vazi la taifa, lugha rasmi, kumbukumbu la mashujaa, majengo muhimu ya kitaifa pamoja na maeneo muhimu ya taifa kama vile milima na maziwa.

**7. Serikali**

Hili ndilo shirika ambalo kwalo nia ya taifa huundwa, kuonyeshwa na kufikiwa. Hii ndiyo asasi ambayo huendesha masuala ya taifa kwa niaba ya wananchi au raia.

**8. Jamii**

Jamii ni kundi la watu wanaoishi pamoja na huwa na utamaduni na maadili sawa, na huwa na mitazamo na hofu zinazolingana.

**9. Washikadau**

Washikadau ni watu au kundi la watu wenyewe mvuto mmoja wa kibinagsi, ima iwe ni mivuto chanya (inayokubalika) ama hasi (isiyokubalika), hasa katika mambo yanayoendelea kwenye nyanja za uchumi, siasa, utamaduni na kwenye michakato ya kimazingira katika jamii.

**10. Utangamano**

Kutangamanisha ni kuleta pamoja. Utangamano huchangia pakubwa katika uwiano wa kijamii. Huwezesha raia kuhusiana na mwenzake kwa uzuri.

**11. Uwiano**

Hii ni jitihada au hali ya kubaki pamoja au ushirika wa pamoja. Ni muumano mzuri au kusikilizana baina yenu. Uwiano hurejelea tofauti chanya katika makundi na jitihada za pamoja (chanya) zinazoonekana katika jamii.

## 12. Uwiano wa Kijamii

Uwiano wa kijamii ni harakati inayoendeleza maadili ya pamoja ya kijamii, changamoto za pamoja na nafasi sawa inayoegemea matumaini fulani, uaminifu na kufaana. Pia inahusisha uhiari wa makundi yenyé maadili na malengo tofauti (pana) kuweza kuishi pamoja, kutumia rasilmali pamoja, yanayoheshimiana na kutii sheria za nchi.

Uwiano wa kijamii unahusisha uundaji wa maadili yanayofanana na jamii zinazofahamika, kupunguza tofauti zinazohusiana na amali na mapato ili kuwezesha watu kwa jumla kuelewa kwamba wanafaa kushirikiana kibashara ili kukabili changamoto zilizopo, na kwamba ni wanajamii wa jamii moja.

## 13. Uwiano wa Kisiasa

Uwiano wa kisiasa unahusisha miundo na asasi zinapofanya kazi ili kuhakikisha kuwa matakwa ya wananchi yanafikiwa huku ikihakikishwa kuwa wahusika katika siasa wanaelewana wao kwa wao.

## 14. Uwiano wa Kiuchumi

Uwiano wa kiuchumi hutokea wakati ambapo mipangilio na asasi za kifedha na kibashara zinapofanya kazi ili kuhakikisha kwamba kuna uwazi na usawa wa ugavi usio na mapendeleo wala ubaguzi wa rasilmali.

## 15. Uwiano wa Kitaifa

Uwiano wa kitaifa huhusisha uundaji wa raia wenye utangamano walio na hisia ya kuwepo kwo mionganoni mwa makundi tofauti tofauti ya wananchi na wanaotoka katika maeneo tofauti tofauti, kuititia kwa udhibiti na usuluhishaji wa tofauti zilizopo pamoja na matakwa na mahitaji yanayokinzana.

## 16. Uwiano na Utangamano wa Kitaifa

Katika muktadha wa Kenya, uwiano na utangamano wa kitaifa ni harakati na matokeo ya kuwatia na kuwawezesha wananchi kuwa na fikra na hisia kwamba ni wananchi wa taifa moja wanaojishughulisha katika asasi sawa, wanaokabiliwa na changamoto na nafasi sawa. Uwiano na Utangamano wa kitaifa unajumuisha umoja, usawa, uhuru, demokrasia, kutokuwepo kwa vita, amani yenyé haki, haki ya kijamii na utawala wa sheria.

Lengo kuu la uwiano na utangamano wa kitaifa ni kuunda jamii mahususi ya kitaifa isiyoegemea desturi za kikabila, ubaguzi wa rangi, kimaeneo, Kitabaka na kidini. Uwiano wa kitaifa hukumbatia umoja wenye lengo la kiushirika wa raia katika harakati za kiuchumi, kijamii na kisiasa.



Picha 1: Shughuli za Uwiano wa Kitaifa

## MADA 2: VIONYESHI VYA UWIANO WA JAMII

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za maagizo.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza wanaoshiriki ili kujadili **sifa muhimu** za jamii iliyowiana.
- Wanaoshiriki wanatoa sifa muhimu za jamii iliyowiana.
- Mwelekezi wanatumia vidokezo muhimu ili kunakili maoni ya washiriki.




#### Vidokezo Muhimu

#### Vionyeshi vya Uwiano wa Jamii

1. Maono sawa na hisia ya kuwepo pamoja
  - a) Jamii ina uwezo mkuu wa kuwa na uwiano katika kiwango cha mashinani ambapo watu wana hisia nzuri za kutangamana na jirani zao katika eneo hilo la mashinani.
  - b) Ili kuthibitisha kuwa watu wanashiriki maono sawa katika eneo lao huko mashinani, kuna haja ya kubaini mtazamo wao kuhusiana na hali yao ya maisha.
  - c) Kuna uwezekano mkubwa wa jamii kuwa na uwiano pale ambapo hapatakuwa na tofauti kubwa katika mtazamo wa watu dhidi ya jirani zao.
  - d) Kuna uwezekano mkubwa wa jamii kuwa na uwiano pale ambapo watu wanahisi kuwa wanawenza kuchangia katika maamuzi yanayohusu eneo lao.
2. Uanuai wa watu, hali na mazingira yao hukubalika na kuthaminiwa
 

Kuna uwezekano mkubwa wa jamii kuwa na uwiano pale ambapo wakazi wake wengi wanakubaliana na kauli hii, hasa katika maeneo yaliyo na makabila madogo.
3. Wale wanaotoka katika hali tofauti za kimaisha wana nafasi sawa.
  - a) Kuna uwezekano mkubwa wa jamii kuwa na uwiano pale ambapo kuna viwango vidogo vya kunyimwa rasilimali na tofauti chache za kiuchumi na kijamii kati ya wanajamii hao.

- b) Kuna uwezekano mkubwa wa jamii kuwa na uwiano pale ambapo ukosefu wa kazi wa muda mrefu sio tatizo kubwa na haujaegemea katika makundi fulani tu ya wanajamii.
4. Mahusiano thabiti na bora yanaimarishwa baina ya watu kutoka kwenye tamaduni mbali mbali katika sehemu za kikazi, shulenii na kati ya majirani.
- Jamii ina uwezekano mkubwa wa kuwiana pale ambapo watu wenye misingi tofauti ya kikabila na kitabaka wanashirikiana kila mara.
  - Jamii ina uwezekano mkubwa wa kuwiana pale ambapo watu kutoka makabila tofauti wanapigania kutopkuwepo kwa ubaguzi kwa msingi ya rangi, dini, jinsia, misimamo ya kimpenzi, ulemavu na umri; na wanaimarisha mahusiano mbali mbali ya kitamaduni na kidini.



Picha 2: Jamii yenye Uwiano na Ustawi wa Kiuchumi

### MADA 3: MANUFAA YA TAIFA LENYE UWIANO NA UTANGAMANO

**Muda:** Dakika 30

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, madaftari na kalamu na kanda za maagizo.

**Mbinu:** Majadiliano ya makundi.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza wanaoshiriki ili kutalii manufaa ya taifa lenye uwiano na utangamano.
- Washiriki wakiwa katika makundi wanayapitia manufaa ya taifa lenye uwiano na utangamano.  
Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa mukhtasari maono ya washiriki



#### Vidokezo Muhimu

#### Manufaa ya Taifa lenye Uwiano na Utangamano

1. Umoja na ushirikiano wa kitaifa katika kukabiliana na masuala ya ustawii wa taifa;
2. Umoja na usawa katika makabiliano dhidi ya matatizo na majanga ya kitaifa;
3. Mbinu ya pamoja katika kukabiliana na hatari kutoka nje ya taifa;
4. Mitazamo sawa, maadili na tamaduni chanya zenyet manufaa kwa taifa;
5. Matamano na matarajio sawa ambayo yanaimarisha ukuaji na ustawii wa taifa;
6. Kujitolea kutimiza maswala muhimu kwa taifa;
7. Uwezo unaoongezeka wa jitihada za pamoja miongoni mwa raia;
8. Kuimarisha matokeo ya kiuchumi na maslahi ya wakenya;
9. Kuwezesha utekelezaji wa Katiba mpya;
10. Kuimarisha usawa katika mgao wa rasilmali za nchi;
11. Kujenga utambulisho dhabiti unaofuma uanuai utakaounda mtagusano bora wa kitaifa; na
12. Uwekaji sawa wa vipengee vya Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (mwaka 2008).

## MADA 4: CHANGAMOTO KWA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za maagizo.

**Mbinu:** Majadiliano ya makundi na uigaji.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza wanaoshiriki ili kuziangazia changamoto za uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Wanaoshiriki wanajadili katika makundi changamoto za uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa mukhtasari maoni ya wanaoshiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Changamoto za Uwiano wa Kitaifa

Utafiti unaonyesha kuwa kuna uhusiano baina ya kutokuwepo kwa uwiano na kutokuwepo kwa usawa katika maisha. Hii inaweza kuwa kisiasa, kiuchumi au kitamaduni katika jamii.

#### Changamoto za Kisiasa

1. Ushawishi na utengaji katika makundi ya nchi kwa msingi wa kikabila hali inayoamua misimamo ya kisiasa na nafasi katika nchi;
2. Kutoaminiana na ubinafsi mionganini mwa viongozi;
3. Ukosefu wa msimamo na maoni yanayoamua mwelekeo wa kisiasa;
4. Uongozi dhaifu katika taasisi za maongozi;
5. Uchangamano katika uhamaji na maswala ya makazi;
6. Kukosa kushughulikia dhuluma za kijadi;
7. Kuenea kwa makundi haramu na wanamgambo; na
8. Usimamizi wa ardhi, mtaji wa kifedha, teknolojia na mawasiliano mionganini mwa viongozi wa kisiasa.

## Changamoto za Kiuchumi

1. Ukosefu wa usawa katika ufikiaji na usimamizi wa rasilmali chache kama vile fedha, ardhi, teknolojia na mawasiliano;
2. Ukosefu wa ubunifu katika uundaji wa mali;
3. Ukosefu wa mipangilio mahususi ya fedha za ustawi kama vile Fedha za Ustawi wa Maeneo bunge (CDF), Fedha za Mabaraza ya Miji (LATF);
4. Ufisadi wa kiwango cha mtu binafsi na asasi; na
5. Ustawi mdogo wa kibashara mionganoni mwa wafanyakazi wenye mapato machache.

## Changamoto za Kitamaduni-Jamii

1. Ukabila – usimamizi wa maadili na asasi pana za kitamaduni;
2. Ukabila mbaya – Ubinafsishaji wa kabilia;
3. Viwango vikubwa vya wasio na elimu;
4. Upungufu wa maadili na uadilifu – viwango vikubwa vya uhalifu, hofu ya uhalifu na tabia zisizokubalika katika jamii;
5. Ufifishwaji wa vitengo vya kifamilia;
6. Watu wengi wasio na matumaini ya kufaulu maishani – ukosefu wa kutambua mazuri yaliyomo katika nchi; na
7. Kutothamini tamaduni za wengine.



Picha 3: Kutafakari kuhusu jamii isiyo na uwiano

## MADA 5: MIENENDO YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 20.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za maagizo.

**Mbinu:** Uwasilishaji na majadiliano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza wanaoshiriki ili kuorodhesha sura mbalimbali za uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Wanaoshiriki wanaorodhesha katika makundi sura mbalimbali za uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu kunakili kwa mukhtasari maoni ya wanaoshiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Sura mbalimbali za Uwiano na Utangamano

Kuna sura mbalimbali za uwiano na utangamano. Hizi zinajumuisha:


1. Mikakati mahususi ya mawasiliano inayofaa kushirikisha vyombo vya habari vya nyanjani mionganini mwa njia nyinginezo katika jitihada za kupiga vita udunishaji wa makundi fulani na mienendo mingine mibaya.
2. Uongozi wenge maono unaozingatia utawala mzuri na unaounda maono ya taifa. Pia inahusisha utoaji wa uwezo kwa jamii kuititia kwa kuwashughulisha katika asasi zilizopo kwenye harakati ya mashauriano kutokea chini na kwenda juu.
3. Ushirikiano wenge manufaa na shughuli za 'mpito' ambazo zinataa kujumuisha wala hazifungiwi kwa:
  - a) Elimu: Shule ni vituo muhimu vya kujenga uhusiano na elimu ya kisiasa;
  - b) Michezo: Michezo siyo tu kumbi za kukutana bali pia huunganisha mataifa, nchi na huunda utangamano wa kihisia;

- c) Utamaduni ni utaratibu mahususi kwa taifa lenye mseto wa tamaduni ndogo kama vile makundi ya kikabila na kidini;
  - d) Shughuli za burudani na kujipumbaza;
  - e) Mazingira ya kikazi, miungano ya wafanyakazi, klabu za wafanyakazi kazini, shughuli za kuimarisha uhusiano, kuwa pamoja, mafunzo, n.k.;
  - f) Makao huwa maeneo muhimu ya kukutana. Makazi huunda aina fulani ya umoja na uwiano; na
4. Maeneo ya kujistarehesha kama vile mabustani, ufukweni, maeneo ya mazoezi ya mwili, mashamba ya kijamii, maeneo ya malisho ya mifugo katika jamii, maeneo ya pamoja ya kutekeea maji, kama vile visima, chini ya miti, kumbi za kijamii na vyama vya kuchangiana.
5. Nafasi za kazi baina ya ngazi za vizazi na dini
- a) Vilabu vya vijana, makundi ya ushirika, makundi ya kisiasa, n.k.;
  - b) Makundi ya wanawake kama vile yanayoshughulikia kujipatia mapato, makundi ya ushirika, klabu za wanachama, n.k.;
  - c) Makundi baina ya madhehebu kama vile Baraza la Kitaifa la Makanisa nchini Kenya (NCCK), Tume ya Kikatoliki ya Amani na Haki, Baraza la Kundu la Hindu la Kenya na Baraza la Wahubiri wa Kiislamu nchini Kenya mionganoni mwa mengine;
  - d) Jithada za kuimarisha amani, mikutano ya amani, n.k.; na
  - e) Majadiliano baina ya makundi yanayoleta pamoja dini zote katika utafutaji wa amani ya kudumu.
6. Ubainishaji wa jamii mbalimbali
- a) Ubainishaji wa jamii huhusisha ugavi wa rasilmali kwa njia inayostahili na tena kwa usawa;
  - b) Ubainishaji huu pia humaanisha uhusishaji wa makundi yote katika hesabu ya wananchi na kutoa data kuhusu sifa zao za kikabila;
  - c) Ni muhimu kutambua makundi ya watu yanayobadilika kila mara kama vile vijana, wanaume, wanawake, mapungufu ya kila aina na makundi mengineyo;
  - d) Uhamaji uchukuliwe kama sehemu mojawapo muhimu ya kuwepo kwa binadamu;

- e) Uhamaji pia unatambua kuwa wahamiaji wanastahili msaada wa serikali na usaidizi; na
- f) Jamii ngeni zinafaa kujumuishwa katika jamii kubwa kulingana na sheria za nchi.

7. Kuzuia shida zinazotarajiwa

- a) Shida zinazotarajiwa zinafaa kuzuiwa kupitia kwa utatuzi wa mgogoro na mipangilio;
- b) Muitiko wa mizozo kwa wakati huzuia athari nyingi. Hii inaweza kupatikana kupitia kwa mifumo ya kijamii ya kijasusi na kiufuatilizi;
- c) Kuna haja ya kuwa na mikakati ya kukabili majanga;
- d) Mikakati ya uzuiaji na kudhibiti wa mgogoro inafaa kusambazwa kwa raia wote; na
- e) Aina zote za makundi yenyе msimamo mkali na yasiyo halali katika taifa kama vile makundi ya kiusalama na wanamgambo yanafaa kudhibitiwa.



Jedwali 2: Taswira ya Uwiano na Utangamano

## Marejeleo

- Alesina A. and E. La Ferrara (2004) 'Ethnic Diversity and Economic Performance' National Bureau of Economic Research WP 10313
- Atieno-Odhiambo E.S., (2002) 'Hegemonic Enterprises and Instrumentalities of Survival: Ethnicity and Democracy in Kenya', African Studies, Vol. 61, No. 2, 223-249
- Bollen K. A. and Hoyle R. H., (1990) A Conceptual and Empirical Examination. USA: University of North Carolina Press
- Council of Europe (2005) Concerted Development of Social Cohesion Indicators: Methodological Guide. Belgium: Council of Europe
- Dion Forster, (2007) The Impact of Knowledge Systems on Human Development in Africa (Pretoria: University of South Africa
- Eghosa E. Osaghae,(1999) 'Democracy and National Cohesion in Multiethnic African States: South Africa and Nigeria Compared' Nations and Nationalism, Volume 5, Issue 2, pages 259–280
- Equality Team (2008) Cohesion and Integration Priorities 2008 – 2011, Leeds Council City Leeds. [www.leeds.gov.uk/](http://www.leeds.gov.uk/)
- Dion Forster, (2007) The Impact of Knowledge Systems on Human Development in Africa (Pretoria: University of South Africa
- Eghosa E. Osaghae,(1999) 'Democracy and National Cohesion in Multiethnic African States: South Africa and Nigeria Compared'
- Nations and Nationalism, Volume 5, Issue pages 259–280
- Equality Team (2008) Cohesion and Integration Priorities 2008 – 2011, Leeds Council City Leeds. [www.leeds.gov.uk/](http://www.leeds.gov.uk/)
- Rothchild and V. A. Olorunsola, editors State Versus Ethnic Claims: African Policy Dilemma Westview Press: London pages 67-84
- Jackson R.H. and C.G. Rosberg, (1982) 'Why Africa's Weak States Persist: The Empirical and the Juridical in Statehood' World 1-24.

- Leonardi Robert (1995) Convergence, Cohesion and Integration in the European Union. New York, NY: St. Martin's Press
- Leopold Senghor, (1964) On African Socialism. London: Pall Mall Press
- Institute of Community Cohesion, (2010) Community Cohesion is an Important Contributor to Health. USA: Equality and Human Rights Commission
- Maathai Wangari, (2009) The Challenge for Africa: A New Vision London: Heinemann
- Mazrui Ali, (1970) 'The Monarchical Tendency in African Political Culture' in M. Doro and N. E. Stultzds (Eds) Governing in Black Africa. Englewood Cliffs, N.J.: Prentice Hall
- Miguel E., (2004) 'Tribe or Nation? Nation-building and Public Goods in Kenya versus Tanzania' World Politics, Vol. 56 Issue No. 3 pages 327-362
- Osberg H., (2003) The Economic Implications of Social Cohesion. Canada: University of Toronto Press
- Regina Berger-Schmitt, (2000) Social Cohesion as an Aspect of the Quality of Societies: Concept and Measurement. EU Working Paper No 14. Mannheim: Centre for Survey and Methodology (ZUMA)

## SOMO LA 2: HALI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanafaa kuikubali hali halisi ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

### UTANGULIZI

Somo hili linashughulikia jitihada zilizofanywa kutokea enzi za uhuru hadi mwaka wa 2007 kwa lengo la kuimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa humu nchini. Somo hili linaangazia changamoto zilizopatikana na muingiliano uliofanyika ili kuunda taifa lenye uwiano na utangamano. Ni muhimu kwa washiriki kuyafahamu masharti yaliyoendeleza au kuzuia kuishi kwa pamoja kwa jamii mbalimbali na yanayoweza kuathiri maisha yao ya baadaye.

### MADA 1: JITIHADA ZILIZOFANYWA ILI KUPATIKANA KWA UWIANO NAUTANGAMANO WA KITAIFA TOKEA UHURU (1963) HADI MWAKA 2007

**Muda:** Dakika 30

**Vitendea-kazi:** Chati, kalamu za wino, daftari na kalamu, Katiba, Ramani ya Kenya, mpango maalum wa Wizara ya Haki, kijitabu cha Rajua ya 2030, Kanda za video na Makala Maalumu.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kueleza kwa **muhtasari** jitihada zilizofanyika ili kupatikana kwa uwiano na utangamano wa kitaifa tangu enzi ya uhuru (1963) hadi mwaka wa 2007.
- Washiriki waelezea hatua za majoribio ya matukio yanayohusiana na uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Mwelekezi anatumia mbinu za kimuhtasari ili kuonyesha maoni ya washiriki.

Chemsha bongo



## Maelezo Muhimu

Hatua zifuatazo na shughuli zinadhihirisha jitihada za nchi ili kufanikisha uwiano na utangamano wa kitaifa:

1. Sherehe za maadhimisho ya siku ya uhuru yanayofanyika kila mwaka tangu mwaka wa 1963;
2. Waraka rasmi nambari 10 wa mwaka wa 1965 kuhusu ujamaa wa Kiafrika na utekelezaji wa Maendeleo ya Kiuchumi Kenya;
3. Jitihada za awali za serikali za mipango ya miaka mitano ya maendeleo ya kitaifa;
4. Harambee na filosofia ya Nyayo;
5. Uzingatiaji wa Maendeleo ya nyanjani ya tarehe 1 Julai 1983;
6. Kuanzishwa kwa wingi wa mifumo ya kisiasa;
7. Mikakati ya kupunguza umaskini wa mwaka wa 2001 hadi 2003;
8. Mikakati ya kufufua uchumi mwaka wa 2003 hadi Desemba 31, 2007;
9. Rajua ya Kenya ya 2030, mpango kamili wa maendeleo wa Januari 1, 2008;
10. Katiba ya Kenya ya 2010;
11. Sera ya kitaifa ya ardhi; na
12. Tume za Ajenda ya 4 (TJRC, CoE, IIBRC, IICDRC, NCIC, IIEC, CIC).



Picha 4: Maadhimisho ya siku ya kitaifa

## MADA 2: CHANGAMOTO KATIKA KUFANIKISHA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA NCHINI KENYA

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea kazi:** Chati, kalamu za wino, daftari na kalamu, Katiba, Ramani ya Kenya, mpango maalum wa Wizara ya Haki na kijitabu cha Rajua ya 2030, Kanda za video na Makala Maalum.

**Mbinu:** Maswali kwa Majibu, miigo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kutaja changamoto zilizoko ili kufikia uwiano na utangamano wa kitaifa nchini Kenya.
- Washiriki wanaweka wazi changamoto ili kupata uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Mwelekezi anatumia mbinu za kimuhtasari ili kuonyesha maoni ya washiriki.

Chemsha bongo



### Maelezo Muhimu

#### 1. Changamoto za kiuchumi

- (a) Ugawaji wa ardhi baada ya Kenya kupata uhuru
- (b) Uungwaji mkono wa kisiasa katika ugavi wa rasilimali za kitaifa
- (c) Ufisadi
- (d) Ugavi usio sawa wa rasilimali za kitaifa


#### 2. Changamoto za kisiasa

- (a) Mauaji ya kisiasa yaliyofanyika miaka ya 1965, 1969, 1975, 1991, 2005
- (b) Taifa kurejelea mfumo wa chama kimoja tarehe 3 Juni, 1982
- (c) Mapinduzi ya kijeshi ambayo hayakufaulu ya mwaka wa 1982
- (d) Harakati za kupigania kuwepo kwa vyama vingi (sabasaba)

- (e) Kurejelea demokrasia ya mfumo wa vyama vingi
- (f) Vita vya kikabila na ardhi kuanzia mwaka wa 1991 na ghasia za kisiasa wakati wa uchaguzi
- (g) Mchakato wa ICC
- (h) Kutolewana kisiasa
- (i) Harakati za kuwepo kwa mabadiliko ya katiba
- (j) Kusakwa kwa wapinzani wa serikali
- (k) Kuingiza ukabila katika huduma za umma
- (l) Tishio kutoka kwa wanamgambo na makundi ya uhalifu
- (m) Machafuko ya uchaguzi ya mwaka wa 2007/2008
- (n) Wakimbizi wa ndani ya nchi

### **3. Changamoto za kijamii/kitamaduni**

- (a) Mfumo gawanishi wa kielimu (unaozingatia kujumuishwa kwa robo ya wanafunzi kieneo) katika shule za kwao
- (b) Mifumo dhaifu ya kuendeleza maadili ya kitaifa
- (c) Mazoea ya tamaa na ubinafsi
- (d) Mielekeo ya kiubabe/kiuduni katika jamii
- (e) Mielekeo hasi ya kikabila
- (f) Desturi hasi za kimila
- (g) Kutokuwa na usawa wa huduma za kijamii



Picha 5: Changamoto za kufanikisha uwiano na utangamano wa kitaifa nchini Kenya

### MADA 3: JUHUDI ZA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 40.

**Vitendea-kazi:** Chati, kalamu za wino, madaftari, kalamu, Katiba, Ramani ya Kenya, mpango maalum wa Wizara ya Haki na kijitabu cha Rajua ya 2030, Kanda za video na Makala Maalum.

**Mbinu:** Majadiliano ya makundi na uwasilishaji.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki ili kutambua **jithada** za kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wanaweka wazi jithada za kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Mwelekezi anatumia mbinu za kumuhtasari ili kuonyesha maoni ya washiriki.



#### Maelezo muhimu

##### Jithada za Kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.

###### 1. Ajenda ya nne ya majadiliano ya kitaifa na maridhiano nchini Kenya

(a) Ajenda ya nne inayolenga kuleta pamoja uwiano na utangamano wa kitaifa.

(b) Kuanzishwa kwa mpango wa kumaliza ugomvi, maridhiano, uwiano na utangamano wa kitaifa.

(c) Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (TJRC).

(d) Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC).

(e) Kamati ya Kitaifa ya kuleta amani na kusuluuhisha mzozo (NSC).

(f) Idara ya Uwiano wa Kitaifa (DNC).

## 2. Rajua ya Kenya ya mwaka 2030: Mpango Kamili wa Maendeleo

Katika nguzo ya kisiasa, Rajua hii inatilia mkazo usalama, kuleta amani, kudhibiti mafarakano na maamuzi.


### 3. Katiba ya Kenya ya 2010

Katiba ilizinduliwa rasmi tarehe 27 Agosti, mwaka wa 2010. Inatoa mazingira bora kwa raia wote kuishi kwa maelewano. Itakapotekelezwa kikamilifu, inatajarajiwa kwamba taifa zima litakuwa na uwiano na utangamano wa kitaifa. Ili kufupisha maelezo zaidi ya jinsi katiba inavyoboresha uwiano na utangamano wa kitaifa yameelezwu kwenye somo la 4 kuhusu sera, sheria na muundo wa uwiano na utangamano wa kitaifa.

### 4. Sera na Miongozo

Uundaji wa sera na miongozo unatarajiwa kuboresha uwiano na utangamano. Baadhi ya sera hizi ni pamoja na:

- (a) Sera ya Utangamano na Uwiano wa Kitaifa.
- (b) Sera ya Kuleta Amani na kusuluhisha mizozo.
- (c) Sera ya Kitaifa ya Ardhi na n.k.



Picha 6: Jitihada za kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa

**Marejleo**

- CCR, (2010) Transitional Justice: A hand book. Nairobi: CCR
- Government of Kenya, (2008) The National Cohesion and Integration Act 2008. Nairobi: Government Printer
- Government of Kenya, (2008) The Truth, Justice and Reconciliation Act, 2008. Nairobi: Government Printer
- Government of Kenya, (2010) The Constitution of Kenya Nairobi: Government Printer
- Machira Apollos, (2009) Armed conflicts and the Law. Nairobi: Aluka Publications
- Machira Apollos, (2009) TJRC Process: A hand book. Nairobi: CCR

## SOMO LA 3: MIKAKATI YA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wataweza kutumia mikakati mbalimbali ili kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.

### UTANGULIZI

Somo hili linatoa maana ya dhana ya mikakati. Linajadili mikakati mbalimbali inayoendeleza utangamano na uwiano wa kitaifa na kuangazia majukumu ya watenda kazi mbalimbali. Pia linaangazia mbinu na shughuli za kuendeleza uwiano wa kitaifa.

### MADA 1: MKAKATI

**Muda:** Dakika 20.

**Vitendea kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za kufundishia.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kueleza maana ya neno mikakati likihusishwa na maendeleo ya uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wanaelezea maana ya mikakati.
- Mwelekezi anatumia hoja kuu kwa muhtasari ili kuonyesha maoni ya washiriki.



### Maelezo Muhimu

#### Maana ya Mikakati

Mikakati ni mbinu au mipango inayotumika ili kuleta matokeo yanayotarajiwa, kama vile kufikia lengo au suluhisho la tatizo. Ni mpango unaochukua kipindi kirefu ili kufikia lengo au shabaha fulani.

#### Matumizi ya mikakati ya uwiano na utangamano.

1. Kuwa na utamaduni mmoja mahususi unaotokana na tamaduni ndogo ndogo za kitaifa ambao pia huitwa mshikamano wa tamaduni (kujumuisha mila ndogo za kitaifa kwa mila moja kuu ya kujitambulisha au kwa tabia na mwelekeo wa kisiasa wa kundi kubwa la kikabila kufanya mila iwe dhabit (kuzoesha mila za sehemu za nchi kwa kiwango fulani au kwa tabia na shirikisho la kisiasa na mila za kabilalenyenye mashiko).
2. Vitambulisho vingi (vinavyojulikana pia kama umoja katika uanuai).

## MADA 2: MIKAKATI YA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za kufundishia.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kuchunguza **mikakati** ya kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wanaeleza mikakati ya kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Mwelekezi anatumia hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki.



### Maelezo Muhimu

Kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa huhitaji mikakati ya kimakusudi ili kulainisha udhibiti wa uanuai nchini Kenya. Mikakati ambayo inaweza kutumiwa kuendeleza uwiano wa kitaifa ni kama:

#### 1. Kuimarisha Asasi Muhimu za Utawala

Ipo haja ya kuimarisha mashirika, asasi za kijamii na mbinu za utawala ili kuendeleza uwiano wa kitaifa. Mageuzi ya asasi za kisiasa na utawala kama vile, Halmashauri kuu, bunge, mahakama, huduma za umma, serikali za mitaa, utawala wa umma, sheria za uchaguzi na uhusika katika chama ni muhimu hasa katika kutimiza uwiano na utangamano wa kitaifa. Mikakati maalum ya kufikia malengo haya inaweza kuhusisha yafuatayo:

(a) Kuteua dhana anuai katika viwango vyote vyaya uongozi wa mashirika katika mifumo ya umma na ya kibinagsi.

Ipo haja ya kutoa mwongozo muhimu utakaohakikisha kuwa kanuni za uwiano zitahusishwa katika wizara, idara na mashirika yote katika sekta za umma. Mashirika ya kibinagsi lazima yahakikishe yamehusisha uwiano wa kitaifa kwenye asasi zao husika hasa katika kuajiri, kupandisha vyeo na kuwabakiza waajiri.

- (b) Kuanzishwa na kuboreshwa kwa vikao vya mazungumzo ya jamii mbalimbali, kuanzisha na /au kuongezea vikao vya mazungumzo mionganoni mwa jamii kama vile, kuwepo kwa warsha na mabaraza ni muhimu. Hali hii hutoa nafasi kwa watu binafsi na wanajamii kujadili maswala nyeti na kutafuta suluhisho kwa matatizo yanayoathiri uwiano na utangamano wa kitaifa.
- (c) Kuimarisha wajibu wa viongozi wa nchi, kaunti na jamii katika kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa. Viongozi wa jamii na mifumo ya jadi inayoendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa kama vile mabaraza ya wazee yanafaa kutambuliwa na kuungwa mkono.
- (d) Kuboresha matumizi ya mitalaa ya elimu pamoja na elimu ya uraia ili kuendeleza uwiano wa kitaifa.

Mfumo wa elimu wa mgao unafaa kuundwa upya ili kuwezesha utangamano wa wanafunzi kutoka makabila mbalimbali na vikundi vya kijamii na maeneo/kaunti. Zaidi ya hivyo, kuimarisha kwa elimu ya uraia kuititia mahusiano ya umma na ya kibinafsi katika kutambua uanuwai kutapunguza migawanyiko, kusaidia kubadilisha mielekeo ya watu na kuimarisha uzalendo.

Kwa upande mwingine, kutekelezwa vilivyo na kwa wakati ufaao kwa Katiba kutamaliza mipango ya sasa ya asasi tepetevu na zisizo thabiti na matendo yasiyofuata Katiba kulingana na uongozi wa kitaifa na maswala ya umma.

- (e) Kutekelezwa na kuboreshwa kwa sheria inayohusu mashtaka ya watu binafsi au vikundi vinavyochochea ukabila hasi na matamshi ya chuki nchini Kenya.

Watu wanaotoa matamshi yanayochochea ukabila hasi na kauli za chuki wanafaa kuripotiwa na kushtakiwa bila kujali kabilalao au hadhi yao katika jamii. Jamii hazifai kuwakubali watu kama hao na badala yake ziwakemee kwa kuchochea uhasama dhidi ya jamii nyingine. Vyombo vya habari navyo visiwapigie debe watu kama hao.

- (f) Kukubali uanuai na alama za umoja wa kitaifa.

Msisitizo unafaa kuwekwa chini ya mamlaka ya watu, usimamizi unaofaa wa lugha asili, alama za kitaifa, wimbo wa taifa, sikukuu za kitaifa, maadili ya kitaifa na kanuni za utawala mionganoni mwa mengine.

- (g) Kuendeleza huduma jumuishi za umma au sekta za umma zinazoakisi uanuai nchini Kenya.

Nafasi za huduma za umma zinafaa kuwakilishwa na makabila yote. Uamuzi wa dhati utekelezwe ili kuboresha uhusishwaji wa walio wachache na makundi yaliyotelekezwa.

- (h) Kuunda na kufuatilia jazi za viashiria na vionyeshi vinavyobainisha wajibu wa asasi za utawala ili kuboresha uwiano.

Viashiria hivi ni pamoja na: Utawala wa kidemokrasia, uzingatiaji wa kanuni za sheria, kupunguza ufisadi, haki na usalama wa binadamu pamoja na kuendeleza mifumo ya kimaadili na sera za umma.

## **2. Kushughulikia Tofauti zilizopo katika Maswala ya Kijamii na Kiuchumi.**

Nchini Kenya kuna tofauti mbalimbali za kimaeneo na kikabila kama vile kukosa kupata elimu na mafunzo, katika maeneo fulani, maji, usafi wa mazingira, huduma za kiafya na makazi mionganoni mwa mengine. Mifumo hii ya kutokuwepo kwa usawa husababisha hisia za kutengwa katika jamii na huenda zikaonekana kama njia za udhibiti mbaya wa kiuanuai, licha ya mambo haya kuwa kizuizi cha uwiano wa kitaifa.

Tofauti ndani na kati ya maeneo zimehusishwa na hisia za kutengwa mionganoni mwa Wakenya wengi. Ili kushughulikia utofauti huu wa kimaeneo na kiuchumi-jamii, mikakati ifuatayo ni muhimu ihusishwe:

- (a) Kuharakisha maendeleo ya maeneo maalum ya kiuchumi ili kuboresha hadhi ya kiuchumi na kijamii katika maeneo ambayo hayajaendelea.

Ni muhimu kwa maeneo haya ambayo hayajaendelea kuboreshwaa kuptitaa kwa uwekezaji wa kimuundomsingi na kiviwanda. Serikali inafaa kuhakikisha kuna maendeleo sawa ya kimuundomsingi katika nchi nzima huku ikitilia mkazo maswala ya barabara, umeme, maji na usafi wa mazingira mionganoni mwa mambo mengine.

- (b) Kugatua kiasi fulani cha rasilimali za serikali kwa kaunti kwa njia yenyewe usawa na uwazi.

Maeneo yaliyotelekezwa yashughulikiwe kikamilifu kuptitaa kwa hazina ya usawazishaji ili yafikie viwango sawa na maeneo mengine ya nchi.

- (c) Kuwezesha uwekezaji sawa katika huduma za kiuchumi na kijamii, elimu, asasi za mafunzo, huduma za afya, chakula, usalama na maji kati ya mambo mengine.

Kuhakikisha kufikiwa kwa haki muhimu za kimsingi za kibinadamu kama vile elimu ya msingi, huduma za afya, maji na uhakika wa kupata chakula.

- (d) Kuboresha usimamizi wa shughuli za ardhi na changamoto zinazohusiana na usimamizi mbaya/ugavi wa rasilimali.

Kwa sababu migogoro mingi nchini Kenya hutokana na ardhi na usimamizi mbaya wa rasilmali, kuna umuhimu wa kuboresha shughuli za usimamizi wa ardhi na kushughulikia kutokwepo kwa usawa katika ugavi wa ardhi na usimamizi mbaya wa rasilmali.

- (e) Kushughulikia ukosefu wa ajira kwa vijana na aina nyingine za kutengwa kiuchumi na kijamii.

Uchumi unafaa kuboreshwa kwa lengo la kuwezesha kuundwa kwa nafasi nyingi za kazi. Vijana wapewe mafunzo yatakayowapa ujuzi na mtaji unaofaa ili kuzalisha mali na kuweza kujitegemea.

### **3. Usimamizi wa Uanuai wa Kikabila, Kitamaduni na Kijamii.**

Utamaduni una nafasi muhimu na jukumu la kimsingi katika kuendeleza utambulisho na uhakika wa usalama katika kuongoza tabia ya mtu binafsi. Vyombo vya utamaduni husaidia kuwaleta watu pamoja ilhali kushiriki kwao katika shughuli za kitamaduni huhakikisha kuwa maswala muhimu ya kitaifa yamepewa hadhi huku ujumbe wa utangamano ukiwasilishwa na hivyo basi kuimarisha kuishi kwa pamoja na kwa heshima.

Ili kuimarisha wajibu wa utamaduni na turathi katika kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa, mikakati ifuatayo inaweza kutumiwa:

- (a) Kutumia maonyesho ya kitamaduni kama vile ngoma, muziki, michezo ya kuigiza na michezo mingine ili kujenga uwiano na utangamano wa kitaifa mionganoni mwa jamii.

Michezo ya kitamaduni na sanaa, hususan ile inayohusishwa na matukio maalum na sikukuu za kitaifa, inafaa kusisitiziwa ili kuchangia katika uwiano na utangamano wa kitaifa.

- (b) Kutumia vyombo vya habari na shughuli za kitamaduni kama vile sanaa, muziki, sinema na filamu ili kutangaza ujumbe wa amani na kuishi vizuri kwa pamoja.

Vyombo vya habari vinafaa kutumiwa ili kuendeleza shughuli mbalimbali za kitamaduni zinazohimiza na kuunga mkono uwiano na utangamano wa kitaifa.

- (c) Kuanzisha na kuunga mkono vituo vya kiutamaduni katika maeneo bunge/kaunti.

Vituo vya kijamii vya kiutamaduni vitatumika kama maeneo ya kuendeleza mazungumzo mionganoni mwa watu wa tamaduni mbalimbali, uwiano wa kitaifa na kuwasilisha turathi za kitamaduni. Turathi hizo basi zitahimiza wingi wa utamaduni katika jamii.

#### 4. Maridhiano, Usuluhishaji na Uzuiaji wa Mizozo

Maridhiano, usuluhishaji na uzuiaji wa mizozo ni muhimu katika uendelezaji wa uwiano wa kitaifa. Jitihada zinahitajika kufanywa ili kushughulikia uzuiaji wa mizozo ili kudumisha amani na kutafuta suluhu mionganii mwa jamii zinazozozana. Haya yanawezekana kufikiwa kupitia kwa mikakati ifuatayo:

- (a) Kuunda mifumo ya usuluhishaji wa mizozo na kuleta maridhiano;
- (b) Kuandalia makundi yanayozozana vikao vya mazungumzo vilivyo salama na vilivyo andaliwa kwa usimamizi bora na wa kitaalamu ili kufanikisha mazungumzo, usuluhishaji wa mizozo na upatikanaji wa maridhiano;
- (c) Kuwahuisha watalaamu wa kuendeleza amani wenye maarifa na mbinu ili kufikia uzuiaji na udhibiti wa muda mrefu wa migogoro; na
- (d) Kuendeleza mafunzo ya amani kwa kutumia makundi yenye ushawishi katika maeneo yanayoweza kukumbwa na mafarakano. Mafunzo hayo yanalenga kuhamasisha kutotumia nguvu kutatua mafarakano, hivyo basi kuimarisha amani.

### MADA 3: WAHUSIKA KATIKA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, madaftari, kalamu na kanda za kufundishia.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano ya vikundi.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki ili kuwataja wahusika wanaoshughulikia uendelezaji wa uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wanataja wahusika hao.
- Mwelekezi anatumia hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki.



#### Maelezo Muhimu

##### 1. Serikali

Serikali hutoa uongozi wenye maono kuitia kwa utawala. Unaimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa katika sera za kitaifa na kuunda mtazamo mmoja ili kuleta muamana na uwiano wa kitaifa. Hata hivyo, serikali inafaa kuimarisha asasi muhimu zinazotekeliza wajibu kama upangaji, uundaji na uratibu wa sera, uelekezaji, utekelezaji, udhibiti na ukaguzi wa uwiano na utangamano wa kitaifa.

##### 2. Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba

Wizara huratibu shughuli za uwiano na utangamano wa kitaifa kuitia upangaji, uundaji na uratibu wa sera, uelekezaji, utekelezaji, udhibiti, ukaguzi na utathmini na uwasilihishaji wa repoti kuhusu maendeleo ya shughuli hizo. Wizara pia huhakikisha mtazamo jumuishi wa uwiano na utangamano wa kitaifa ambao huchangiwa na washikadau mbalimbali.

### **3. Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC)**

Jukumu la Tume ni pamoja na kuondoa ubaguzi wa kikabila, rangi, dini ama asili ya kijamii, kuwezesha jamii zote kushiriki katika maswala ya kitaifa na kuunga mkono amani na upatanifu mionganoni mwa jamii na rangi mbalimbali.

### **4. Vijana**

Vijana ndio rasilmali muhimu ya maendeleo ya kitaifa na mabadiliko ya kijamii. Ndio wengi na kundi lenye nguvu katika nchi, hivyo basi, ni wahusika muhimu wanaoweza kubaini hatima ya nchi. Ndiposa kuna haja ya kuwashirikisha katika mipango yote inayolenga muamana na maridhiano ya kitaifa. Vijana wanafaa kupewa ari, kutiwa nguvu na kupewa motisha ili washiriki katika viwango vyote vya maendeleo kisiasa, kijamii na kiuchumi, katika kупинга maovu ya kijamii kama vile mielekeo mibovu ya kikabila, upendeleo na ghasia.

### **5 Makundi ya wanawake**

Bidii inayofanywa na wanawake katika shughuli za kuleta uwiano ni kama kichocheo cha maendeleo katika jamii. Nguvu zao, ubunifu, sifa na mwelekeo wao hubaini hatua za maendeleo ya taifa. Kupitia kwa vipawa vyao vya ubunifu na nguvu zao za kazi, taifa hupiga hatua kubwa katika uchumi na maendeleo ya kisiasa na kijamii. Wanawake huchangia katika utatuzi wa migogoro, kuleta amani, uwiano na utangamano wa kitaifa.

### **6. Vyombo vya habari**

Magazeti na vyombo vya elektroniki vina jukumu kubwa katika kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa kupitia kuwajibika vyema kwa uanahabari. Hii inaweza kupatikana kwa kuangazia mitindo mizuri ya kuripoti na kusitiza maswala ya kitaifa dhidi ya maswala ya ubaguzi kama vile siasa za kikabila.

### **7. Wazee wa jamii**

Wazee wa jamii wana jukumu la kufundisha maadili mema yanayokuza uongozi, utawala mwema na uwiano. Wazee wa jamii wanafaa kuhimiza na kusaidia jamii kuzingatia maadili ya uadilifu, uaminifu, unyenyekevu, bidii, uzalendo, huduma kwa jamii na kujitolea kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa.

### **8. Viongozi wa kisiasa**

Uongozi imara na utendaji kazi ni muhimu katika kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa. Uongozi wenye maono ya kudumisha dhana ya umoja katika uanuai kutoa mwelekeo mzuri wa shughuli za uwiano katika jamii.

## 9. Mashirika ya Kidini (FBOs)

Mashirika ya kidini yana mchango mkubwa katika kuleta amani na hufanikisha utekelezaji wa miradi ya amani. Yanachangia pakubwa katika kutatua migogoro, kuleta amani na kukuza uwezo kwa ajili ya amani na hatua za maridhiano. Mashirika ya kidini yana uwezo wa kukuza rasilimali ambayo ni jamii na kuchangia zaidi katika uwiano wa jamii nchini Kenya.

## 10. Mashirika ya Kijamii (CBOS)

Mashirika ya kijamii huendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa kwa kuhimiza wenyiji kushiriki katika shughuli mbalimbali ambazo zinasaidia katika udhibiti wa uanuai wao. Kupitia shughuli zao nyingi mashinani, yanasaidia jamii mbalimbali kutangamana na kupata suluhisho la kuishi pamoja kwa amani, hivyo basi kuacha njia potovu za kugawanya na kutenga jamii zingine.

## 11. Vikosi vya Usalama na Ulinzi

Vikosi vya ulinzi hudumisha amani na usalama, jambo muhimu katika kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa. Vikosi vya ulinzi na usalama huendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa kwa kutoa huduma za usalama kwa jamii zote kwa usawa bila ubaguzi. Pia hufanya miradi ya ujenzi wa uwiano katika jamii mbalimbali.

## 12. Shule na Vyuo

Shule na vyuo huhimiza kutangamana pakubwa mionganoni mwa wanafunzi kutoka katika makabila na makundi ya kijamii, maeneo na kaunti mbalimbali. Hutayarisha nafasi nzuri ya kujenga utambuzi wa uanuai wao, kuondoa mitazamo mibaya kuhusu wengine, kusaidia kubadilisha mielekeo na kuendeleza uaminifu na uzalendo kwa taifa.

## 13. Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali (NGOS)

Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yamejihuisha katika shughuli zinazosaidia kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa. Hii ni pamoja na kuwapa makao watu waliohamishwa kutoka makwao, suluhisho la migogoro, ujenzi wa amani na kuhamasisha maswala yanayohusiana na uwiano wa kitaifa. Hayaelimishi kuhusu changamoto zinazoikumba jamii zilizotelekezwa nchini na pia husaidia katika maendeleo ya maeneo yaliyotelekezwa.

## 14. Sekta ya Kibinafsi

Sekta ya kibinafsi imeathirika vibaya kwa kukosa uwiano na hivyo basi ina haja na jukumu kuu la kutekeleza katika kuhakikisha uwiano wa kitaifa umepatikana. Sekta hii inafaa kuhimizwa kuchukua na kutekeleza kanuni zinazoendeza uwiano na

utangamano wa kitaifa kwa wanachama wake. Sekta ya kibinafsi inaweza kutumika kama mshirika mkuu wa serikali ili kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.


### 15. Wafadhili na Mashirika ya Kimataifa

Wafadhili na mashirika ya kimataifa hutoa fedha za ujenzi wa amani. Pia hutoa nafasi za ushirikiano, misaada ya kiufundi, habari kuhusu amani, suluhisho la migogoro na uwiano na utangamano wa kitaifa.

#### Mbinu na shughuli za kutekeleza uwiano wa kitaifa

Uwiano na utangamano wa kitaifa unaweza kuendelezwa kwa kuimarisha uwezo wa wanajamii katika kutangamana, kuelewa na kufanya kazi na jamii zingine. Mbinu na shughuli ambazo zinaweza kutumika ili kuendeleza uwiano wa kitaifa ni pamoja na:

- (a) Michezo ya pamoja kama vile riadha, kabumbu, mpira wa nyavu, mpira wa kete n.k.;
- (b) Ushirika wa kijamii na kutembeleana baina ya jamii ili kufahamiana na kujifunza miongoni mwao;
- (c) Faida za pamoja katika uekezaji na miradi ya kibiashara;
- (d) Sherehe za pamoja za kitamaduni na shughuli kama vile tamasha, sherehe n.k.;
- (e) Sherehe za kitaifa na kimaeneo kama vile sikukuu za kitaifa na matukio muhimu ya kimaeneo;
- (f) Miradi ya ufadhili katika jamii kupitia makanisa na mashirika yasiyo ya kiserikali; na
- (g) Kazi za kujitolea kupitia makundi kama vile maskauti wa kiume na wa kike makomando na wengine.



Jedwali 3: Wahusika katika Kuendeleza Uwiano na Utangamano wa Kitaifa

## MAREJELEO

- Ali Mazrui, (1972) Cultural Engineering and Nation-building in East Africa. Evanston: Northwestern University Press
- Amitai Etzioni, (1965) Political Unification: A Comparative Study of Leaders and Forces. New York: Holt, Rhinehart NS Winston Inc
- Nik Abdul Rashid bin Nik Abdul Majid, 'Understanding National Integration for Development', mimeo pages 3-4
- Ozonnia Ojielo, (2010) 'A Shared Future: Approaches To National Cohesion And Integration', Amani Papers, UNDP, Kenya. Volume I No 3

## SOMO LA 4: MUUNDO WA KISERA, KISHERIA NA KIASASI KWA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wataweza kuikubali sera, muundo wa kisheria na kiasasi ambamo uwiano wa kitaifa umejengwa.

### UTANGULIZI

Vyombo vyta kisheria hutoa muundo unaoongoza mahusiano mbalimbali katika jamii. Vyombo hivi ni pamoja na Katiba, Sheria za bunge, sera, makubaliano, mikutano, mikataba na maafikiano. Ni kuitia kwa vyombo hivi ambapo taasisi mbalimbali hupata uwezo wao na wajibu ili kuhakikisha kuwepo kwa taifa lenye uwiano. Mfumo huu hata hivyo unatilia mkazo umuhimu wa kushirikiana kwa karibu kati ya Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba, Tume ya Uwiano na Utangamano wa kitaifa, Wizara ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Ndani, Wizara ya Elimu, Wizara ya Maswala ya Vijana na Michezo mionganini mwa washikadau wengine muhimu.

### MADA 1: UFAFANUZI WA MANENO “SERNA, MUUNDO WA KISHERIA NA KIASASI”

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati, kalamu za wino, madaftari na kalamu, Katiba ya Kenya 2010, Kijitabu cha Rajua ya 2030 na sera nyingine zifaazo, Sheria ya uwiano na utangamano wa kitaifa ya 2008, Sheria ya Ukweli, Haki na Maridhiano ya 2008 pamoja na Sheria zingine za Bunge, Makubaliano ya Kimataifa, Mikataba na maafikiano yanayohusiana na uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kufafanua maneno, ‘serna, sheria na muundo wa Kiasasi’ kwa ajili ya uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wajaribu kueleza maana ya maneno haya.
- Mwelekezi atumie maeleo muhimu katika kujumuisha maoni ya washiriki.



Chemsha bongo

## Maelezo muhimu


### Maana ya Sera, Sheria na Muundo wa Kiasasi

#### 1. Sera

Sera ni kanuni za msingi ambazo huongoza serikali. Haya ni malengo yaliyowekwa ambayo serikali au taasisi inahitaji kudumisha na kuhifadhi kwa manufaa ya jamii kitaifa.

#### 2. Muundo wa Kisheria na Kiasasi

Muundo wa Kisheria na Kiasasi ni mfumo wa sheria, taratibu na miongozo inayoiimarishwa kupitia taasisi za kijamii zinazodhibiti tabia. Mfumo wa sheria, masharti na taratibu unaoendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa ni vigumu kuufikia kwa sababu ya wingi wake na vile vile kwa sababu ni swala ngumu kulitungia sheria.



Picha ya 7: Stakabadhi za Kisheria na sera za Uwiano na Utangamano

## MADA 2: SERA ZINAZOENDELEZA UPATIKANAJI WA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

### Muda: Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati, kalamu za wino, madaftari na kalamu, Katiba ya Kenya 2010, Kijitabu cha Rajua ya 2030 na sera nyingine zifaazo, Katiba ya Kenya 2010, Sheria ya uwiano na utangamano wa kitaifa ya 2008, Sheria ya Ukweli Haki na Mapatano ya 2008, pamoja na sheria zingine za Bunge, sera, Makubaliano ya Kimataifa, Mikataba na Maafikiano yanayohusiana na uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kutambua sera zinazoendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wajaribu kutambua sera hizo.
- Mwelekezi anatumia maelezo muhimu na kujumuisha maoni wa washiriki.



### Maelezo muhimu

Sera zinazoendeleza upatikanaji wa uwiano na utangamano wa kitaifa:

- a. Sera ya Ardhi ya Kitaifa;
- b. Sera ya kuleta amani na udhibiti wa mizozo;
- c. Sera ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa;
- d. Sera ya Jinsia;
- e. Sera ya Vijana; na
- f. Sera ya Ulemavu.

### MADA 3: VIPENGELE VIKUU VYA KIKATIBA VINAVYOWEZESHA UPATIKANAJI WA UWIANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 60.

**Vitendea-kazi:** Chati, kalamu za wino, madaftari na kalamu, Katiba ya Kenya ya 2010, Kijitabu cha Rajua ya 2030 na sera nyingine zifaazo, Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa 2008, Sheria ya Ukweli, Haki na Mapatano ya 2008 na Sheria nyingine za Bunge, Makubaliano ya Kimataifa, Mikataba na Maafikiano yanayohusiana na uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

#### Shughuli

- Mwelekezi awaongoza washiriki kutambua sera vinavyowezesha upatikanaji wa Uwiano wa Kitaifa.
- Washiriki wajaribu kuelezea vipengele hivi vikuu vya kikatiba.
- Mwelekezi hutumia hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki.



#### Maelezo Muhimu

#### Vipengele Vikuu vya Kikatiba Vitakavyowezesha Upatikanaji wa Uwiano wa Kitaifa

Kuidhinishwa kwa Katiba tarehe 27 Agosti, 2010 kulileta mwamko mpya wa Kiuchumi-jamii na kisiasa nchini Kenya. Waraka na ari ya Katiba kunalenga kukuza na kulinda maslahi ya mtu, familia, jamii na taifa zima kwa jumla. Inalenga kuangazia maswala yaliyowagawanya wakenya siku za awali kwa lengo la kuweka taratibu zitakazohakikisha kuwepo kwa jamii yenye uwiano na utangamano sambamba na Rajua ya Kenya ya 2030. Huku Katiba ikiwa imejikita kwenye misingi ya uwiano wa kitaifa, hivyo kuweka vipengele maalum ambavyo vinalenga kuangazia maswala ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Dibaji ya** katiba inaafiki kuwa Wakenya wanajivunia '*uanuai wa wakimaadili, kitamaduni, na kidini na kwa vyovoyote vile wameamua kuishi kwa amani na umoja kama taifa moja huru lisiloweza kugawanyika*' [Imetiliwa mkazo].

## Ibara ya 27

Ibara hii kuhusu usawa na uhuru wa kutokubaguliwa inasema kuwa:

- Kila mtu ni sawa mbele ya sheria na ana haki sawa ya kulindwa na manufaa sawa za kisheria;
- Usawa unajumuisha kufurahia kwa ukamilifu haki zote pamoja na uhuru wa kimsingi; na
- Taifa halitabagua moja kwa moja au vinginevyo dhidi ya mtu ye yote kwa msingi wowote wa rangi, jinsia, uja uzito, mtu aliyeoa ama kutooa, hali ya afya, kabilia, asili, rangi, umri, ulemavu, dini, falsafa, imani, utamaduni, mavazi, lugha ama kuzaliwa.

**Vifungu vingine muhimu kwenye katiba ni pamoja na ; Ibara za 7, 19, 20, 22, 33, 40, 43, 48, 52 – 57. Ibara hizi zinatilia mkazo vipengele vifuatavyo vya uwiano na utangamano wa kitaifa:**

- Uhuru wa watu;
- Lugha rasmi ya kitaifa na lugha nyinginez;
- Alama za kitaifa na siku kuu za kitaifa;
- Maadili ya kitaifa na kanuni za uongozi;
- Utamaduni;
- Haki za kimsingi hususan Ibara ya 53 (watoto), 54 (walemvu), 55 (vijana), 56 (jamii za watu wachache na zilizotelekezwa) na Ibara ya 57 (wazee katika jamii);
- Ardhi na mazingira;
- Uongozi na uadilifu;
- Uwakilishaji wa watu;
- Kuendeleza kwa uwakilishaji wa jamii zilizotelekezwa katika Bunge (Ibara ya 100) na haki ya kumuondoa mbunge (Ibara ya 104);
- Ugatuvi wa Serikali; na
- Usawa wa kugawana mapato ya kitaifa (Ibara ya 202) na Hazina sawia (Ibara ya 204).

## MADA 4: VYOMBO VYA KISHERIA VINAVYOWEZESHA KUPATIKANA KWA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

### Muda: Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati, kalamu za wino, madaftari na kalamu, Katiba ya Kenya ya 2010, kijitabu cha Rajua ya 2030 na sera muhimu, sheria ya uwiano na utangamano wa kitaifa, 2008, Sheria ya Ukweli, Haki na Mapatano ya 2008 na Sheria nyingine za Bunge, makubaliano ya kimataifa, mikataba na maafikiano yanayohusu Uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki kutaja **vyombo vya kisheria vinavyowezesha kupatikana kwa uwiano na utangamano wa kitaifa**
- Washiriki wanajaribu kutoa maana ya maneno.
- Mwelekezi hutumia hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki.



### Maelezo Muhimu

**Vyombo vya Kisheria vinavyowezesha kupatikana kwa Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.**

Vyombo hivi vya kisheria ni pamoja na vya kimataifa, maeneo na kitaifa.

#### 1. MUUNDO WA KISHERIA WA KIMATAIFA

##### a. Makubaliano ya kimataifa ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za Kibinadamu na za Kisasia.

### Ibara ya 2

- Kila taifa mwanachama wa makubaliano yaliyopo lina wajibu wa kuheshimu na kuhakikisha kuwa kila mtu aliye katika eneo lake na ambaye yuko chini ya mamlaka yake anafurahia haki zinazotambuliwa katika makubaliano yaliyoko bila ya ubaguzi wa aina yoyote, uwe wa rangi, jinsia, lugha, dini, siasa ama maoni mengine, chimbuko la uraia au kijamii, uzao au hadhi nyingine.

- ii. Kila taifa mwanachama katika maagano hayo kuzingatia sheria hiyo ama mikakati mingine ambayo itachangia kuimarisha haki hizo zinazotambuliwa katika makubaliano hayo kulingana na mchakato wa kikatiba.
- iii. Kila taifa mwanachama kwenye makubaliano hayo linahitajika:
  - a. Kuhakikisha kuwa mtu yejote ambaye haki ama uhuru wake unatambuliwa kwenye makubaliano hayo na unakiukwa atasaidiwa bila kujali kuwa anayekiuka ni afisa mwenye cheo kikubwa;
  - b. Kuhakikisha kuwa mtu yejote anayedai kuwa haki zake zimekiukwa kesi yake itaamuliwa na mahakama iliyohitimu, ama mamlaka ya utawala au ya sheria ama mamlaka yoyote itakayotolewa na mfumo wa sheria wa taifa, na kutafuta uwezekano wa kutatua kesi hiyo; na
  - c. Kuhakikisha kuwa mamlaka yaliyohitimu yatawezesha usaidizi huo iwapo itaruhusiwa.

### **Ibara ya 27**

Katika mataifa ambayo makabila, dini au lugha ni chache, watu wote kwenye makundi hayo hawatanyimwa haki ya kufurahia utamaduni wao, kukiri au kufuata dini yao au kutumia lugha zao. Ibara hii hasa inahusu "watu waliomo kwenye ... wachache", sio kwa vikundi au jamii zenyewe ijapokuwa kwa jumla umuhimu wa haki hii iko kwenye kauli ya "katika jamii na watu wengine wa jamii hiyo" ambayo imejumuishwa kwenye Ibara.

#### **b. Makubaliano ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za Kiuchumi, Jamii na Utamaduni**

Ibara ya 3 ya makubaliano hayo inasema kuwa taifa mwanachama litahakikisha kuwa haki ya usawa kwa waume na wake katika kufurahia haki kiuchumi, kijamii na kiutamaduni zimo kwenye makubaliano.

#### **c. Azimio Maalum la Ulimwenguni la Haki za Kibinadamu**

Ibara ya 2 ya azimio maalum inaeleza kuwa kila mmoja ana haki na uhuru ambao umo kwenye Makubaliano hayo, bila ubaguzi wa aina yoyote, uwe wa rangi, jinsia, lugha, dini, siasa ama maoni, chimbuko ama asili ya taifa, mali ama hadhi yoyote. Zaidi ya hayo, hakuna tofauti yoyote inayofaa kuzingatiwa kwa misingi ya siasa, mahakama ama hadhi ya kimataifa ama eneo ambalo mtu anatoka, iwapo inajisimamia, ni ya kiamana, haijitarwali yenyewe, ama kizuizi chochote cha kiutawala.

#### **d. Makubaliano ya Kimataifa ya Kuondoa hali zote za Ubaguzi wa Rangi (1965)**

Makubaliano haya yalikubaliwa na Umoja wa Mataifa ili kuharakisha kuondoa hali zote za ubaguzi wa rangi na kujidhifirisha kwake, na kuzuia na kukabiliana na mafundisho na matendo ya kiubaguzi ili kuendeleza maelewano kati ya watu wa rangi tofauti na kujenga jamii ya kimataifa iliyokombolewa dhidi ya aina za ubaguzi au kutengwa kwa rangi.

Mkataba wa Kimataifa wa kuondoa aina zote za Ubaguzi wa Rangi (ICERD) sio tu yale yaliyochukuliwa kuwa "ubaguzi wa rangi", yaani, mifumo rasmi ya sheria ambayo inabagua kwa misingi ya rangi. Kwa kweli, utekelezaji wa ICERD ni mpana kwani, "ubaguzi wa rangi" unaelezwa kuwa "kutengwa kwa aina yoyote, kuzuiwa ama kuchaguliwa kwa misingi ya rangi, ukoo asili ya utaifa au kabilia yenyewe kusudi au athari ya kuubatilisha au kudhoofisha kutambuliwa, kufurahia au kutumia kwa usawa haki za binadamu na uhuru wa msingi katika siasa, uchumi, jamii, utamaduni au katika nyanja nyingine za maisha ya umma."

#### **e. Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto**

Huu ndio na mataifa 191 wanachama, huu ndio mkataba wa haki za kibinadamu uliyoidhinishwa na mataifa mengi zaidi duniani. Makubaliano hayo yanalenga kuchangia na kulinda haki za mtoto. Watoto wanaelezwa kuwa watu walioko chini ya umri wa miaka 18 sawa na jinsi ilivyo nchini Kenya. Makubaliano hayo yanatoa hakikisho kwa haki za watoto kwa "kila mtu" chini ya vyombo vingine vya kimatifa.

**Ibara ya 2** inaeleza kuwa haki katika makubaliano lazima zihakikishiwe bila ya ubaguzi miongoni mwa sifa nyingine kama vile, rangi, lugha, dini, chimbuko la kitaifa ama kabilia. Kamati ya Haki za Mtoto ni chombo ambacho kina wataalamu wenye uhuru wanaochunguza utekelezaji wa mkataba kuhusu haki za mtoto na mataifa wanachama.

#### **f. Makubaliano ya kuondoa Hali Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake**

Kamati ya kuondoa Ubaguzi Dhidi ya Wanawake inasimamia Makubaliano haya, ambayo yanahu haki za wanawake. Haki hizi zinajumuisha haki ya kutendewa usawa kwa mujibu wa sheria; usawa wa elimu, kushiriki kisiasa, ajira, afya, na uchumi; uhuru wa kutodhulumiwa kimapenzi; na uwezekano wa mikakati ya muda mfupi ya kukabiliana na kutokuwepo kwa usawa. Pamoja na hayo kukubali kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake na "mtu yeyote, ama shirika au shughuli", Mataifa wanachama yamekubali kuchukua hatua madhubuti, "kubadilisha au kufutilia mbali sheria zilizopo, utaratibu, mila na vitendo" ambavyo vinawabagua wanawake.

Kamati ya Kuondoa Ubaguzi Dhidi ya Wanawake kwa kawaida imeeleza hali ya wanawake wakati wa mizozo na dhuluma za kijinsia. Mwaka wa 1992, Kamati hiyo

ilianza kuzingatia maoni ya jumla (No.19) kuhusu dhuluma dhidi ya wanawake, kuangazia pakubwa kimataifa kuwa wanawake wanazidi kubaguliwa kwa sababu ya jinsia yao.

#### **g. Makubaliano ya 1951 kuhusu Kuzuia na Adhabu ya Uhalifu wa mauaji ya Halaiki**

Makubaliano hayo yanafafanua mauaji ya halaiki kuwa '...yoyote kati ya matendo haya yaliyotekelawa kwa lengo/nia ya kuharibu, yote ama sehemu, taifa, jamii, rangi, kundi la dini kama vile:

- a. Kuua wanachama wa kikundi;
- b. Kusababisha maumivu makali ya kimwili au kiakili kwa wanachama wa kikundi;
- c. Kusababisha kimakusudi hali za kimaisha za kundi za kimaisha ambazo zinaweza kuwadhuru kimwili kwa ujumla ama sehemu;
- d. Kutumia njia zinazonua kuzuia uzao miiongoni mwa kundi; na
- e. Kuhamisha kwa lazima watoto wa kundi moja hadi lingine.

Makubaliano hayo yanaharamisha mauaji ya halaiki na yanahimiza mataifa yote yanayoshiriki kuzuia na kuadhibu vitendo vya mauaji ya halaiki katika vita na wakati wa amani.

#### **h. Azimio Maalum la 2007 kuhusu Haki za Wenyeji**

Azimio hilo linaweka wazi haki za mtu binafsi na wenyeji hali kadhalika haki zao za utamaduni, utambulisho, lugha, ajira, afya, elimu na maswala mengine. Aidha linasisitiza haki za wenyeji kudumishwa na kuboresha taasisi zao, utamaduni na itikadi, na kufanya maendeleo ya kutimiza mahitaji na matamanio yao. Linazuia ubaguzi dhidi ya wenyeji na kuendeleza kushiriki kwao kikamilifu katika maswala yote ambayo yanawahu na haki ya kubaki tofauti na kufanikisha maono yao ya kiuchumi na maendeleo ya kijamii.

### **2. VYOMBO VYA KISHERIA NA KISERA VYA KIMAENEO VINAVYOleta UWIANO WA KITAIFA**

#### **Muundo wa Makubaliano ya Kisheria**

Katika juhudzi zao za kujenga amani, maendeleo ya uchumi na kijamii, mataifa ya Afrika chini ya Umoja wa Afrika (AU,) yamepiga hatua kadhaa katika nyanja mbali mbali. Baadhi yao ni:

- a. Mpango wa Matendo wa Lagos (LPA) na Sheria Kamilifu ya Lagos (1980); ambayo ilijumuisha mipango na mikakati ya maendeleo ya kujitegemea na kushirikiana kati ya mataifa ya Afrika;

- b. Mkataba wa Afrika kuhusu Binadamu na Haki za Watu (Nairobi 1981), na Azimio maalum la Grand Bay na Mpango wa Matendo kuhusu Haki za Binadamu. Vyombo hivi viwili vilikubaliwa na OAU kuendeleza Ubinadamu na Haki za watu katika bara;
- c. Mpango Maalum wa uokoaji wa Uchumi wa Afrika (APPER) (1985): Huu ulikuwa mpango wa dharura ulioundwa kushughulikia majanga yaliyotatiza maendeleo katika miaka ya 1980, kufuatia ukame uliochukua muda na njaa ambayo ilikuwa imekumba bara na athari za madeni ya nje;
- d. Mkataba kuhusu Kushiriki kwa wengi ulikubaliwa mwaka wa 1990: Huu ulikuwa ushuhuda wa ari mpya ya OAU kuweka wakazi wa Afrika katikati ya maendeleo na uamuzi;
- e. Maafikiano ya 1991 yalianzisha Jumuiya ya Uchumi ya Afrika (AEC) uliojulikana kama Maafikiano ya Abuja. Yanayolenga kubuni/kuunda (AEC/JUA) kuititia awamu/ngazi sita zitakazochangia kuwepo kwa Soko la Pamoja la Afrika kuititia jumuiya za kikanda ama maeneo (RECs) kama viambajengo. Maafikiano hayo yamekuwepo tangu mwaka wa 1994;
- f. Mbinu ya mwaka wa 1993 ya Kuzuia Kusimamia, na Kusuluuhisha Mizozo ni dhihirisho ya bidii ya viongozi wa Afrika kutafuta suluhisho kwa mafarakano, kuendeleza amani, usalama na uthabiti/utulivu Afrika;
- g. Ajenda ya Makubaliano ya Cairo (1995) ni mpango wa kuzindua tena maendeleo ya Afrika ya kisiasa, kiuchumi na kijamii;
- h. Uamuzi wa Algiers kuhusu Mabadiliko yasiyo ya Kikatiba ya Serikali (1999) na Azimio maalum la Lomé kuhusu Muundo wa utendakazi wa OAU (2000);
- i. Azimio Maalum la 2000 kwenye Kongamano kuhusu Usalama, Uthabiti, Maendeleo na Ushirikiano unaunda kanuni za kimsingi za kuendeleza Demokrasia na uongozi mwema barani;
- j. Ushirikiano Mpya wa Maendeleo Barani Afrika (NEPAD) ulikubaliwa kama mpango wa AU katika kikao kilichofanyika jijini Lusaka (2001).

### **3. VYOMBO VYA KISHERIA NA KISERA VYA KITAIFA VINAVYOENDELEZA UWIANO WA KITAIFA.**

#### **a. Utaratibu wa Kitaifa wa Majadiliano na Maridhiano ya Kenya**

Utaratibu wa Kitaifa wa Majadiliano na Maridhiano ya Kenya (KNDR) ulikuwa mfano mzuri wa njia ya kukabiliana na majanga kwa haraka. Uliwakilisha "ukomo" na kurejesha utulivu na fursa ya kuangazia matatizo ya kimsingi nchini Kenya. Nafasi hiyo ilikuwa inatoweka na ilihitajika kurejeshwa ili kutekeleza ufanisi huo.

**Makubaliano na Maamuzi**

01 Februari 2008 – Taarifa iliyokubaliwa kuhusu mbinu za haraka na zilizohitajika kuangazia majanga yanayowahusu wanadamu;

04 Februari 2008 – Taarifa iliyokubaliwa kuhusu mbinu za usalama kurejesha urazini na kuruhusu uponyaji wa kitaifa;

14 Februari 2008 – Taarifa iliyokubaliwa kuhusu jinsi ya kusuluuhisha migogoro ya kisiasa;

28 Februari 2008 – Makubaliano kuhusu kanuni za ushirikiano katika serikali ya muungano/mseto;

28 Februari 2008 – Makubaliano kuhusu ugavi wa mamlaka yaliungwa mkono na Sheria ya Makubaliano ya amani ya Kitaifa na Maridhiano ya 2008;

04 Machi 2008 – Makubaliano kuhusu Kamati huru ya Marekebisho;

04 Machi 2008 – Makubaliano ya kuanzisha Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano kuangalia mchakato wa maridhiano;

04 Machi 2008 – Makubaliano ya kuanzisha Tume ya Ghasia za baada ya Uchaguzi (CIPEV iliyofahamika kama Tume ya Waki);

04 Machi 2008 – Makubaliano ya kuangazia maswala ya muda mrefu na kuyatafutia suluhisho kwa kukamilisha mchakato wa kuhakiki Katiba;

04 Machi 2008 – Makubaliano kuhusu Kamati Huru ya Kuhakiki Katiba;

04 Machi 2008 – Makubaliano ya kuanzisha Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano kusimamia mchakato wa maridhiano; na

30 Julai 2008 – Taarifa ya Vinara wakuu kuhusu maswala ya muda mrefu na suluhisho.

**b. Sheria ya Makubaliano na Maridhiano ya Kitaifa**

Hii ni Sheria ya Bunge ambayo iliyapa nguvu Makubaliano kuhusu Kanuni za Ushirikiano wa Serikali ya Muungano. Makubaliano haya yalilenga kuimarisha makubaliano na maridhiano ya kitaifa ili kuwezesha serikali ya muungano kuanzisha afisi za Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri kwenye Serikali ya Kenya. Makubaliano hayo yalichangia dhima ama wajibu mbali mbali.

### c. Rajua ya 2030 ya Kenya

Rajua ya 2030 ni mpango wa maendelelo ya Kenya kuanzia kipindi cha mwaka wa 2008 hadi 2030. Inalenga kuanzisha mfumo mpya nchini Kenya unaotegemea viwanda. "Taifa la watu wenyewe mapato ya kadri na kutoa maisha bora kwa kila raia ifikapo mwaka wa 2030". Rajua ya mwaka 2030 inaangazia nguzo tatu, ambazo ni uchumi, jamii na siasa. Nguzo ya uchumi inalenga kuhakikisha mafanikio kwa wakenya wote ifikiapo 2030 na kukua kwa asilimia 10 ya uchumi kwa mwaka. Nguzo ya jamii inalenga kujenga "Jamii yenye uwiano na usawa katika mazingira salama na safi." Nguzo ya siasa inalenga kutimiza mfumo wa kisiasa wa kidemokrasia uliojengwa kwa siasa za hoja na kanuni ya sheria na kulinda haki na uhuru wa kila mtu katika jamii.

Kukabiliana na ukosefu wa usawa na upendeleo unaosababishwa na ubaguzi kwa misingi ya rangi, ukabila na jinsia ni muhimu kwa kuhakikisha kuwa Kenya inakuwa taifa la watu wenyewe mapato ya kadri kama ilivyo kwenye Rajua ya 2030. Ubaguzi ni kikwazo kikubwa kwa kufikia malengo ya Rajua ya 2030.

Mpango wa kadri wa Awamu ya Kwanza (2008-2012) umechukua nafasi ya Mikakati ya uokoaji wa Uchumi kwa Utajiri na kubuni nafasi za Ajira (2003-2007) kama Mpango wa Awamu wa kadri. Nakala hiyo ilichapishwa baada ya kushiriki kwa wadau wengi wakiwemo serikali, sekte ya kibinagsi, mashirika ya jamii na washirika wa maendeleo. Kwa mujibu wa jukumu lake la kuunda sera za uchumi na mpango wa maendeleo wa taifa kwa jumla, afisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Taifa na Rajua ya 2030 zilichukua nafasi ya uongozi kwenye utaratibu wa kuchapisha Mpango wa kadri wa kitaifa. Katika mwaka wake wa kwanza, mpango wa MTP 2008-2012 ulilenga kujumuisha mwingilio uliopendekezwa kwenye ripoti ya Kamati Tekelezi ya Kitaifa ya Makubaliano na Mikakati ya uokoaji wa Uchumi na katika mwaka mmoja Mpango wa Uokoaji wa Uchumi kuangazia masuala ibuka yaliyotokea 2007 baada ya uchaguzi.

### Vifungu vya Uongozi, Kuleta Amani na Udhibiti wa Mizozo

Mikakati huu unalenga kuimarisha imani mionganoni mwa wakenya, haswa ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa usalama na ulinzi wa wakenya umehakikishwa wakati wote; kuwa wakenya wa matabaka mbali mbali wanaweza kupata haki na kuwa migogoro inatatuliwa kwa njia nzuri kwa kuzingati sheria. Tume Huru ya Ukweli, Haki na Maridhiano (TJRC) ilianza kufanya kazi mwaka wa 2008. Kuendeleza uwiano wa kitaifa, tume huru ya kudumu ya Uwiano na Utangamano ilianza kazi mwaka wa 2008. Aidha, sera ya kitaifa na muundo wa sheria zilikuwa na zinandelea kuenda sambamba na uchumi pamoja na haki za msingi na usawa wa kijinsia.

Mkakati ulipendekeza kuwa sheria na masharti yinazofungamanisha vyama vyakisiasa na muundo wa mchakato urekebishwe kulingana na malengo ya Rajua ya Kenya ya 2030 ya kuendeleza ushindani wa haki na maswala yanayohusu siasa.

#### **d. Sheria ya Uwiano na Utangamano wa kitaifa ya mwaka wa 2008**

Hii ni Sheria ya Bunge ambayo inalenga kuhimiza uwiano na utangamano wa kitaifa kwa kuharamisha ubaguzi kwa misingi ya ukabila, dini, rangi na chimbuko ama asili ya mtu. Sheria ilitoa uanzilishi, uwezo na majukumu ya Tume ya Uwiano na utangamano wa kitaifa. Inaelezea wazi kuwa lengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa Tume hiyo lilikuwa kuendeleza usawa wa nafasi, mahusiano mema, umoja na amani mionganoni mwa watu wa makabila mbali mbali na wa rangi tofauti katika nchi ya Kenya na kuishauri serikali katika masuala yoyote kama hayo.

**Ibara ya 25** inaelezea lengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa Tume hiyo ilikuwa ni kuendeleza usawa wa nafasi, mahusiano mema, umoja na amani mionganoni mwa watu wa makabila mbali mbali na wa rangi tofauti katika nchi ya Kenya na kuishauri serikali katika masuala yoyote kama hayo.

#### **e. Sheria ya Ukweli, Haki na Maridhiano ya mwaka wa 2008**

Hii ni Sheria ya Bunge ambayo inaeleza majukumu na mamlaka ya Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano. Tume hiyo inalenga kufanikisha malengo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kupitia kuanzisha rekodi kamilifu za visa vyta ukiukaji wa haki za binadamu kuanzia Desemba 12 mwaka wa 1963 hadi Februari 28 mwaka wa 2008.


Malengo muhimu ya Tume ni pamoja na kuendeleza amani, haki, umoja wa taifa, upatanishi na maridhiano mionganoni mwa watu wa Kenya kupitia kuanzisha ripoti kamilifu ya ukiukaji ikiwemo, asili na kiwango cha ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa haki za uchumi na pia kutoa nafasi kwa wahusika kukiri na waathiriwa kuwasikia.

#### **f. Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba**

Hii ni Wizara ambayo ilianzishwa kutoa ushirikiano na kuendeleza haki na uhuru wa kimsingi kupitia kubuniwa kwa utaratibu wa Kikatiba, kuendeleza demokrasia, kukuza na kuendeleza mfumo sawa wa haki kwa kila mtu. Kuendeleza utamaduni usiokuwa na ujisadi. Maono yake ni Haki, hayana ujisadi na Ustawi wa Kenya'. Idara ya Uwiano wa Kitaifa ilibuniwa mwaka wa 2009 mahsus kuwajibikia kuendeleza uwiano na utangamano mionganoni mwa wakenya. Hili linafikiwa kupitia mipango mbali mbali na shughuli nyingine mionganoni mwa wadau.

Jukumu lingine la Wizara ni pamoja na kubuni sera ya sheria kuhusu usimamizi wa haki, maswala ya kikatiba, elimu ya sheria, mikakati dhidi ya ujisadi, uadilifu na

maadili, marekebisho ya sheria, vyama vya siasa, msaada wa sheria, huduma za ushauri na uchaguzi. Wizara ina wajibu wa kusimamia vyombo ama asasi huru: Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya (KNCHR), Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC), Chuo cha Sheria cha Kenya (KSL), Tume ya Marekebisho ya Sheria ya Kenya (KLRC), Tume ya Haki Ukweli na Maridhiano (TJRC), Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC) na Tume ya Usimamizi wa Haki (CAJ).



*Jedwali 4: Vyombo vya kisheria vinavyoendezea uwiano na utangamano wa kitaifa*

## MADA 5: ASASI MUHIMU ZINAZOWAJIBIKIA UENDELEZAJI WA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 40.

**Vitendea-kazi :** Chati za kugeuzwa, kalamu za wino, madaftari na kalamu, Katiba ya Kenya ya 2010, kijitabu cha Ruwaza ya mwaka wa 2030 na sera nyingine, Sheria ya Uwiano na utangamano wa kitaifa ya mwaka wa 2008, Sheria ya Haki na Maridhiano ya mwaka wa 2008, na Sheria nyingine za Bunge, Mikataba ya kimataifa, mikataba na makubaliano yanayohusu uwiano wa kitaifa na utangamano.

**Mbinu:** Chemsha Bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi awaongoza washiriki kutaja vyombo vyaheria ambavyo vinachangia uwiano na utangamano.
- Washiriki wajaribu kutaja vyombo hivyo.
- Mwelekezi atumie hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki.



### Maelezo muhimu

#### Asasi Muhimu Zinazowajibikia Uendelezaji wa Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.

Hizi ni pamoja na zifuatazo lakini kuna nyingine ambazo hazijatajwa:

1. Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya Kikatiba;
2. Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC);
3. Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KNCHR);
4. Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi;
5. Tume ya Marekebisho ya Sheria ya Kenya;
6. Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano;
7. Wizara ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Ndani; na
8. Wizara ya Elimu.

## **1. Sheria ya Ukweli, Haki na Maridhiano ya mwaka wa 2008**

TJRC ni sehemu ya ajenda ya nne (4) ya uwajibikaji ya makubaliano ya Amani ya kitaifa yaliyosainiwa mwaka wa 2008. Kwa kuelezea chanzo na athari za kukiukwa kwa haki za binadamu, TJRC inalenga kuchangia umoja wa kitaifa, maridhiano na upatanishaji. Katika utenda kazi wake, tume hiyo inaazimia kutimiza malengo sita muhimu: ukweli, haki, amani, umoja wa kitaifa, upatanishaji (taifa na mtu binafsi), na urejesho wa hadhi ya binadamu kwa waathiriwa na wakiukaji.

## **2. Wizara ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Ndani – Kamati inayoongoza Upatikanaji wa Amani na Udhibiti wa Mizozo (NSC)**

Kupitia wizara ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Ndani, serikali ya Kenya inahakikisha kuwa raia wake hawafurahii tu usalama katika mipaka yao bali pia wanaishi kwa amani wenye kwa wenye kwa kudumisha sheria na utangamano. Kupitia idara zake mbali mbali, wizara hiyo inaweza kutekeleza majukumu yake. Kwa kuzingatia uwiano wa kitaifa, kamati inayoshughulikia upatikanaji wa amani na udhibiti wa mizozo, ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa jamii zinaishi kwa amani hivyo kuchangia uwiano wa kitaifa.

Kamati hiyo ilibuniwa mnamo mwaka wa 2001, na huleta pamoja wadau kwa lengo la kuwashirikisha na kuleta juhudi zao ili kuwa na amani na kutatua mizozo nchini Kenya na pia kwenye mipaka yake. Ikiwa na malengo ya kuendeleza amani kupitia mifumo madhubuti kati ya serikali, wadau wengine na jamii katika viwango vya kitaifa na kimaeneo, NSC inalenga kuleta juhudi za wadau mbali mbali pamoja na kushirikiana nao kwani amani haiwezi ikapatikana bila juhudi hizo.

## **3. Wizara ya Elimu**

Wizara ya Elimu ina mchango mkubwa katika kuendeleza Uwiano na Utangamano wa kitaifa. Malengo ya Elimu nchini Kenya yamechangia:


- a. Kuimarisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa taifa;
- b. Kuendeleza maendeleo na utoshelevu wa mtu binafsi;
- c. Kuendeleza maadili mema ya kijamii na kidini;
- d. Kuendeleza usawa wa jamii na uwajibikaji;
- e. Kuimarisha heshima na maendeleo, kati ya tamaduni mbali mbali za Kenya;
- f. Kuboresha utaifa na heshima hata katika mataifa mengine;
- g. Kuboresha dhana njema ya kulinda mazingira na pia kuwa na afya njema;

na

h. Kuboresha maendeleo ya kitaifa kupitia jamii, uchumi, teknolojia na viwanda.

#### **4. Wizara ya Michezo na Maswala ya Vijana**

Wizara ya Michezo na Maswala ya Vijana ilianzishwa Desemba mwaka wa 2005 kuwakilisha na kuangazia maswala ya vijana nchini Kenya. Wajibu muhimu wa Wizara ya Michezo na Maswala ya Vijana ni pamoja na kuwapa uwezo; kushirikisha; kufunza na kutatua maswala yanayowakumba vijana.



*Jedwali 5: Taasisi muhimu zilizowezeshwa kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa*

#### **MUUNDO WA KIMATAIFA WA KIASASI**

Chini ya muongozo wa Baraza la Uchumi na Jamii (ECOSOC), Mipango maalum na washirika kama vile Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira (UNEP), Tume ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu, (UNHCR), Taasisi ya Utafiti ya Umoja wa Mataifa ya kutwaa silaha

(UNIDIR), na wengine wengi wanaojaribu kuzuia mizozo kutosambaa kwa kuangazia chanzo chake wala sio tu kushughulikia dalili zake.

Kuzuia mizozo na kuendeleza amani kumekuwa muhimu tangu vita vikuu vyta pili, silaha zimekuwa hatari zaidi. Mbali na hayo, ijapokuwa kuna utajiri mkubwa ulimwenguni, ugavi wake sio sawa. Pengo hili kati ya tajiri na maskini linaonekana kila mahali na katika kila taifa, na linaongezeka, haswa kati ya mataifa ya Kaskazini na Kusini.

Ama kwa kweli, mizozo hukuwa kwa haraka katika mazingira ya umaskini. UNDP imewezeshwa kuchangia kupunguza umaskini, kuwaleta wanawake pamoja, kuhifadhi mazingira na kuboresha taasisi za kidemokrasia. Usimamizi wa uchaguzi unadhihirisha hili bayana. UNDP haiko peke yake katika kutekeleza majukumu hayo, kwani kuna maelfu ya mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) yanayojaribu kutekeleza kwa njia moja ama nyingine.

### **Marejleo**

Government of Kenya, (2008) National Cohesion and Integration Act,  
No. 12 of 2008. Nairobi: Government Printer

Government of Kenya, (2008) Truth Justice and Reconciliation Act No. 6  
of 2008. Nairobi: Government Printer

Government of Kenya, (2010) Constitution of Kenya, 2010 Nairobi:  
Government Printer

## SOMO LA 5: MIFUMO YA TAHADHARI NA MIITIKO YA MAPEMA - MBINU ZA UPATIKANAJI WA UWIANO

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wataweza kutambua majukumu ya kukabiliana na mifumo ya tahadhari za mapema na miitikio ili kufikia uwiano wa kitaifa.

### Utangulizi

Umuhimu wa tahadhari na miitiko ya mapema katika upatikanaji wa uwiano wa kijamii hauwezi kupuuzwa. Katika kutambua umuhimu wa somo hili, mbinu za kuzuia migogoro isiyojitekeza zafaa kupewa kipaumbele.

### MADA 1: DHANA YA TAHADHARI NA MIITIKO YA MAPEMA

**Muda:** Dakika 20.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, kalamu, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi awaongoza washiriki kueleza dhana ya ‘**tahadhari ya mapema**.’
- Washiriki wajaribu kuelezea maana ya neno.
- Mwelekezi atumie hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki.

Chemsha  
Brainstorm  
bonqo

### Maelezo Muhimu

#### Tahadhari ya mapema

Tahadhari za mapema katika utaratibu wa uwiano na utangamano ina maanisha dalili za mzozo. Hivyo tahadhari za mapema, hututahdarisha kuwa huenda kuna mzozo ambao unakaribia kuibuka. Na kwamba pana haja ya maandalizi mema ili kuhakikisha kuwa mizozo inachukua mkondo usio wa vurugu. Wakati mizozo ambayo haijajitokeza ingalipo, huenda ni wakati mwafaka wa kuzuia na kuingilia kuchipuka

kwake. Maswala ya tahadhari za mapema yanalenga kubashiri matokeo ya mizozo ama kung'amua kuenea kwa ghasia ili kuokoa maisha na mali. Kukabiliana kwa haraka na ghasia hizo ndio ufanisi wa kuzuia kwa tatizo hilo. Mikakati kabambe ya uzuiaji ina kanuni tatu: jinsi utakavyofanya kufuatia dalili za ghasia; njia kamilifu na yenye uwiano ya kukabiliana na shinikizo hizo, ama hatari zinazochangiwa na mizozo na juhudzi za pamoja za kukabiliana na vyanzo vya ghasia. Maelezo ya ishara za awali kimsingi zimetolewa kwa ukiukwaji wa haki za binadamu/dhuluma. Ugazi wa haki za binadamu ni wa muda mrefu na tathmini ya hali ya haki za binadamu katika nchi ama eneo. Inajumuisha ukusanyaji wa habari ama maelezo kwa njia mwafaka zinazohusiana na dhuluma za haki za binadamu. Ishara za dhuluma hizo huenda zikawa ni za kiuchumi ama kijamii.

### **Dalili za Kiuchumi:**

- Sifa za kiuchumi ambazo zinasababisha mzozo ni zippi? Madini, biashara, ardhi, maji, mipaka n.k.
- Rasilmali zinazodumisha mzozo huo zinatoka wapi?
- Je, athari za mzozo huo kiuchumi ni zippi?

### **Dalili za Kijamii:**

- Je, mzozo huo umekuwa na athari gani kwa huduma za kijamii kama vile elimu, afya na makazi?
- Je, watu wa umri tofauti, jinsia, makabila ama makundi ya kisiasa wanaathiriwa tofauti?

Habari kuhusu uwezekano wa kuzuka kwa mzozo inaweza kupatikana kutokana na vyanzo mbali mbali. Hivi ni pamoja na - ya kinyumbani, ya kitaifa ama mashirika ya kimataifa yasiyokuwa ya kiserikali, makundi ya kidini, wataalam, madaktari, mawakili, wafanyakazi wa jamii, wanahabari, miungano ya wafanyakazi, wabunge/madiwani, vyombo vya usalama, polisi, majeshi, mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN), mabalozi na serikali mionganoni mwa vingine.

Kimsingi, ni muhimu kubuni njia za kutambua uwezekano wa kutokea kwa mzozo kabla haujatokea. Kwa mfano, kwa kuzingatia juhudzi sawa na hizo za kubashiri majanga ya kiasili na mavuno, wengi wamejaribu kujenga mifumo ya kuonya ama ya tahadhari za mapema. Unaweza kutofautisha tahadhari za mapema, kwa mfano kuingia kwa wakimbizi na kuzuia mzozo. Tahadhari za mapema ni za kufurahisha kwani zinatoa fursa ya kuzuia kuenea ama kuibuka kwa mzozo. Maisha yanaweza kuokolewa na hata mzozo kuthibitiwa.

## MADA 2: MANUFAA YA TAHADHARI NA MIITIKO YA MAPEMA

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, kalamu, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi anaongoza washiriki kueleza **manufaa ya tahadhari** na miitiko ya mapema na jinsi ya kukabiliana nazo.
- Washiriki wajaribu kutaja manufaa.
- Mwelekezi atumie hoja muhimu kujumuisha maoni ya washiriki na kutathmini.



### Maelezo Muhimu

#### Manufaa ya tahadhari na miitiko ya mapema ya mizozo

- a. Lengo la mfumo wa tahadhari za mapema linaweza kueleweka kama kuepusha ama kupunguza mizozo, hali ya kuzuia majanga ya kibinadamu ambayo yanatishia maendeleo endelevu ya binadamu.
- b. Mfumo mwafaka wa tahadhari za mapema sio tu suluhisho la muda mfupi, lakini pia umeundwa kuchangia uteuzi wa mikakati ya maendeleo ya muda mrefu ambao unaweza kupunguza majanga ya siku za baadaye.
- c. Mfumo wa tahadhari za mapema ni zaidi ya kupata habari ama maelezo. Unatoa tathmini mwafaka ambayo inaweza kupunguza viwango vya mizozo ama ukosefu wa uthabiti.
- d. Mfumo wa tahadhari za mapema unaweza kutoa tathmini ambayo inaweza kutambua sifa zinazochangia ukosefu wa uthabiti na kutoa misingi ya kutathmini hali ya siku zijazo na kutoa mapendekezo kwa waundaji wa sera za kitaifa na kimataifa jinsi ya kukabiliana na hali hiyo.
- e. Mifumo kama hiyo inafaa pia kuweka mikakati ya kuzuia, ambayo imetumika katika miktadha mbali mbali iliyopita, kiasi cha ufanisi na gharama zake. Tathmini kama hiyo huboresha ubashiri wa kutokea kwa mzozo mapema. Mfumo wa sasa

wa tahadhari umepatikana kuwa sahihi kwa asilimia themanini (80%) ya wakati. Hii inaweza kutumika kujenga miungano ya kisiasa kati ya waliona uwezo wa kuitikia ili kuimarisha njia za kuzuia kwa kiasi cha kuzuia mizozo na kubuni mbinu za kudumisha amani. Kadhalika miungano hiyo lazima ijumuise ilie ya kitaifa, kimataifa, ya kibinagsi na umma na kwa hivyo kuimarisha taasisi za kidemokrasia na uwezo wao wa kudhibiti mizozo yao kwa muda mrefu.

**Wakati wa kutathmini tahadhari za mapema ni muhimu kuzigawanya kwa namna mbili:**

- a. Kwanza, kuna lengo la kukusanya data ili kuamua iwapo hali fulani ni hatari na kuamua ni yapi ya muhimu yatakayoweza kufuatiliwa.
- b. Pili, ni jukumu la kuwashawishi viongozi wa kisiasa kuchukua hatua kulingana na tahadhari za mapema hasa pale ambapo pana habari za uwezekano wa kutokea mzozo. Ni muhimu kuzingatia kuwa ijapokuwa wakosoaji ni wepesi kusema kuwa tahadhari za mapema mara nyingi hazina ufanisi, waungaji mkono wa mfumo huu kila mara hutumia mifano ambapo imeonyesha ufanisi. Wanaeleza kwamba thamani yake ni kubwa mno kuliko kuacha kushughulikia jambo hilo hata kama kuna ugumu wa aina yoyote.

Mtandao mzuri wa tahadhari za mapema ni ule wenye sifa zifuatazo:

- a. Uko karibu na mahala penye mzozo. Taratibu za tahadhari na miitiko ya mapema zinazotokana na tahadhari za mapema za raia ni mwafaka;
- b. Kuwa na mtandao imara wa wale wanaofuutilia;
- c. Kutumia vyanzo mbali mbali vya habari na kutumia mbinu mbali mbali za uchambuzi;
- d. Kutumia kikamilifu teknolojia inayofaa ya habari na mawasiliano;
- e. Kutoa ripoti za kila mara; na
- f. Ina uhusiano imara na utaratibu wa miitiko.

### MADA 3: UTAMBUZI WA ISHARA ZA TAHADHARI ZA MAPEMA

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-Kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo, kujadili.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi kuongoza wanaoshiriki kutambua **ishara za tahadhari za mapema**.
- Washiriki wanajaribu kutambua ishara za hatari.
- Mwelekezi kutumia vidokezo muhimu kwa kutoa mukhtasari wa maoni ya washiriki.



#### Vidokezo Muhimu

##### **Ishara za tahadhari za mapema zinazoweza kutokea**

- a. Mabadiliko ya ghafla ya idadi ya watu katika makazi na kufurushwa kwao;
- b. Ongezeko la viwango vya ukosefu wa ajira na mvurugiko wa kura za maamuzi au chaguzi;
- c. Mikingamo ya kiuchumi au majanga ya kifedha;
- d. Uharibifu au uchafuzi wa maeneo ya kidini;
- e. Ubaguzi au mapendeleo ya kundi moja dhidi ya jingine kisheria;
- f. Ongezeko la kutovumiliana ‘kijamii’ na mapendeleo;
- g. Ongezeko la maandamano au mikutano ya makundi na ukandamizaji wa serikali; na
- h. Ongezeko la wakimbizi na kuingilia kati kwa mataifa ya kigeni.

## MADA 4: HATUA ZA KUZUKA KWA MAFARAKANO/ MIGOGORO

**Muda:** Dakika 30

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki kuorodhesha **hatua za kuzuka kwa mafarakano ama migogoro.**
- Washiriki wajaribu kuorodhesha hatua hizo.
- Mwelekezi kutumia vidokezo muhimu kwa kutoa mukhtasari wa maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Hatua za Kujisuka kwa Mgogoro/Mzozo

##### 1. Miundo ya hofu au kudorora kwa usalama:

Hatari zinazoweza kutokea katika hatua hii zinaweza kutambuliwa kwa kufuatilia chanzo chake au hali zilizopangika ambazo huunda vyanzo vya hofu na hali ya hatari.

Mifano inahusisha historia ya ukandamizaji wa nchi, misimamo ya kutenga, na ukosefu wa hali ya demokrasia, ongezeko la mianya katika mapato na nafasi za kiuchumi, usababishaji wa ardhi kukauka na shirikizo kutokana na ongezeko la watu. Hali hizi zilizopangika hubadilika polepole, na hivyo kuunda msingi wa tathmini ya muda mrefu wa hali ya hatari. Katika hatua hii, kuna uwezekano mkubwa kwamba hatari itatokea baada ya miaka au miongo kadha. Kwa hivyo, kuna haja ya kujenga amani ili kuzuia hali ya hatari au harakati za kuleta amani kuititia kwa uimarishaji wa mipango ya muda mrefu.


## 2. Ueneaji

Hatari zinazoweza kutokea katika hatua hii muhimu zinaweza kubainishwa kupitia kwa ufuatiliaji wa hali pana au 'vichochezi' vinavyoweza kueneza hali zilizopo, na hatimaye kuzidisha hofu. Mifano inahusisha upatikanaji wa silaha na rasilmali, matukio ya mienendo ya kutisha au ghasia za kiwango cha chini, sera mpya za kubagua au kukandamiza, kutopatikana kwa mazao ya mimea, na thamani ya sarafu kudorora. Haya ndiyo matukio ambayo huonekana mapema na kutoa misingi ya ishara tahadhari za mapema. Viashiria hivi vinaonyesha uwezekano wa mzozo kutokea katika miezi au majuma yajayo. Kwa hivyo, uanadiplomasia wa mapema wa kuzuia migogoro na jitihada za kuudhibiti, au mipango ya kupata msaada wa kibinadamu na kuweka amani katika dakika za mwisho huwa muhimu sana.

## 3. Mgogoro/Vita

Mazingira yanayopelekea kufikia watu ili kupewa misaada ya kibinadamu ama hata vita kamili, huweza kudhihirika kwa matukio kama vile jaribio la mapinduzi, mauaji ya kisiasa, au tangazo la hali ya hatari kwa nchi – hatua inayoweza kuwa kichocheo kama vile cheche za moto zinazoweza kuchoma miti au magogo makavu yanayoweza kusababisha miale mikali (hali za kimpangilio) na nyasi kavu au mafuta (vichocheo vya mzozo). Katika hatua hii, nafasi ya kukingga huwa imepita, lakini haja ya kuwepo kwa taarifa muhimu na kuchukua hatua kunahitajika.

Mifumo ya tahadhari za mapema na miitiko huhitaji taratibu za kutathmini hatari ya kimpangilio inayoweza kuibua hatua zinazofaa za kuzuia ili kukabili matatizo ya kimpangilio, na tahadhari pana za mapema kwa lengo la kuwa na jitihada za kumaliza mizozo hiyo haraka iwezekanavyo.



*Mchoro wa 6: Hatua za Kuenea kwa Mafarakano ama Migogoro*

## MADA 5: MASWALA YA MAADILI KATIKA UTARATIBU WA TAHDHARI ZA MAPEMA

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi kuwaongoza washiriki **kuorodhesha masuala ya kimaadili** katika utaratibu wa tahadhari za mapema.
- Washiriki wanajaribu kuorodhesha masuala ya kimaadili. Mwelekezi atumia vidokezo muhimu katika Kunakili kwa ufupi maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Maswala ya kimaadili katika Tahadhari za Mapema

##### 1. Kutokuwa na mapendeleo

Watu wanaohusika katika tahadhari za mapema wanafaa kuepuka mapendeleo wakati wote ule. Hii inamaanisha kuwa wanafaa kujitolea kukabiliana na masuala yote katika njia sawa bila kujali kama yanawaathiri wao au rafiki na jamaa zao. Inaweza pia kumaanisha kuwa hawafai kufanya mapendeleo kwa wahusika wowote katika mazingira ya migogoro inayoweza kuvuruga kupatikana kwa amani.

##### 2. Faafu

Tahadhari za mapema, kama sehemu muhimu ya kuimarisha amani, inahitaji kwamba wahusika wawe ni wenye maadili ya hali ya juu katika jamii. Kwa hivyo, wahusika hao, wanafaa kuwa waaminifu na wenye ukweli nyakati zote.

##### 3. Kutegemewa

Tahadhari za mapema zinahitaji uhusishaji wa watu wanaoweza kutegemewa na watakapatikana kila mara kwa ajili ya kazi hii muhimu. Watu hawa wanafaa wawe wa kutegemewa katika ukusanyaji habari bila kujali changamoto wanazoweza kukumbana nazo na hivyo kuleta matokeo bora.

#### **4. Kuzingatia usiri**


Tahadhari za mapema ni utaratibu unahitaji umakini na unaohusisha ushughulikiaji wa habari muhimu sana. Ushughulikiaji mbaya wa taarifa hizo unaweza kusababisha hatari kubwa. Njia mojawapo ya kuepuka hali hii ni kutumia mbinu ya usiri mkubwa katika shughuli hii. Vyano vya habari hizo vinafaa kulindwa ili kusalia kuwa muhimu katika mfumo mzima wa utafutaji wa habari. Kadhalika, haifai kabisa kutoa siri kwa wahusika wa pande zisizokuwa kwenye mifumo ya kushughulikia habari za tahadhari za mapema za migogoro na uchukuaji wa hatua za mapema kwa mfumo huo.

#### **5. Kujitolea kwa dhati**

Mifumo ya tahadhari za mapema kote ulimwenguni hutegemea watu ambao katika kufahamu umuhimu wa mbinu kama hizo kwa jamii yao au taifa, hutoa huduma zao kwa malipo madogo au hata bila malipo kabisa kama sehemu ya mchango wao wa kuleta amani. Wakati ambapo katika mazingira mengine, tahadhari za mapema husababisha kuwepo kwa haja ya kuwafidia wanaohusika kwa ajili ya muda na rasilmali zao, ila tu sehemu ya kujitolea inafaa kuwa kichocheo muhimu kwani hutoa hakikisho la umiliki na ushiriki katika ngazi ya jamii.

#### **6. Kutii sheria**

Kushiriki katika tahadhari za mapema hakumzuii mtu kutii sheria. Kwanza kabisa, kama sehemu muhimu ya masuala ya maadili inayohitaji uzingativu mkubwa, wale wote wanaohusika lazima wahakikishe kuwa wanadumisha sheria. Hii pia inahusisha kuheshimu utawala wa serikali na majukumu yake yote. Kuhusika kwa utawala wa serikali katika hali hii kuna umuhimu mkubwa katika ufanisi wa mkakati huu.



*Jedwali 7: Maswala ya Kimaadili katika Tahadhari za Mapema*

## MADA 6: MBINU ZA KUPUNGUZA MIGOGORO KWA KUTUMIA MIFUMO YA TAHADHARI ZA MAPEMA NA MIITIKO

**Muda:** Dakika 50

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, kalamu, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki katika kuorodhesha **mbinu za kupunguza migogoro** kwa kutumia mifumo ya tahadhari za mapema na miitiko.
- Washiriki wanajaribu kuorodhesha mbinu hizo.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu katika kunakili kimukhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu


#### Mikakati

- (a) Kufunza wafanyakazi wa Mashirika ya Kijamii kuhusu tahadhari za mapema na miitiko. Hii itawapa maarifa yanayohitajika.
- (b) Kuunda mtando: Mitando inafaa kusambazwa kwa mataifa mbali mbali ili kufanya kazi kwa ushirikiano hasa katika miradi ya usalama ya ubadilishanaji kama vile kuingizwa kwa silaha au kutekwa nyara kwa watu mipakani.
- (c) Kuimarisha vyombo vya habari: Kwa hakika, taarifa nyingi za vyombo vya habari huonyesha mielekeo tofauti ya kijamii. Kuhusu tahadhari za mapema, mifumo iliyoundwa kulinda uhuru wa vyombo vya habari kama vile uchambuzi na tahadhari za mapema zinataifa kutiliwa mkazo. Vyombo vya habari ni muhimu katika ujenzi wa taifa hasa wakati ambapo shughuli zinaposimamiwa vyema. Panafaa kuwepo kwa mpango wa ufundishaji wa wanahabari ili kuwashamasisha kuhusu tahadhari za mapema na maswala ya miitiko.
- (d) Kuhusisha mamlaka ya kitamaduni: Ushirikiano wa viongozi wa kitamaduni katika utekelezaji wa mifumo ya tahadhari za mapema na miitiko ni muhimu. Hata kama pana haja ya kutilia mkazo utawala wa kiwango cha kitamaduni kwa lengo la tahadhari za mapema za migogoro, kadhalika pana haja kama hiyo ya kutoa

mafunzo kabambe kwa mamlaka ya kitamaduni kuhusiana na majukumu yao katika tahadhari na miitikio ya mapema.

Kwa ufupi, uzuiaji mgogoro unahitaji ufuutiliaji makini wa viashiria vya kuongezeka kwa hofu na hivyo kuchukua hatua za kupunguza hali hiyo. Tahadhari za mapema zinahusisha ukusanyaji wa data, tathmini ya maswala yenye hatari, na kusambaza habari pamoja na mapendekezo kwa makundi ya watu ambao ndio walengwa. Mifumo ya miitiko ya mapema inamaanisha jitihada za uzuiaji zinazofaa na zinazowekwa kwa wakati ufaao, aghalabu zinafanywa mapema kabla ya kutokea kwa migogoro. Mifumo ya tahadhari za mapema na miitiko imetumiwa na mashirika ya kimataifa, mashirika yanayohudumu baina ya mataifa, taasisi za utafiti na makundi yasiyokuwa ya Kiserikali. Hata hivyo, kuna tetesi kwamba tahadhari za mapema hazijasaidia pakubwa katika upatikanaji wa suluhu kamilifu la migogoro.

Ijapokuwa kuna changamoto katika kushughulikia hali hii, sehemu ngumu zaidi imekuwa kuwabembeleza viongozi wa kisiasa na umma kwa jumla kushughulikia tahadhari hizo zinapotolewa. Mara nyingi, mashirika ya kijamii hulazimika kutekeleza maradufu majukumu yao ya kutahadharisha na kushughulikia hatua za kukabili hatari. Baadhi ya wachanganuzi wanasisitiza haja ya kutambua kwamba tahadhari za mapema zinaingiliana na siasa – katika swala la “ni yupi anayemuonya yupi na hadi kwa kiwango gani?” na pia katika njia za kufahamu kwamba ni tahadhari gani zinazofuatwa. Pia pamekuwa na shinikizo kwamba lazima tahadhari hizi zizingatie viashiria vya usalama wa binadamu unaojumuisha kutunza haki za kijinsia na zile za wanyonge. Ukiukaji wa haki hizo unaweza kuwa kiashiria cha kuongezeka kwa hali ya hofu na migogoro. Kwa ufupi, mifumo ya tahadhari za mapema na hatua zinazochukuliwa huhitaji msaada zaidi ili kuhakikisha zinaffaa katika siku za usoni.



*Jedwali 8: Mikakati ya Kupunguza Migogoro*

**Marejleo**

- Baldwin C., Chapman C., and Gray Z., (2007) 'Minority Rights: The Key to Conflict Prevention. London: Minority Rights Group International
- Brown S., Doe S. G., Nyheim D., Rosenblum-Kumar G., and Shanahan Y., (2005) Early Warning and Early Response Handbook. Conflict Prevention and Post-Conflict Reconstruction Network
- Goldstone J. A., (2008) 'Using Quantitative and Qualitative Models to Forecast Instability', Washington DC.: United States Institute of Peace
- Lund M., (1995) 'Under-rating Preventive Diplomacy: A Reply to Stedman', Foreign Affairs, July/August
- Machira Apollos, (2011) Conflict Transformation. Nairobi: Aluka Press
- Matveeva A., (2006) Early Warning and Early Response: Conceptual and Empirical Dilemmas. Hague: European Centre for Conflict Prevention,
- Nyheim D., (2009) Preventing Violence, War and State Collapse: The Future of Conflict Early Warning and Response. Paris: Organization for Economic Cooperation and Development (OECD)
- Schmeidl S. and Piza-Lopez E., (2002) Gender and Conflict Early Warning: A Framework for Action. London: International Alert
- Srinivasan S., (2006) Minority Rights, Early Warning and Conflict Prevention: Lessons from Darfur. London: Minority Rights Group International
- Stedman S. J., (1995) 'Alchemy for a New World Order: Overselling Preventive Diplomacy?' Foreign Affairs, May/June
- Zartman W., (2001) 'Preventing Deadly Conflict', Security Dialogue, vol. 32, no. 2, pp. 137-154

## SOMO LA 6: MAWASILIANO KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Ifikapo mwisho wa somo hili, washiriki wanafaa kuwa na uwezo wa kuthamini namna mawasiliano bora yanavyoimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa.

### Utangulizi

Mada hii inafasiri mawasiliano shirkishi na kujaribu kueleza harakati ya mawasiliano. Inaangazia umuhimu wa mawasiliano mwafaka katika uimarishaji wa uwiano na utangamano wa kitaifa na kuorodhesha vizuizi katika mawasiliano shirkishi. Kadhalika, jukumu la Serikali katika uimarishaji wa mawasiliano shirkishi linajadiliwa.

### MADA 1: MAWASILIANO SHIRIKISHI

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo

### SHUGHULI

- Mwelekezi atawaongoza washiriki ili kufasiri **mawasiliano shirkishi**.
- Washiriki wataeleza maana ya neno hilo.
- Mwelekezi atatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa muhtasari maoni ya washiriki.

Chemsha bongo



### Vidokezo Muhimu

#### Mawasiliano

Mawasiliano ni mtiririko wa habari katika njia ya kuwili ambapo mawazo hubadilishwa kati ya makundi mawili ama zaidi. Mawasiliano yanaweza kuwa ya kimazungumzo, yasiyo ya kimazungumzo, maandishi, au matumizi ya ishara na viashiria, hali ambayo maana hutoka kwa huyu na kwenda kwa yule. Mawasiliano ni dhima muhimu ya binadamu kwa sababu inatuwezesha kujumuika sisi kwa sisi, kueleza hisia zetu na kutoa mwelekeo na kuzipa maana shughuli zetu za kila siku.


Mawasiliano yanaweza kufafanuliwa kama upashanaji wa habari kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine na kurejeshwa tena kwa mtu wa kwanza – utaratibu wa kuwasilisha ujumbe kutoka kwa mwasilishaji hadi kwa mpokeaji na kisha kupata majibu. Mawasiliano yanaweza kuwa rasmi au yasiwe rasmi.

Mawasiliano rasmi hufanyika katika taasisi za serikali, kati ya mashirika na mazingira mengineyo rasmi. Ni aina ya mawasiliano inayofuata mfumo fulani na ambayo huundwa na kuelekezwa kwa kanuni fulani. Kwa upande mwingine, mawasiliano yasiyo rasmi ni aina ya kawaida ya mawasiliano inayojumuisha watu wa kawaida bila mifumo yoyote au urasmi. Wakati mwingine huwa ya ghafla, huwa ya hiari na mara nyingi, bila mpangilio. Mawasiliano pia yanaweza kuwezesha kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio, runinga, simu na tovuti mionganoni mwa vingine.

### **Mawasiliano shirikishi**

Msomi Mefalopulos (2007) anafafanua mawasiliano shirikishi kama shughuli inayowezesha ushirika wa watu katika kufanya maamuzi kuhusu masuala yanayoathiri maisha yao. Ni utaratibu unaoweza kukidhi haja fulani na mambo muhimu kwa watu na kwa wakati huo huo kuwawezesha. Mawasiliano shirikishi hupigia upatu ushirika wa washikadau katika viwango vyote katika uchanganuzi wa matatizo, ubunaji wa suluhisho na utekelezaji wa mikakati inayofaa.

Majadiliano ni kanuni kuu katika mawasiliano shirikishi. Mshirika anafaa kuwa na uwezo mzuri wa kusikiliza, mwenye huruma, kuwa na hoja nzito, hiari ya mtazamo chanya, heshima na kujimini kwa ajili ya kushiriki kikamilifu katika mjadala.



*Mchoro wa 1: Mfumo wa Mawasiliano*

## Mfumo wa Mawasiliano Shirikishi

Mfumo huu wa mawasiliano shirikishi unaegemezwa kwa elimu ya Freire kutokea miaka ya 1960. Unahimiza harakati ya hatua ya pamoja na uakisi wa washikadau wanaofaa badala ya kuwasilisha habari sahihi au zinazostahili kwa hadhira fulani. Mfano huu wa mawasiliano shirikishi unahimiza kuwapa uwezo raia kwa kuwahusisha kikamilifu katika utambuzi wa shida, ubunaji wa suluhisho na utekelezaji wa mikakati inayofaa.

## Utaratibu wa Mawasiliano Shirikishi

Mawasiliano shirikishi hufanyika kuitia kwa muafaka wa wahusika katika hatua zilizoorodheshwa hapa chini:

- a. Utambuzi na usajili wa washiriki;
- b. Kusanifu harakati itakayotumika (aghalabu ikijumuisha washiriki katika awamu hii);
- c. Fasiri ya tatizo na uchanganuzi wake;
- d. Ubainishaji na tathmini ya suluhisho m'badala;
- e. Utoaji maamuzi;
- f. Ukamilishaji na uidhinishaji wa suluhi; na
- g. Utekelezaji.

## Aina za Mawasiliano Shirikishi

### a. Ushirika wa juu juu

Katika ushirikishi huu, washikadau wa kimsingi wanahuishwa kwa kuarifiwa kuhusu kitakachotokea au kilichotokea tayari. Majibu ya washiriki ni machache au yanaweza yasikuwepo kabisa na ushirika wao hupimwa kwa kutumia mbinu kama hesabu ya watu waliopo na mchango wao katika mjadala.

### b. Ushirika kwa Mashauriano

Huu ni ushirika wa udondozi ambapo washikadau wanajibu maswali yaliyoulizwa na watafiti na wataalamu wa nje. Mchango wa washirika hutolewa wakati wowote na wala sio tu kuitia kwa mikutano. Hata hivyo, katika uchanganuzi wa mwisho,

utaratibu huu huyabakizia mamlaka ya utoaji maamuzi ya mwisho kwa wataalamu wa nje ambao wana uhuru wa kuhusisha ama kutohusisha mchango wa washikadau.

### c. Kushiriki kwa njia ya Muungano

Hapa, makundi ya washikadau wakuu hushiriki katika majadiliano na kuchanganua malengo ya awali yaliyoamuliwa. Huhitaji uhusika wa dhati katika utaratibu wa utoaji maamuzi ya malengo yaliyoamuliwa. Utaratibu huu unahusisha mawasiliano kati ya wahusika na uimarishaji wa uwezo mionganoni mwa washikadau.

### d. Ushirika wa Upatianaji Uwezo

Katika ushirika wa upatianaji uwezo, washikadau wakuu wana uwezo na nia ya kuanzisha utaratibu huo na pia kuwa mionganoni mwa wahusika katika uchanganuzi. Hali hii inawezesha utoaji wa maamuzi ya pamoja kuhusu kinachofaa kufikiwa na kwa njia gani. Washikadau wakuu ni washirika sawa na wenyewe usemi mkuu katika utoaji wa maamuzi kuhusiana na maisha yao. Katika ushirika huu wa upatianaji wa uwezo, majadiliano hutambua na kuchanganua masuala muhimu mbali na kubadilishana maarifa na tajriba, hivyo basi kupelekea kupatikana kwa suluhisho kwa matatizo ya jamii. Katika aina hii ya ushirika, umiliki na udhibiti wa harakati husalia mikononi mwa washikadau wakuu.



*Jedwali 9: Aina ya Mawasiliano Shirikishi*

## MADA 2: UTARATIBU WA MAWASILIANO

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki **kuorodhesha utaratibu wa mawasiliano.**
- Washiriki wanaorodhesha utaratibu wa mawasiliano.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu katika kunakil mukhtasari wa maoni.



### Vidokezo Muhimu

#### Utaratibu wa Mawasiliano

Mawasiliano thabiti ndio kiungo kikuu cha ubora katika ushirika kwenye mawasiliano. Njia ambayo watu huchukuliana na kuongea na wenzao kuhusu masuala mbalimbali huwa ni chombo muafaka cha kuleta maelewano kwenye jamii. Tayari imethibitishwa kwamba mawasiliano dhaifu hupunguza ubora, hudhoofisha mafanikio, na mwishowe kuzua hasira na kutoaminiana mionganini mwa watu katika shirika fulani.

Sehemu kuu za utaratibu wa mawasiliano ni kama ifuatavyo:

#### 1. Muktadha

Mawasiliano huathirika pakubwa kwa kutegemea mazingira ambamo yanafanyika. Muktadha huo huweza kuwa katika mazingira yanayoonekana ama hata yanayoshikika, kijamii, kikronolojia au kitamaduni. Kimsingi, kila mawasiliano hufanyika katika muktadha fulani. Anayewasilisha huchagua ujumbe wake katika muktadha fulani.

## 2. Muwasilishaji/Msimbaji

Muwasilishaji/Msimbaji ni mtu anayetuma ujumbe. Muwasilishaji hutumia alama (maneno au michoro ama vifaa vinavyoonekana, tovuti na mbinu nyinginezo) ili kupidisha ujumbe na kuibua majibu yanayofaa. Muwasilishaji anaweza kuwa mtu binafsi, kundi au shirika. Maoni, usuli, mbinu ya kuukabili, maarifa, umilisi, na elimu ya muwasilishaji huwa na athari kubwa kwa ujumbe. Alama za mazungumzo na zisizo za mazungumzo zilizochaguliwa huwa muhimu katika kuhakikisha kuwa tafsiri ya ujumbe kwa mpokeaji katika hali iliyokusudiwa na muwasilishaji inafika bila kubadilika.

## 3. Ujumbe

Ujumbe ni wazo kuu ambalo muwasilishaji hulenga kuwasilisha. Hii huwa ishara ambayo huibua jawabu kutoka kwa mpokeaji. Utaratibu wa mawasiliano huanza na uamuzi kuhusu ujumbe unaofaa kuwasilishwa. Ni muhimu kuhakikisha kwamba lengo kuu la ujumbe limewekwa wazi.

## 4. Chombo


Chombo ni njia inayotumiwa kubadilishana/ kutuma ujumbe. Ni lazima muwasilishaji achague njia mwafaka ya kutuma ujumbe huo, vinginevyo, ujumbe unaweza kukosa kuwafikia wapokeaji walio lengwa. Uteuzi wa njia mwafaka ya mawasiliano ni muhimu katika uboreshaji wa ujumbe na ufasiri wake kwa wapokeaji. Uteuzi huu wa njia ya mawasiliano hutegemea sifa za mawasiliano. Mathalan, njia ya maandishi huteuliwa kama ujumbe unafaa kuwasilishwa kwa kundi dogo la watu ilhali njia ya kimazungumzo huchaguliwa ikiwa majibu ya haraka kutoka kwa mpokeaji yanahitajika na pakitokea kutolewana basi suluhu hupatikana papo kwa hapo.

## 5. Anayepokea ujumbe /Msimbuaji

Anayepokea ujumbe/Msimbuaji ni mtu yule mlengwa halisi wa ujumbe, kusudiwa au dhamiriwa. Kiwango cha uelewa ambacho mpokeaji huuelewa ujumbe hutegemea pakubwa mambo kadha kama vile maarifa ya muwasilishaji, maitikio yao kwa ujumbe, na utegemezi wa muwasilishaji kwa mpokeaji.

## 6. Majibu

Majibu ni sehemu kuu ya utaratibu wa mawasiliano kwa sababu huruhusu muwasilishaji kuchanganua ufaafu wa ujumbe. Humsaidia muwasilishaji kuthibitisha kama kweli mpokeaji alifasiri ujumbe huo vyema. Majibu yanaweza kuwa kwa mazungumzo (kupitia kwa maneno) au yasiwe katika mazungumzo (katika mfumo wa tabasamu, miguno, n.k). Inaweza kuwa kwa njia ya maandishi kama vile kupitia kwa memoranda, ripoti, n.k.



*Mchoro 2: Utaratibu wa Mawasiliano*

### MADA 3: UMUHIMU WA MAWASILIANO KATIKA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 20.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza washiriki ili kuorodhesha umuhimu wa mawasiliano bora katika uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki kuorodhesha umuhimu huo.
- Mwelekezi kutumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa ufupi maoni ya washiriki.



#### Vidokezo Muhimu

##### Umuhimu wa mawasiliano shirikishi katika uwiano na utangamano wa kitaifa

- a. Huimarisha mabadiliko kuhusiana na mitazamo na mienendo ya kijamii na kuzisaidia jamii kubaini nafasi endelevu na njia za upatikanaji wa suluhu thabiti zilizo karibu nao;
- b. Huwapa fursa washikadau muhimu;
- c. Hutekeleza jukumu la upatanishaji katika utatuaji mizozo, kufikia maelewano na kuafikiana kuhusu sera na hatua zinazofaa kuchukuliwa;
- d. Huibua taarifa zinazofaa kuandaa sera kupitia kwa ushirika wa raia wa kawaida katika kuleta pamoja jamii, mijadala ya umma na midahalo ya sera;
- e. Inajumuisha makundi yote katika ajenda na malengo ya taifa;
- f. Inahamasisha kuhusu haki, majukumu na wajibu;
- g. Inawezesha kugawana taarifa zinazofaa katika uundwaji wa sera na utekelezaji wake; na

- h. Inaunda jamii yenyewe usawa, ujamaa, isiyo na mapendeleo na yenyewe haki.

## MADA 4: VIZUIZI KATIKA MAWASILIANO SHIRIKISHI

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi aongoza washiriki kuvifahamu vizuizi katika **mawasiliano shirikishi**.
- Washiriki wabaini vizuizi hivi.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kuorodhesha kwa muhtasari maoni ya washiriki.




### Vidokezo Muhimu

#### Vizuizi katika mawasiliano shirikishi

- a. Lugha;
- b. Kujikinga dhidi ya tetesi za matokeo ya wapokeaji ujumbe na mitazamo mibovu;
- c. Kufasiri visivyo lugha ishara ya mwili na mbinu nyingine za mawasiliano yasiyo ya kimazungumzo;
- d. Ukosefu wa subira, hasa, mhusika mmoja anapoanza kuunda majibu kabla hata ya kuelewa ujumbe kutoka kwa muwasilishaji; na
- e. Kutojali tamaduni – jamii huundwa kutokana na tamaduni mbali mbali ambazo huwafanya watu kuwa na mitazamo tofauti, maadili, desturi, mila na miiko. Udhahilishaji wa kundi fulani nao unaweza kusababisha kutoelewana.

#### Jinsi ya kudumisha mawasiliano shirikishi

- a. Kuchemsha bongo – kutoshiriki kikamilifu ili kuruhusu wanaoshiriki wajadili maswala fulani;
- b. Shughuli za makundi – Hii huhimiza ushirika na kutangamana kwa washiriki. Wakati mwingine shughuli ya makundi hufurahiwa kwa sababu ya mchango wa washiriki wenzao;
- c. Uwezeshaji – haki za kibinadamu, elimu kwa umma na uwezeshaji wa kiuchumi ni shughuli inayoweza kutimizwa kuititia makongamano na semina;
- d. Washiriki wanafaa kufunzwa maarifa ya kujadili mbinu za kupata muafaka na hatua ziorodheshwe ili kuwasaidia katika shughuli hii;
- e. Matumizi ya mifumo ya utawala wa mitaa kama vile vingozi wa kijamii, mabaraza ya machifu, wanamaoni kwenye jamii na asasi za kidini, vyote vinafaa kuhimizwa;
- f. Uchunguzi wa kuridhisha kutumika kama mbinu nzuri ya kutafuta njia faafu, matokeo bora, ujuzi wa juu na huduma. Kama mwelekezi, tumia uchanganuzi wa kuridhisha ili kuthamini washiriki na kuimarisha yale mambo mazuri;
- g. Tumia shughuli zinazoweza kuwashirikisha wanajamii kama vile michezo, uigizaji, maonyesho na vichekesho, mionganini mwa mbinu nyinginezo.
- h. Tumia majibu kutoka kwa vyombo vya habari – majorida, barua pepe n.k.; na
- i. Wezesha mifumo ya kiasili katika jamii – kwa mfano, unaweza kualika wazee kutoa hotuba juu ya masuala yanayohusu uwiano na utangamano wa jamii.



## MADA 5: JUKUMU LA SERIKALI KATIKA MAWASILIANO SHIRIKISHI

**Muda:** Dakika 10

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi awaongoza washiriki ili kuorodhesha **jukumu la Serikali katika mawasiliano shirikishi.**



- Washiriki wanaorodhesha majukumu ya Serikali.

Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kuorodhesha kwa muhtasari maoni ya washiriki.

### Vidokezo Muhimu

#### Jukumu la Serikali katika mawasiliano shirikishi

Serikali hutekeleza majukumu yafuatayo katika uimarishaji wa mawasiliano shirikishi:

- Kuifahamisha jamii kuhusu mielekeo ya sera zake;
- Kushauriana na jamii kama njia mojawapo ya utaratibu wa kuunda sera ya serikali au kuimarisha ufahamu na uelewa wa jamii;
- Kushirikisha jamii kwa kutumia mbinu mbali mbali ili kuhakikisha kwamba maswala na mawazo yanaeleweka na kuzingatiwa kama sehemu ya utaratibu wa utoaji wa maamuzi;
- Kushirikiana na jamii kwa kujenga mtagusano kwa lengo la kubuni njia m'badala na kutoa mapendekezo;
- Kuiwezesha jamii ili wajisaidie kujifanyia maamuzi, kutekeleza na kusimamia mabadiliko; na
- Kuunda mkakati wa mawasiliano ili kuwezesha majadiliano, majibu na kubadilishana mawazo kuhusu uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Marejleo**

- Atsen J., (1994) Africa Communication Development and the Future. Nairobi, Kenya:  
URTN Program Exchange Centre
- Ainslie Rosalynde, (1967) The Press in Africa: Communications Past and  
Present. New York, USA: Walker and Coy
- Ake Claude, (1996) Democracy and Development in Africa. Washington  
DC: Brookings
- Bhabha Homi, (1994) The Location of Culture. New York: Routledge  
success. Houston, Texas: Dane
- Doob Leonard W., (1961) Communication in Africa: A Search for  
Boundaries. New Haven: Yale University Press
- Guy Bessette and C. V. Rajasunderam, (1996) A West African Agenda.  
Ottawa: International Development Research Centre
- IFAD, (2010) the IFAD Adaptive Approach to Participatory Mapping: Design  
and Delivery of Participatory Mapping Projects. Rome: IFAD
- Mefalopulos Paolo and Chris Kamlongera, (2004) Participatory  
Communication Strategy Design. Rome: Food and Agriculture  
Organization of the United Nations
- Obeng Samuel Gyasi & Beverly Hartford, (2008) Intercultural  
Communications. New York: Nova Science Publishers
- Obeng Samuel Gyasi & Beverly Hartford, (2008) Political Discourse  
Analysis. New York: Nova Science Publishers
- Obeng Samuel Gyasi & Beverly Hartford, (2008) Topics in Political  
Discourse Analysis. New York: Nova Science Publishers
- Saik Yoon Chin, (1996) Participatory Development Communication.
- Tufte Thomas and Paolo Mefalopulos, (2009) Participatory  
Communication: A Practical Guide. Washington: The World  
Bank

## SOMO LA 7: UDHIBITI NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA KUIMARISHA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanahitajika kuwa na maarifa yanayofaa, ujuzi na mitazamo muhimu ya udhibiti na utatuzi wa migogoro.

### Utangulizi

Somo hili linajenga ufahamu wa kimsingi udhibiti na utatuzi wa migogoro. Pia linashughulikia mitazamo mbalimbali kuhusu udhibiti na utatuzi wa migogoro.

### MADA 1: UFAFANUZI WA MAANA YA MANENO MGOGORO, UDHIBITI WA MGOGORO NA MANENO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYA

**Muda:** Dakika 15

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, projekta (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza washiriki kutoa maana ya maneno **mgogoro, udhibiti wa mgogoro na maneno mengine yanayohusiana na haya.**
- Washiriki wanaeleza uelewa wao kuhusu maneno haya.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kuorodhesha kwa muhtasari maoni ya washiriki..



### Vidokezo Muhimu

#### Ufafanuzi wa neno Mgogoro

Wasomi mbalimbali wanatoa ufanuzi tofauti tofauti wa neno mgogoro. Kwa hivyo kuna maelezo mengi ya neno mgogoro kama kulivyo na wasomi wengi wa masuala ya migogoro. Baadhi ya maelezo hayo yanaweza kuelezwa katika njia rahisi kama zifuatazo:

- Kutopatana, uhasama, mabishano, ugomvi, migongano, mikwaruzano na kutolewana au kutengana baina ya watu wawili au zaidi;

- b. Kung'ang'ana au mashindano baina ya watu wawili au zaidi kuhusu maadili, hadhi, mamlaka au rasilmali haba. (Coser, 1967:1);
- c. Mienendo isiyofanana ambayo malengo yake yanaonekana kuwa tofauti;
- d. Mahusiano yaliyovurugika;
- e. Aina ya mashindano ya kimakusudi kuhusu rasilmali ambapo washindani hawakusudii tu kuwapiku wenzao bali kuwaondoa katika mashindano au kuwaumiza, ili kuwasimamia au kuwanyima kitu fulani kinyume na mapenzi yao (Williams 1970); na
- f. Kauli ya kutolewana kuhusu kitu fulani muhimu kwa pande zote zinazozozana.

## MADA 2: SURA YA MIGOGORO NA VISABABISHI VYAKE

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, projekta (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza washiriki **kupigia darubini sura ya migogoro na visababishi vyake.**
- Washiriki wanatalii sura ya migogoro na visababishi vyake.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kuorodhesha kwa muhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Sura ya Mgogoro ('Sura' 3 za Migogoro)

Mgogoro umefafanuliwa kama wa kiasili, wa kawaida na ule usio na athari chanya au hasi.

- a. Mgogoro unaweza kuwa wa kiasili kwa sababu umekuwepo na bado ungalipo na hauwezi uondolewa. Migogoro ilianza tangu ulimwengu uliopoumbwa na itaendelea kuwa nasi kwa maisha yetu yote. Kwa hivyo ni muhimu kuitazama kama matukio asili na ambayo yanafaa kukabiliwa yanapojitokeza.
- b. Mgogoro utaonekana kuwa si chanya au hasi kwa sababu unaweza kuathiri kila mtu bila kujali umri, tabaka la kijamii, rangi, jinsia au sifa zozote zinazofautisha.
- c. Kwa kuhitimisha, mgogoro ni tukio la **kawaida** linalotokea wakati wowote na ni sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Ukweli ni kwamba mgogoro hauwezi ukapuuzwa lakini unafaa kukabiliwa wakati wowote unapozuka.

### Viwango vya Migogoro

Kimsingi, ni muhimu sana kufahamu kwamba kutokana na uchangamano wa swala hili la migogoro, huenda ikawa vigumu kuweka migogoro hii katika viwango mbali mbali.

Kwa sababu ya mwongozo huu, viwango vifuatavyo vinaweza kutumika:

- a. Mgogoro wa kibinafsi (pia huitwa mgogoro wa ndani kwa ndani): Huu ni mgogoro ambaa mtu huwa nao ndani yake mwenyewe ama tuseme ni mgogorobin afsi. Huathiri mitazamo, hisia na maamuzi yanayofanywa na mtu binafsi;
- b. Mgogoro baina ya watu: Huu unarejelea tofauti kati ya watu kwa kiwango cha watu binafsi;
- c. Mgogoro wa kundi: Huu unahusu kutolewana kati ya wanachama wa kundi. Unaweza kuhusu sera, mikakati, maadili, viwango vya ubora au hata malengo;
- d. Mgogoro baina ya makundi: Huu unahusu kutolewana baina ya makundi; na
- e. Mgogoro baina ya nchi: Huu ni mgogoro kati ya nchi tofauti.

### **Visababishi vya Migogoro**

- a. Kulimbikiza mamlaka ya nchi kwa sehemu ya nguzo Kuu ya Serikali
- b. Kutoheshimu utawala wa sheria;
- c. Mashindano juu ya uchache wa rasilmali;
- d. Ugavi usiosawa wa rasilmali za umma;
- e. Usimamizi duni wa rasilmali, hasa ardhi;
- f. Ukiukaji wa haki za kibinadamu kwa kiwango kikubwa;
- g. Ukosefu wa uwazi na uwajibikaji katika harakati za uchaguzi;
- h. Mfumo dhaifu wa mahakama na uzingatifu wa ubora wa makabila fulani dhidi ya utambulisho wa utaifa na uraia;
- i. Ufisadi;
- j. Utawala mbaya wa serikali;
- k. Mapendeleo kwa watu wa ukoo; na
- l. Uingizaji wa siasa katika ukabila na dini.

### MADA 3: MIKAKATI YA UDHIBITI WA MIGOGORO

**Muda:** Dakika 35

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, projekta (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi anaongoza washiriki ili kubaini **mikakati ya kudhibiti migogoro**.
- Washiriki kubaini mikakati ya kudhibiti migogoro.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kuorodhesha kwa muhtasari maoni ya washiriki.



#### Vidokezo Muhimu

##### Mikakati ya Kudhibiti Mgogoro

###### a. Uepukaji

Watu huepuka mgogoro kwa kutoroka au kuukimbia, hali inayomaanisha kukataa au kujiondoa katika hali ya mgogoro. Watu wanapoepuka mgogoro, hawaridhishi matakwa yao binafsi au ya pande nyingine. Hii ni hatua hasi kwani huhakikisha kuwa pande zote zimegawana hasara (zote tupoteze). Katika dunia ya wanyama, mzee kobe hukana kuwepo kwa tatizo kwa kuingiza kichwa chake ndani ya kaka lake huku mbuni kwenye kaida na ngano za kale, anasemekana alificha kichwa chake ndani ya changarawe. Mtu anayekwepa kukabili shida katika familia bado atakutana na shida hiyo siku ifuatayo. Mtu anayekwepa kutatua shida ya ulevi au uraibu wa dawa za kulevyia kwa kuendelea kulewa ama kubwia unga bado atalazimika kuishi na shida hiyo.

###### b. Kuvumilia

Huu ni moyo wa kuwapa walio katika upande mwingine kile wanachotaka kwa kuafikiana nao badala ya kuandama imani zako binafsi na vishawishi. Hii ni hali yenye matokeo ya nipoteze-nawe-ushinde (*nipoteze/ushinde*), kwa kuwa upande mmoja huachilia matakwa yake na kukubali ya upande tofauti bila kuzingatia mahitajio na matamanio ya kibinafsi.

### c. Ushindani


Hii inahusisha kutumia nguvu ili kumshinda mwenzako katika kufanya maamuzi kwa lengo la kupata unachotaka kwa njia zozote zile. Lengo hapa likiwa ni kushinda huku upande mwingine ule ukipoteza kwa kuthamini sana maoni na shauku zako huku ukidunisha thamani ya upande pinzani. Utaratibu huu huwa na matokeo ya *nishinde-nawe-upoteze* (*nishinde / upoteze*).

### d. Kulegeza msimamo

Hii huwa na matokeo ya *shinda-nami-nishinde* (*sote tushinde*) ambapo pande zote zinazozozana huafikia maridhiano ya nusu kwa nusu kwa kushinda kidogo na kupoteza kidogo kwa wakati mmoja.

### e. Kushirikiana

Katika utaratibu huu, pande zote zinazozozana hung'ang'ana ili kuridhisha matakwa yao kwa kutafuta mambo m'badala yanayoweza kuzaa manufaa makuu yanayowaridhisha wote. Hali hii husababisha matokeo ya *shinda-nishinde* (*shinda-na mimi-nishinde*). Jedwali lililo hapa chini linaonyesha tofauti ya kujiali kibinafsi ikilinganisha mahusiano ya wakati wa mgogoro.



Mchoro 4: Mikakati ya kudhibiti Migogoro

Kulingana na mchoro huo, matakwa ya mtu binafsi (*kujijali mwenyewe tu*) yanapowekwa juu, watu huamua kushindana ili kupata wanachotaka kwa kutumia njia zozote zile walizonazo. Hali hii hulenga upatikanaji wa matokeo au majibu. Kwa upande mwingine, swala la kujali uhusiano linapokuwa juu, watu hukirimiana, wakiandaa hali ya kujiondoa. Sehemu ya pembeni zaidi inaonyesha hali ambayo mahusiano ya pande zote husika na ya kibinafsi yako chini. Katika hali hii, pande husika hukwepa masuala yaliyopo na badala yake kuikimbia shida hiyo. Mchoro huu pia unaonyesha mbinu za ulegezaji wa msimamo na ushirikiano kama chombo, huku mahusiano ya binafsi na yale ya pamoja yakiashiria ushirikiano ukijali pande zote mbili. Hali hizi mbili huzua matokeo yanayotiririka.

Kila mbinu kati ya hizi inaweza kufafanuliwa katika vigezo viwili: *Kujitetea* (*kujipigania*) na kushirikiana. Hakuna moja kati ya mbinu hizi isiyo sahihi katika matumizi, lakini pana nyakati zisizofaa au zinazofaa kuzitumia. Sehemu zifuatazo zinafafanua mifano mitano.

Habari hizo zinaweza kusaidia kila mwanakundi kufafanua mfano wake wa kukabili mgogoro.

*Jedwali 10: Kuelezea Mitindo ya Migogoro*

Mitindo ya mgogoro	Manufaa	Hatari
Kushindana	Ushindani unaweza kutumika pale ambapo upande mmoja una nguvu zaidi na wala hautaki kulegeza msimamo ( <i>k.m. jitihada za kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni kwa mataifa ya Afrika, au makundi ya wanawake kukabili jamii inayotawaliwa na wanaume kwa ajili ya kupata haki ya kupiga kura</i> ).	Mbinu mojawapo ya kukabiliana huwa kwa matumizi ya fujo, na hii mara nyingi husababisha ghasia zaidi.
Kulegeza msimamo	Hapa pande zote zinaheshimu kila mmoja na kupoteza kiasi fulani na hii huzuia kuvuruga mahusiano.	Pande zote zinapoteza nusu ya matakwa yao na kupata nusu.

Kushirikiana	Pande zote zinaonyeshana heshima. Zinafanya mambo kwa pamoja kwa minajili ya matokeo mazuri kwa kila mmoja wao. Mbinu hii huzalisha ' <i>matokeo ya shinda-nishinde</i> '.	Mbinu hii huwa na kuhimili uchungu na mara nyingi huwa ngumu kwa wanaohusika. Inahitaji kujitolea kutimiza harakati hiyo na uvumilivu, hali ambayo ni nadra sana kwa watu wanaozozana.
Uepukaji	Inaweza kutumika katika mazingira ambayo hakuna mahusiano baina ya pande zote au uwezekano wa mahusiano ya siku za usoni.	Haiwezi kutumika katika mazingira umbayo pande zote zina uhusiano wa karibu. Huwa inachelewesha tu yale yasiyoepekika. Pande zote huja kuzozozania suala hilo siku za baadaye kama suala hilo litapuuzwa na ' <i>kutiwa mvunguni</i> '.

Kuna matokeo aina nne yanayowezekana panapotumika mitindo hii.

#### a) Poteza- Nipoteze (*Tupoteze sote*)

Hutokea wakati pande zote zinazozozana hazitimizi mahitaji yazo. Mara nyingi, mzozo huendelea au huchipuka baadaye. Hali hii inaweza kufanyika kama kuna mgogoro wa kinyumbani pale ambapo mke hukubali kudhulumiwa/kutendewa mabaya na mumewe.

#### b) Nipate-nawe-ukose (*Nishinde-nawe-upoteze*)

Hapa upande mmoja katika mgogoro huridhisha matakwa yake huku mwenzake akikosa. Mfano mzuri ni kesi ya kortini.

#### c) Shinda - na mimi - nishinde (*Sote tushinde*):

Hapa ni pale ambapo pande zote zinazozozana hushirikiana kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya kila mmoja. Iwapo mtu mwenye mtindo wa kushindana anazozana na mwengine wa mtindo wa kuipuka, mshindani ana nafasi kubwa ya '*kushinda*' huku anayeepuka '*akipoteza*' kwenye mgogoro huo. Watu wawili wenye mtindo wa kushirikiana wanapozozana, kuna uwezekano mkubwa wa matokeo kuwa '*shinda-na mimi-nishinde*'.

#### d) Poteza-nishinde, shinda-nipoteze

Hapa huwa kunakuwa na hali ya kulegeza msimamo ambapo upande mmoja hupoteza kidogo na kupata kidogo. Huwa kunakuwa na hali sawazishi kwa pande zote mbili.

## NJIA ZA KUSULUHISHA MIGOGORO

Kila mara mgogoro unapotokea watu hulazimika kutafuta suluhisho. Hizi ndizo hatua ambazo huamua matokeo ama hatima ya mgogoro.

Kimsingi, hatua hizi zinaweza kugawika katika makundi matatu:

**a) Mwitiko wa kujiondoa:**

Huhusisha kukataa kukabili mgogoro kwa kujiondoa kuitia kwa kukana au kukanusha, kujitoa au kuepuka kabisa.

**b) Mwitiko wa kupigana:**

Hapa watu hukabili mgogoro kwa kutumia nguvu ili kushinda upande mwingine unaohusika katika mzozo, kwa kutumia nguvu au kuzua ushindani.

**c) Mwitiko wa kujadiliana:**

Hii huhusisha matumizi ya majadiliano kama njia ya kutafuta suluhu la tatizo kwa kurejelea mbinu zinazoridhisha kila upande katika mgogoro kama vile mashauriano na mapatano.

Kutolewana kunapozuka, pande zote zitajaribu kusuluhiha suala hilo kuitia kwa mojawapo ya mbinu zifuatizo:

**a. Mbinu inayoegemea mamlaka**

Katika hali hii, mamlaka yanamaanisha uwezo wa kufanya mtu mwengine afanye jinsi unavyopenda bila ya hiari yake. Mamlaka yanaweza kuwa halali au haramu. Utaratibu huu huamua ni nani aliye na nguvu, hali inayomaanisha kuwa upande wenyewe nguvu ndio huamua matokeo yanayopatikana.

Utaratibu huu aghalabu hutumika kwa njia halali na mtu aliye katika nafasi fulani kwenye mamlaka, kama vile: Utawala wa mkoa, polisi, wazazi, walimu, n.k, kwa lengo la kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kwa upande mwingine, utaratibu huu hutumika visivyo au/na kiharamu ikiwa mamlaka yanapatikana kutokana na utajiri, dini, utamaduni, umri, tabaka la kijamii, n.k, yakitumika kukandamiza wasiobahatika zaidi katika jamii. Katika dunia ya sasa, kazi hii hutekelezwa na polisi au jeshi ambalo hutumia mamlaka halali kusuluhiha mizozo. Wakati mwingi, Serikali, zimetumia nguvu kupita kiasi kuzima watawaliwa. Tatizo la mbinu hii ni kwamba huwa ni ghali, sio mbinu yenye utu na wala haitafuti kiini cha tatizo hilo. Matokeo au amani inayodaiwa kutokana na mbinu hii huwa ni ya muda tu na tena ni hasi.

### b) Mbinu inayoegemea Haki

Mbinu hii hutegemea sheria, desturi na maadili ya shirika au jamii husika. Katika hali fulani, maamuzi hufanywa kwa kutumia mitindo huru iliyowekwa kubaini usawa au katika mahakama, madai ya nani ndiyo yaliyo halali zaidi. Katika jamii za kitamaduni, huwa kuna desturi na sheria zilizowekwa ambazo huongoza utatuaji wa mizozo inayohusiana na ndoa, uhalifu na kadhalika. Katika dunia ya sasa, mbinu hii hutumiwa hasa kwenye mahakama ili kubaini ni nani aliye sahihi na yupi asiye sawa. Upande ulio sahihi hushinda huku ule upande mwingine ukipoteza. Utaratibu huu hufuata sheria. Tatizo la mbinu hii ni kwamba upande mmoja hypoteza huku mwingine ukishinda na huu sio utaratibu mzuri kwa lengo la mapatano na utatuaji wa migogoro.

### c) Mbinu Inayoegemea Maslahi

Utaratibu huu hulenga kuoanisha haja, matamanio na matakwa ya pande zinazozozana. Pande zinazozozana hutafuta njia bora zaidi ambayo maslahi yao yatativimizwa na vile vile kuimarisha mahusiano. Utaratibu huu hulenga matokeo ya *shinda-na mimi-nishinde* ambapo kila mmoja huwa mshindi. Maslahi ya kila upande unaozozana huorodheshwa na kujadiliwa.

Mbinu hizi tatu huzipa pande hasimu fursa ya kuchagua mifumo mbalimbali inayoweza kutatua tofauti zazo. Kadhalika, njia hizo huweza, mara nyingine, kutumika kwa pamoja. Kila moja huwa na uzuri na udhaifu wake. Muktadha unaotumika na pande hizo, wakati mwingine, huamua aina ya mbinu itakayokuwa bora zaidi.

### Njia za Kusuluuhisha Migogoro

Mbinu zilizopo za kutatulia migogoro huwa ni za aina mbili:

**Mbinu za upatanisho (mahusiano ya kidiplomasia)** inamaanisha mbinu za utatuzi ambapo mamlaka ya kufanya maamuzi kuhusu migogoro husalia kwa pande zinazozozana. Kwa hivyo zinaweza kukubali au kukataa maamuzi yaliyofikiwa kama upande mmoja unahisi haukuridhika. Hali hii huhusisha mashauriano, mapatanisho, maridhiano, usuluuhishaji, kusaidiana na hali kadhalika usuluuhishaji wa migogoro bila ya kutumia vikwazo ama masharti.

### Mbinu zisizokuwa za kidiplomasia

Zinahusisha matumizi ya nguvu, hukumu na utatuzi wenyewe vikwazo na masharti. Katika hali hii pande husika katika migogoro hutupilia mbali mamlaka yao ya kufikia uamuzi na kuachia mtu wa nje kutoa maamuzi, na hivyo pande zote husika zikalazimika kukubali matokeo hayo.

## 1. Mbinu za Kisheria

- a. **Utumiaji wa nguvu:** Hapa, upande mmoja huzidi mwengine kwa kutumia nguvu au fujo. Mbinu hii hutumika hasa na serikali ili kudhibiti mzozo. Kwa mfano, wakati wa maandamano ya fujo na ghasia, walinda usalama wamezoea kutumia nguvu ili kurejesha utulivu. Kadhalika, nguvu zinaweza kutumika kutawanya makundi mawili au watu wanaopigana. Mbinu hii haitafuti kiini cha shida na hivyo huwa ni ya muda tu, huku ikilenga kuyapunguza makali ya mgogoro mpaka ule unaoweza kukabiliwa. Watu wanaohusika katika harakati kama hii huwa wachache. Katika nchi yoyote ile, polisi hutumia mamlaka halali ili kulazimisha pande zinazozozana kuachana na ghasia.
- b. **Maamuzi ya kisheria:** Pia huitwa mfumo wa mahakama; mbinu hii ya kisheria huwa mfumo wa hali ya juu unaotekelawa katika mahakama za kisheria. Jaji au hakimu asiyekuwa na mapendeleo (mwamuzi) aliye wakili/mwanasheria aliyefunzwa kitaalamu husikiliza ukweli katika mzozo, na kwa msingi wa kisheria/kanuni zilizopo hulazimisha uamuzi unaotekelawa kwa kuzawadia asiyenye na kosa na kumuadhibu mhalifu/aliye na kosa. Mwamuzi huwa na mamlaka ya kulazimisha aliyopewa na nchi na hivyo hulazimisha maamuzi yanayoingiliana na sheria. Hapa, pande hasimu hazina uwezo wa kuchagua msuluhishi wake na hivyo mwamuzi huwa hazingatii hisia (maadili, imani, haja) lakini huzingatia tu masuala yanayohusiana na sheria. Yaani, maamuzi huegemea ushahidi unaoshikika kisheria na wala hayafuati masuala ya mahusiano.
- c. **Usuluhishaji:** Katika usuluhishaji, pande zinazozozana huchagua msuluhishi kwa pamoja. Msuluhishi aweza kuwa wakili/mwanasheria mtaalamu asiyeegeemea upande wowote, ambaye katika sheria ya upatanishaji ameruhusiwa kisheria kusikiza maoni ya pande zote na kulazimisha uamuzi.


## 2. Mbinu za Kidiplomasia (*Upatanisho*)

- a. **Kuridhiana:** Hapa upande wa nje (*nafsi ya tatu*) huwa mpatanishi ambapo pande husika hukutana na kusuluhisha tofauti zao. Hali hii hufanyika kama mgogoro umezua mihemko na hisia kali hivi kwamba pande zote husika haziwezi kuonana ana kwa ana. Kwa hali hii, huwa na hisia za kutoaminiana na kudhaniana katika pande zote hasimu. Upande huo wa tatu (msuluhishi) kwa hivyo hupeleka ujumbe kwa kila kundi, kwa matarajio kuwa kila kundi litatuliza hamasa zake na kupunguza shauku, kuwezesha kuwepo kwa nafasi ya mkutano wa makundi haya hasimu na kisha kusuluhisha tofauti zao.
- b. **Uelekezaji:** Mwelekezi wa upande wa tatu husaidia kuimarisha mawasiliano baina ya makundi hasimu hasa kupitia kwa mikutano. Hali hii huwa ni utaratibu uliopangwa, ambapo upande wa tatu usiokuwa na mapendeleo na usioamrisha linalofaa kufanywa (*mwelekezi*), kwa kutumia utaratibu

uliowekwa anahimiza kuwepo mtiririko thabiti wa mawasiliano baina ya makundi hayo hasimu. Mara nyingi hii hujumuisha kuwapasha yanayostahili kujadiliwa, kuwezesha mawasiliano, kuwezesha kusemezana na kuongoza utaratibu mzima. Uwezeshaji hutumika kuelezea mbinu na mtindo wa mwasilishaji katika shughuli ya kufundisha. Uwezeshaji huwa na malengo sawa na upatanishaji, lakini haifuati utaratibu mkali. Msuluhishaji anaweza kuwa mtu asiyehusika na mgogoro au mtu kutoka mojawapo ya makundi anayeweza kutoa mwelekeo na kujizuia katika kuegemea upande wowote wa majadiliano.

- c. **Majadiliano:** Hapa pande husika zinakutana zenyewe ili kutatua tofauti zao. Ni utaratibu wa kujitoa kwa hiari ili kujadili kwa lengo la kusuluhisha tatizo/kufanya maamuzi kwa pamoja, ambapo makundi mawili au zaidi hukutana na kujadili matatizo yao, na kujaribu kufikia suluhi. Ni uhusiano wa kujaribu kuafikiana baina ya makundi mawili au zaidi (*wasuluhishaji*) yaliyo na mgogoro/maslahi dhahania au halisi.
- d. **Upatanishaji:** Hii inamaanisha kuingilia kati kwenye mzozo au majadiliano na kundi lisilohusika katika mgogoro (kundi la nje) lisilopendelea na kuegemea upande wowote na ambalo halina mamlaka makuu ya kuamrisha au kufanya maamuzi, ili kusaidia makundi hasimu kujitoa kwa hiari kufikia usuluhishaji wa mgogoro kwa njia inayokubalika na yenye manufaa kwa wote wanaozozana. Kwa ufupi, haya huwa ni majadiliano yanayojumuisha pia kundi la nje lenye ufahamu wa utaratibu madhubuti wa majadiliano. Katika jamii nyingi za Afrika, wazee wamekuwa katika mstari wa mbele katika majukumu yao ya kupatanisha. Mpatanishi husaidia makundi husika kushirikiana katika shughuli zake na kuboresha majadiliano yao kwa lengo la kuafikiana.

### MITINDO YA USULUHISHAJI WA MIGOGORO



Jedwali 11: Mitindo ya usuluhishaji wa migogoro

## MADA 4: MANUFAA YA UDHIBITI WA MIGOGORO

**Muda:** Dakika 30

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi kuwaongoza washiriki ili kuyafahamu manufaa ya **udhibiti wa migogoro**.
- Washirika wanabaini manufaa haya.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa ufupi maoni ya washiriki.



### Vidokezo muhimu

#### 1. Upande Mzuri (Chanya) wa Migogoro

- a. Migogoro husaidia kuibua utambulisho na uhuru wetu. Katika hatua za mapema za maisha, husaidia mhusika kuthibitisha utambulisho wake binafsi kinyume na dhana ya kijumla ya matamano, imani na mienendo ya wale wanaomzunguka.
- b. Kasi ya migogoro huonyesha ukaribu na umuhimu wa mahusiano. Mahusiano ya kimapenzi huhitaji uonyeshaji wa hisia kali zinazokinzana, kama vile kupenda au hata kukasirika. Uwepo wa hisia hizi mbili katika mahusiano huunda upeo wa juu hasa mzozo unapoingia. Na ijapokuwa upana wa hisia hizo unaweza kutisha kuvuruga uhusiano, unaweza pia kupima uzito na umuhimu wa uhusiano hasa ikiwa utakabiliwa kwa njia inayofaa.
- c. Mgogoro unaweza kujenga mahusiano mapya kwa kuleta pamoja watu waliokuwa hawana uhusiano wowote hapo awali. Katika harakati ya mgogoro na usuluhishaji wake, punde husika zinaweza kugundua maslahi yao kwa pamoja na kisha kushirikiana ili kudumisha uhusiano huo ulioanzishwa.
- d. Mgogoro unaweza kuzua uhusiano, kwa mfano mahasimu wanapoungana ili kuandama lengo moja au kufukuza hatari inayowaathiri wote pamoja. Mara nydingi, hali hiyo huleta uwezekano mkuu wa ufanisi, na uadui uliokuwepo awali kuzimwa huku pande zilizozozana zikiendelea kushirikiana kufikia malengo haya makubwa.

- e. Mgogoro hutekeleza jukumu kama lile la vali ya kuleta usalama, ambao hupunguza hofu na kuimarisha uhusiano. Mahusiano yanayozima chuki huimarika na kuwa thabiti jinsi muda unavyosonga. Makabiliano wakati wa mzozo mbele ya msuluhishaji, wakati mwingine husaidia kutoa uhasama nje na hivyo hupunguza hofu katika mahusiano.
- f. Mgogoro husaidia pande husika kupima nguvu ya kila mmoja na hivyo huweza kutekeleza jukumu la kugawa mamlaka katika mfumo wa utawala. Migogoro huhusisha baadhi ya njia chache zinazowezesha pande husika kujipima nguvu. Ikiwa hapana usawa wa kimamlaka, upande mmoja unaweza kujitahidi ili kuongeza nguvu zao za ndani (binafsi) hali ambayo baadaye hubadilisha mfumo wa mamlaka katika utawala uliokumbwa na mazozano.
- g. Migogoro huunda na kudumisha utambulisho wa kila kundi kutokana na mipaka dhahiri inayoundwa ili kutofautisha '*kundi la ndani*' na '*kundi la nje*'. Hii inaweza kusaidia wahusika kuelewa jinsi walivyo katika kundi fulani na kisha kuwaleta pamoja ili kuchukua hatua ya kutetea maslahi ya kundi husika.
- h. Mgogoro huimarisha uwiano wa kundi kupertia kwa usawazishaji wa maswala na imani zao. Wanachama wa kundi lililo katika hatari hujiweka pamoja huku waasi na wapinzani waking'olewa. Katika hatua hii, masuala na imani huwekwa dhahiri. Hii hatimaye huzua mwelekeo wa kundi ulio bayana na unaokubalika kwa wote.
- i. Mgogoro hujenga ama kubadilisha sheria, desturi, kanuni na taasisi kwa kuzua masuala. Kutoelezea shida ama mahangaiko husababisha mambo kubakia kama yalivyo.

### **Matokeo ama Athari Mbaya za Migogoro**

Athari mbaya za migogoro zinahusishwa na wala hazifungiwi tu kwa:

- a. Kupoteza maisha;
- b. Uharibifu wa mali;
- c. Kuwatishia watu huku wengine wakiachwa wale mavu;
- d. Kutengana kwa familia;
- e. Kuwepo kwa majanga ya kibinadamu kama vile njaa na kukosekana kwa chakula/utapiamlo;
- f. Kuenea kwa UKIMWI na kuwaweka watu katika hali ya kushikwa na magonjwa na maradhi kwa urahisi;
- g. Hupanda mbegu ya chuki miiongoni mwa watu waliokuwa na umoja; na

- h. Hujenga chuki na kutoaminiana huku watu wakijitahidi kuzoea au kutafuta njia mwafaka za kulipiza kisasi.

### **Marejeleo**

- Afigbo A.E., (1989) "Federal Character: Its Meaning and History", in P.P Ekeh and E. Osaghae, (eds), Federal Character and Federalism In Nigeria. Ibadan: Heinemann
- Anderson Benedict, (1991) Imagined Communities: Reflection On The Origin and Spread of Nationalism. Revised Edition London and New York: Verso
- Azar Edwards, (1990) The Management of Protracted Social Conflict: Theory and Cases. Dartmouth: Aldershot
- Brass P.R., (1991) Ethnicity and Nationalism: Theory and Comparison. London: Sage Publications
- Burton John, (1990) Conflict Resolution and Prevention. New York: St. Martin's Press
- Burton John, (1997) Violence Experienced: The Source of Conflict Violence and Crime and their Prevention. New York: Manchester University Press
- Horowitz Donald, (1985) Ethnic Groups in Conflict. Berkeley: University of California Press
- Lakes D. A. and Rothschild, Donald (1996) 'Containing Fear: The Origins and Management Of Ethnic Conflict,' International Security, vol. 21, no. 2:41-75
- Rothschild Donald, (1997) Managing Ethnic Conflict in Africa: Pressures and Incentives for Cooperation. Washington DC: Brookings Press
- Rupesinghe Kumar, (1987) 'Theories Of Conflict Resolution And Their Application To Protracted Ethnic Conflicts,' Bulletin Of Peace Proposals. Vol.18, no.4: 527-539
- Stavenhagen Rudolfo, (1990) The Ethnic Question. Tokyo: United Nations Press
- Vail Leroy, (1989) The Creation of Tribalism in Africa. London: James Currey

## SOMO LA 8: UTARATIBU WA MAPATANO NA MARIDHIANO KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washirika wanafaa kuwa na uwezo wa kutumia mafunzo waliyopata katika mapatano na maridhiano.

### UTANGULIZI

Somo hili linatoa fasiri ya dhana za mapatano na maridhiano. Linafafanua utaratibu wa mapatano na maridhiano huku likiorodhesha umuhimu na changamoto za utaratibu huo. Kadhalika, linaweka wazi mbinu za mapatano na maridhiano.

### MADA 1: SWALA LA MAPATANO NA MARIDHIANO

**Muda:** Dakika 15

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na Tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kutoa ufanuzi wa swala la mapatano na maridhiano.
- Washirika wanaeleza uelewa wao kuhusu dhana hizi.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa ufupi maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

### UFAFANUZI

### Upatanishi

Upatanishi unaweza kufafanuliwa kama utaratibu ama mkakati unaoimarisha afya ya kisaikolojia (mawazo) ya watu kutokana na mzozo.

## Maridhiano

Maridhiano, kwa upande mwengine, yanaweza kueleweka katika njia mbalimbali kama ifuatavyo:

- a. Ni harakati ambayo kwayo watu binafsi, jamii na mataifa husahaulia mbali utengano wa awali na kushirikiana (Apollos 2010);
- b. Huhusu uelewa wa pamoja wa mambo yaliyopita na hamu ya kuishi pamoja katika maisha ya amani na kuheshimiana;
- c. Ni harakati ambayo kwayo jamii hufufua uhusiano uliovunjika kutokana na mzozo;
- d. Kuridhiana ni mbinu ya kusuluuhisha mizozo ambayo lengo lake kuu siyo tu kurejesha uhusiano uliokuwepo kabla ya mzozo bali pia kutafuta njia ya kufikia mahusiano yenye amani.

## MADA 2: UTARATIBU WA MAPATANO NA MARIDHIANO

**Muda:** Dakika 15

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na Tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo, majadiliano, maigizo na mifano.

### SHUGHULI

- Mwelekezi kuwaongoza washiriki ili kutalii utaratibu wa mapatano na maridhiano.
- Washirika wanatalii utaratibu huo.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa ufupi maoni ya washirika.



### Vidokezo Muhimu

#### Utaratibu

Maridhiano yanajumuisha jitihada za kufufua uhusiano. Huwa ni machungu yaliyopita katika majadiliano pamoja na mambo ya wakati huu na kadhalika yatakayotokea baadaye.

Maridhiano ni harakati ya muda mrefu inayozingatia uaminifu na ukweli. Nguzo zifuatazo ni muhimu sana katika kuwepo kwa maridhiano.

- a. Mkosaji kukubali makosa yake;
- b. Kulipa fidia (kurejesha upya, kulipia hasara);
- c. Kuridhiana na wahasiriwa; na
- d. Ishara.

Maridhiano hayawezi kufanyika kutokea nje. Ni lazima yashughulikiwe na wale watu wanaotafuta maridhiano. Kimsingi, maridhiano ni jukumu la kila mmoja. Kila harakati ya kuridhiana huwa na upekee wake kwa kuwa utamaduni na muktadha uliosababisha kuwepo kwa mzozo ambao hutofautiana kila mara. Kwa hivyo, tathmini nzuri ya mzozo inahitajika ili kusanifu mbinu ya kuridhiana yenye sifa ya uthabiti, ukweli, haki na mapatano.

Uwiano unahusisha nguzo muhimu za kupata mtagusano, kama vile:

- Usalama wa umma;
- Haki na maridhiano;
- Uongozi na kushiriki; na
- Maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### **Hali zinazoweza Kuathiri Mafanikio ya Maridhiano**

- Matarajio ambayo hayakufikiwa – kukosa kuujua ukweli;
- Wachochazi kutokubali makosa yao;
- Kupuuza kwa baadhi ya aina fulani za ukiukaji ambazo wahasiriwa huzichukulia kwa umuhimu sana;
- Kukosa kutekeleza mapendekezo yaliyofanywa na tume zilizoundwa kuchunguza vyanzo vya mizozo. Mfano wa tume hizo ni kama tume ya Waki, tume ya Kriegler na tume ya Akiwumi mionganini mwa nyingine;
- Ukosefu wa kulipia fidia zilizotarajiwa;
- Kuzuka kwa mbinu mpya za ghasia; na
- Kukosa kutekeleza makubaliano ya Ajenda ya 4.



*Picha 8: Hali zinazoathiri ufanisi katika maridhiano*

### MADA3: MANUFAA NA CHANGAMOTO ZA MAPATANO NA MARIDHIANO

**Muda:** Dakika 30

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, vitia-alama, projekta (LCD) na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo, majadiliano na mifano.

#### SHUGHULI

- Mwelekezi kuwaongoza washiriki ili kutalii manufaa na changamoto za mapatano na maridhiano.
- Washirika wanajaribu kutafuta manufaa na changamoto.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa ufupi maoni ya washirika.



#### Vidokezo Muhimu

##### 1. Manufaa ya mapatano na maridhiano

- a. Uthabiti wa kisiasa/amani/umoja;
- b. Maendeleo ya kiuchumi na ustawi;
- c. Uthabiti wa kijamii na kitamaduni;
- d. Maendeleo ya kijamii; na
- e. Udhabiti wa kibinagsi.

##### 2. Changamoto za Mapatano na Maridhiano

- a. Uongozi na utawala mbaya;
- b. Ugavi wa rasilmali na nafasi za kimaisha usio sawa;
- c. Matatizo ya kisiasa;
- d. Ukabila;
- e. Ufisadi;

- f. Hofu inayotokana na ugatuzi;
- g. Usimamizi mbaya wa rasilimali za umma;
- h. Siasa za kimaeneo (jiopolitikia); na
- i. Mienendo mibaya ya vyombo vya habari.

### **Marejeleo**

Accord 4/2002.What makes Democracy work? Conflict Trends  
Centre for Conflict Resolution, (2000) Human Rights and Conflict  
Management Training Manual. Nakuru: Kenya  
Centre for Conflict Resolution, (2009) Post Conflict Violence-The Way  
Forward.  
Diallo Y., (1978) African Traditions and Humanitarian Laws. Geneva:  
ICRC  
Government of Kenya, (2008)The National Cohesion and Integration Act  
No. 12 of 2008. Nairobi: Government Printer  
Machira Apollos, (2009) Working for Peace. Nairobi: Aluka press  
Machira Apollos, (2010) The TJRC Process: A Hand Book. Nairobi: Aluka  
Publications  
Nakuru: Amu Press  
Osamba J., (1998) Political Conflicts in Kenya. Dakar, Senegal:  
CODESRIA Books  
Simon Dekha Ibrahim et al, (2008) Working with Conflict. Birmingham,  
UK

## SOMO LA 9: MFANO WA KUIGWA KATIKA UIMARISHAJI WA TAIFA LENYE UWIANO

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanafaa kuwa na uwezo wa kutambua mchango wa vielelezo katika uhakikishaji wa uwiano wa kitaifa.

### UTANGULIZI

Somo hili linafafanua maana halisi za mfano wa kuigwa na mabingwa wa uwiano. Kadhalika, somo linagusia majukumu ya mabingwa wa uwiano katika uimarishaji wa uwiano kwenye jamii.

### MADA 1: DHANA KAMILI YA MFANO WA KUIGWA NA MABINGWA WA UWIANO

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia-alama, projekta (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kutoa maana ya **dhana ya mfano wa kuigwa na sifa za mabingwa wa uwiano**.
- Washiriki wanajaribu kutoa maelezo ya neno.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa ufupi maono ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Maelezo

##### 1. Mifano ya Kuigwa

Mifano ya kuigwa ni watu wanaoweza kuigwa, kufuatwa au kutegemewa katika uongozi. Watu ambao ni mifano ya kuigwa hawana ubinafsi na huleta msukumo na hamasa ya ubora. Kwa upande mwagine, kuna watu wabaya ambao huzua 'athari

mbaya' kwa wenzao na hawastahili kuigwa. Mara nydingi wanarejelewa kama watu wabaya.

## 2. Mabingwa wa Uwiano

### Sifa za Mabingwa wa Uwiano

Mabingwa wa Uwiano huathiri mienendo, imani, na mahusiano katika ulimwengu wa tamaduni mseto. Raia hawa:

- a. Wanaelewa athari ya utamaduni kwa mienendo na imani zao, na mienendo na imani za watu wengine;
- b. Wanafahamu imani ya tamaduni fulani, thamani, na hisia zinazoweza kuathiri jinsi wao na wenzao wanavyowaza ama kuamini;
- c. Kutambua na kukubali uwingi wa imani, mionekano, na mitindo ya maisha;
- d. Anafahamu kuwa maarifa ya kihistoria huundwa, na hivyo hufinyangwa kutokana na uwezo wa kibinagsi, kisiasa na kijamii;
- e. Wana uwezo wa kuchukua mtazamo usiokuwa wa makundi ya juu wanapojuifunza kuhusu matukio ya kihistoria;
- f. Wanafahamu kuhusu matukio ya kihistoria ya mataifa mengine na kuelewa kwamba matukio haya yanaweza kuathiri mienendo, imani, na mahusiano na watu wengine;
- g. Wanafahamu mfanano baina ya makundi kutoka tamaduni tofauti na kukubali tofauti zilizopo kati yao;
- h. Wanaelewa hatari za mtazamo mbaya dhidi ya wengine pamoja na mapendeleo; wanajua na kuwa makini mno katika masuala ya ubaguzi wa rangi na unyanyapaa watu; na
- i. Wanaweza kuwasiliana, kushirikiana, na kufanya kazi na wenzao wanaotoka katika tamaduni nyingine.

## MADA 2: MANUFAA YA MABINGWA WA UWIANO KATIKA JAMII

**Muda:** Dakika 20

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu, kalamu za kutia alama, projekta (LCD) na Tarakilishi/Ngamizi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washirika ili kuorodhesha manufaa ya mabingwa wa uwiano kwenye jamii.
- Washiriki wanajaribu kutaja manufaa.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa muhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Manufaa ya Mabingwa wa Uwiano kwenye Jamii

- a. Ukuaji wa kibinafsi na kujifunza;
- b. Ongezeko la hadhi katika jamii;
- c. Ustawi wa maarifa ya kiuongozi;
- d. Mabadiliko ya utambulisho na mawazo chanya;
- e. Maarifa ya kibinafsi na kupungua kwa hofu ya tofauti za hoja zilizopo;
- f. Kujikubali;
- g. Ufahamu wa jinsi mambo yanayoathiri kila mtu yanavyoweza kuzidi nguvu tofauti hizo;
- h. Kila mtu kujisaidia alivyo na kuzidi kujiamini;
- i. Kujali masuala yanayohusiana na jinsia;
- j. Kutobagua wengine na kumaliza kasumba ya mapendeleo;
- k. Kufahamu na pia kuzuia vitendo vya ubaguzi katika jamii; na
- l. Kutumikia kama mfano wa kuigwa kwa wanajamii wengine.



Picha 9: Watu ambao ni Mifano ya Kuigwa ya Uwiano

### Marejeleo

- Bozeman B. and Feeney M. K., (2007) 'Toward a Useful Theory of Mentoring: A Conceptual Analysis and Critique'.  
Administration & Society Vol. 39 Issue no. 6 pages 719–739
- DuBois David L. and Michael J. Karcher, (2005) Handbook of Youth Mentoring. Thousand Oaks, California: SAGE Publications Ltd
- Parsloe E., Wray M. J., (2000) Coaching and Mentoring: Practical Methods to Improve Learning. Kogan Page

## SOMO LA 10: KUIWEZESHA JAMII KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanafaa kuwa na uwezo wa kutambua mbinu za uvezeshaji ili kuimarisha uwiano na utangamano.

### UTANGULIZI

Somo hili linakusudia kuwafahamisha washiriki kuhusu masuala mbali mbali yanayohusiana na uvezeshaji ili kuimarisha uwiano na utangamano wa kijamii.

### MADA 1: KUIWEZESHA JAMII

**Muda:** Dakika 15

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu, vitia-alama, projekta (LCD) na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kutoa maeleo ya neno uvezeshaji na uvezeshaji wa jamii.
- Washiriki wanajaribu kutoa maana ya maneno hayo.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa muhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

### Ufafanuzi wa Maneno

#### 1. Uvezeshaji

Uvezeshaji humaanisha utaratibu unaotumiwa na watu ili kuweza kuthibiti hali na maamuzi yanayobadilisha maisha yao. Ni utaratibu ambao watu huongeza wanachomiliki na sifa zao, hali inayowawezesha kufikia, kushirikiana, kuungana na/ama kuwa na usemi, ili kupata udhibiti zaidi. 'Uvezeshaji' hurejelea ongezeko la

uwezo wa kiroho, kisiasa, kijamii, au kiuchumi wa watu na jamii. Aghalabu huhusisha kuimariika kwa uwezo katika mazingira yao wenyewe.

## 2. Uwezeshaji wa Jamii

Uwezeshaji wa jamii unamaanisha utaratibu wa kuiwezesha jamii kuongeza udhibiti wa kuyaendesha maisha yao. Kwa hivyo, uwezeshaji wa jamii, ni zaidi ya kuhusishwa, kushirikishwa ama kuwekwa pamoja kwa jamii. Inaweza kuwa umiliki wa jamii na hatua zinazolenga mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Uwezeshaji wa jamii hulenga kukabili asasi za kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi zinazoambatanisha maslahi ya jamii kwa jumla, na kwa lengo la kuimariisha ushirikiano na sekta nyinginezo katika utafutaji wa suluhu.

## MADA 2: UTARATIBU NA WAJIBU WA KUIWEZESHA JAMII KUPATA UWIANO WA KITAIFA

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kutathmini utaratibu na wajibu wa kuiwezesha jamii.
- Washiriki wanajaribu kutathmini utaratibu wenyewe.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa muhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Utaratibu wa Kuiwezesha Jamii

Utaratibu wa kuiwezesha jamii husaidia watu/makundi ya watu kuiwezesha ama kuwezeshana ili kujipatia mamlaka, na uwezo wa kuathiri, na hivyo kutumia uwezo huo wanapotangamana na watu wengine, asasi na jamii nyingine. Uwezeshaji wa jamii huhimiza watu kujipatia maarifa na akili zinazowawezesha kukabiliana na vizuizi katika maisha yao au mazingira ya kikazi na hatimaye, kusaidia kujiimarisha wao wenyewe au hata jamii nzima.

Utaratibu wa Kuiwezesha Jamii unafaa kuwasaidia watu binafsi na makundi ya watu kuongezea: -

- a. Uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu hali zinazowazunguka/ama mazingira ya jumla;
- b. Uwezo wa kufikia habari na rasilmali kwa ajili ya kufanya maamuzi;
- c. Uwezo wa kuzingatia maamuzi mbalimbali ambayo kwayo unaweza kuchagua;
- d. Uwezo wa kuonyesha ushupavu katika ufanyaji maamuzi ya pamoja;

- e. Mawazo chanya kuhusu uwezo wa kufanya mabadiliko;
- f. Uwezo wa kujifunza na kufikia maarifa ya kujistawisha kibinafsi/ama kwa jumla;
- g. Uwezo wa kuathiri mitazamo ya watu wengine kupitia mabadilishano, elimu na utangamano;
- h. Kujihusisha na harakati ya ustawi usioisha ambao unaanzishwa na mtu binafsi;
- i. Sifa nzuri ya kibinafsi na ukiukaji wa unyanyapaa; na
- j. Uwezo wa kutofautisha kati ya yaliyo sahihi na yasiyo sahihi.

**Wajibu wa Kuiwezesha Jamii ili kupata Uwiano wa Kitaifa**

- a. Mashirika na usemi;
- b. Kushirikiana na kujihusisha;
- c. Mawasiliano shirikishi;
- d. Ukabilianaji wa matukio makuu yanayoweza kuzua migongano;
- e. Ukugazi na tathmini katika shughuli za uwiano wa kitaifa;
- f. Ujengaji wa dhana ya pamoja na mahusiano chanya; na
- g. Uundaji wa mipango ya shughuli za kijamii.

### MADA 3: AINA ZA UWEZESHAJI WA JAMII

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kutambua aina za uvezeshaji wa jamii.
- Washiriki wanajaribu kubaini aina za uvezeshaji.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa mukhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Aina za Uvezeshaji wa Jamii

##### 1. Uvezeshaji wa Kisiasa

Hali hii inamaanisha uhamasishaji wa wanajamii unaowawezesha kuchagua viongozi wenye maadili na ambao wanajali maslahi yao. Hii pia inajumuisha kuwaelimisha ili watupilie mbali mienendo ya kuwarejesha nyuma kama vile hulka ya kitu kidogo na aina nyinginezo za vishawishi ambavyo hufifisha ukaguzi wa viongozi bora. Jamii zinatafaa kuwajibika zinapovunjwa moyo na wanasiasa k.m. sheria ya kuwang'oa mamlakani.

##### 2. Uvezeshaji wa Umma

Hali hii inajumuisha uhamasishaji kuitia elimu ya umma ili kufahamisha jamii kuhusu haki zao na kuimarisha uwezo wao wa kuchukua hatua za kiraia zinazojumuisha ukaguzi wa kijamii na miradi ya hatua za kijamii mionganini mwa mambo mengine.

##### 3. Uvezeshaji wa Kiuchumi

Hali hii inamaanisha harakati ya kuimarisha uwezo wa watu binafsi na jamii kwa ajili ya kukusanya rasilimali zinazohitajika katika ufikiaji wa matazamio yao. Hii inaweza kufanyika kwa kuanzisha miradi ya kijamii kuleta mapato au kuwawezesha kufikia

mikopo na misaada mionganoni mwa nyingine. Watu wanapojikimu vyema kivyao, visa vyaa mizozo vinapungua na hivyo uwiano unaimarika.

#### **4. Uwezeshaji wa Kisheria**

Hali hii inamaanisha kuwafahamisha wanajamii ili kuelewa mfumo wa sheria na sera za kijiendeleza. Kadhalika, ina malengo ya kufanya mageuzi asasi za kisheria ili kulingana na matakwa ya kijamii. Kadhalika, inarejelea watu wote kuwa na uwezo wa kufikia haki ili kuhakikisha kuwa pana usalama wa kibinadamu unaopelekea kuwepo kwa nafasi bora za maendeleo ya binadamu.

#### **5. Uwezeshaji wa Kijamii**

Hali hii inamaanisha uimarishaji wa sekta mbalimbali za kijamii ili kuinua maslahi na masuala yao. Sekta hizi zinaweza kuhusisha wanawake, vijana, walemvu, watu wakongwe, wanamazingira, wakereketwa wa kijinsia, na mashirika ya jamii kwa jumla yanayopigia darubini utendakazi wa Serikali na hata sekta ya kibinafsi.

#### **6. Uwezeshaji wa Kitamaduni**

Hali hii inamaanisha uhamasishaji kati ya wanajamii kuhusu athari ya mienendo yao ya kitamaduni kwa jamii nzima. Uwezeshaji wa kitamaduni hupigania udumishaji wa mienendo ya kitamaduni ambayo inaweza kuleta maendeleo ya jamii na kutupilia mbali ile mienendo ambayo inazuia maendeleo ya jamii kama vile wizi wa mifugo, ukeketaji wa wanawake, na uharibifu wa mazingira na wanyamapori mionganoni mwa mambo mengine.

#### **7. Uwezeshaji wa Kidini**

Hali hii inamaanisha kuifahamisha jamii ili ielewe imani yao na kutambua na kuvumilia mifumo ya imani ya wenzao. Uwezeshaji wa kidini hupinga misimamo mikali ya kidini na hukumbatia majadiliano ya kidini na usuluhishaji wa tofauti katika jamii.

## MADA 4: UMUHIMU WA UWEZESHAJI

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo, majadiliano na kazi ya makundi.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kuchungua **umuhimu wa uwezeshaji** wa jamii.
- Washiriki wanajaribu kuchanganua umuhimu huu.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa mukhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Umuhimu wa Uwezeshaji

- a. Huimarisha ubora wa maisha ya wenyiji;
- b. Huwezesha uwajibikaji na uwazi;
- c. Huongeza ushirikishwaji wa waliotelekezwa na makundi ambayo hayakubahatika kwenye jamii;
- d. Huwezesha ushiriki bora katika uongozi wa jamii; na
- e. Huwezesha kufikia rasilmali na ustawi wa kiuchumi katika jamii.

## MADA 5: MIKAKATI ENDELEVU YA KUIWEZESHA JAMII

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu, vitia-alama, projekta ya LCD na tarakilishi.

**Mbinu:** Chemsha bongo, majadiliano na kazi ya makundi.

### SHUGHULI

- Mwelekezi anawaongoza washiriki ili kufahamu **mikakati endelevu** ya kuiwezesha jamii kuimarisha uwiano na utangamano wa kitaifa.
- Washiriki wanajaribu kufahamu mikakati hii.
- Mwelekezi anatumia vidokezo muhimu ili kunakili kwa mukhtasari maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### **Mikakati Endelevu ya Kuiwezesha Jamii katika Kuimarisha Uwiano na Utangamano wa Kitaifa**

- a. Miradi ya kijamii;
- b. Uimarishaji na udumishaji wa haki za kibinadamu;
- c. Ugavi sawa wa rasilimali;
- d. Elimu ya umma ili kuuhamasisha kuhusu masuala yanayoimarisha maslahi k.m sheria ya haki za kimsingi;
- e. Ushirikishaji na ushiriki katika uundaji sera, utawala na utoaji huduma;
- f. Utekelezaji wa mipango ya kubadilishana elimu baina ya wanajamii na shughuli za michezo;
- g. Uimarishaji wa Rajua ya Kenya ya 2030;
- h. Utekelezaji wa Katiba ya Kenya, 2010;
- i. Kuwafunza wafundishaji kuhusu masuala ya uwiano na utangamano wa kitaifa; na

- j. Kusaidia asasi za kijamii kama vile baraza la wazee na kamati za amani.

### **Marejleo**

Blanchard Kenneth H., John P. Carlos, and Alan Randolph, (1996)

Empowerment Takes More Than a Minute. San Francisco:

Berrett-Koehler

Stewart Aileen Mitchell, (1994) Empowering People Pitman, London:

Financial Times Management

Thomas K. W. and Velthouse B. A., (1990) 'Cognitive Elements of

Empowerment: An 'Interpretive' Model of Intrinsic Task

Motivation,' Academy of Management Review, Vol 15, No. 4,

pp. 666-681

Wilkinson A., (1998) Empowerment: Theory and Practice. Personnel

Review Vol. 27, No. 1, pp. 40-56

## SOMO 11: USAWA NA UHUSISHWAJI KWA AJILI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanatarajiwa kuthamini jukumu la usawa na uhusishwaji kwa ajili ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

### UTANGULIZI

Somo hili linatoa maelezo kuhusu usawa na uhusishwaji kama njia ya kukuza uwiano na utangamano wa kitaifa. Pia, linaangazia asili na aina za kutengwa pamoja na njia za kukuza usawa na uhusishwaji. Linamalizia kwa kuchunguza manufaa ya usawa na uhusishwaji kwa ajili ya kukuza uwiano na utangamano wa kitaifa.

### MADA 1: USAWA NA UHUSISHWAJI

**Muda:** Dakika 15.

**Vitendea-kazi:** Ramani ya Kenya, picha, chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala ya sera inayohusu uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi awaongoze washiriki kutoa maana ya **usawa, uhusishwaji na maneno mengine husika**.
- Washiriki wajaribu kutoa maana za maneno hayo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kutoa muhtasari wa maoni ya washiriki.



**Vidokezo Muhimu.**

**Maana za Maneno:**

#### 1. Usawa

Usawa unamaanisha udhihirishaji wa haki za kijamii. Kimsingi, usawa unahusu ugavi wa rasilmali kwa njia ya haki. Usawa ni zaidi ya usawa katika kupata kitu. Usawa

unahitaji matokeo ambayo yanalingana na mahitaji ya mtu binafsi yakilinganishwa na mahitaji ya watu wengine.

## **2. Uhushwaji**

Uhushwaji ni tendo au hali ya kuwa sehemu ya kundi, muundo au mfumo fulani. Mfumo wa uhushwaji unalenga kila mtu na huwafanya watu kuhisi kuwa wanathaminiwa. Hii ni muhimu katika ufanisi wa kundi, shirika, jamii au nchi.

## **3. Utengwaji**

Utengwaji huhusu taratibu za kimakusudi ambapo watu au jamii nzima wanazuiliwa kupata haki, nafasi au rasilmali (kama makao, kazi, huduma za afya, kuhushwaji kiraia, kushiriki kidemokrasia na mengineyo) ambazo zinapatikana kwa matumizi ya wanajamii na ambazo ni muhimu katika kuleta utangamano wa jamii. Pia, utengwaji unaweza kuelezwa kama utaratibu wa mitazamo anuai ya kuendeleza usambaratikaji wa jamii, kutenga makundi na watu binafsi katika kuhusiana kijamii au kitaasisi, na kuwazuia kushiriki kikamilifu katika matendo ya kawaida kwenye jamii wanamoishi.

## **4. Utelekezwaji**

Utelekezwaji ni utaratibu ambao sehemu ya jamii haihusishwi au kujumuishwa katika maswala ya kijamii, kisiasa au kiuchumi ya jamii pana, kutokana na idadi yake au tofauti za kimazingira na mambo mengine. **Ibara 260 na 27(4)** ya Katiba ya Kenya-2010 inaeleza utekelezwaji kama:

**“kundi lilitotekelezwa”** ambalo ni kundi la watu ambao, kutokana na sheria au desturi za awali, wakati huo au baada ya tarehe ya utekelezaji, walidhulumiwa au wanadhulumiwa kutokana na kubaguliwa kwa namna moja au zaidi zilizoko katika Ibara ya 27(4). Kwa upande mwingine, Ibara ya 27(4) inaeleza kuwa nchi haitabagua mtu yeyote kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kwa msingi wowote ule kama vile mbari, jinsia, ujauzito, hali ya ndoa, hali ya afya, kabilia au jamii, rangi, umri, ulemavu, dini, dhamiri, imani, mila, mavazi, lugha au uzazi.

## **5. Maamuzi ya dhati**

Hii inarejelea hatua za kimakusudi za sera ambazo zinazingatia vipengele kama “mbari, rangi, dini, jinsia, mapendeleo ya kimapenzi au chanzo cha taifa la mtu” ili kunufaisha kundi tengwa, hasa kama njia ya kukabili athari za ubaguzi unaotokana na historia. Hatua kama hizo hunuia kusawazisha mambo.

## **6. Nafasi sawa**

Hii ni kanuni ya kutobagua, ambayo hutilia mkazo kuwa nafasi za elimu, kazi, ugavi wa rasilmali na maeneo mengine, zastahili kuwekwa wazi kwa wananchi wote, bila

kujali umri, mbari, jinsia, dini, mahusiano ya siasa, kabilia, au sifa zozote za kibinafsi au za kikundi ambazo hazihusiani na uwezo, utendakazi au uhitimu wa mtu.

## 7. Uhusishwaji wa kijamii

Hii ni dhana yenyewe mitazamo anuai ambayo huwezesha watu kuwa wabunifu na kuimarisha malengo ya kitaifa kutokana na yale wanayopinga au yale wanayochagua. Huwezesha watu kukuza ubunifu na kuwa na malengo ya kitaifa ambayo yataendeleza sera kuhusu masuala mbali mbali ili kufanikisha matokeo.

## 8. Utengwaji wa kijamii

Huu ni utaratibu wa mitazamo anuai inayoendeleza usambaratikaji wa jamii, kutenga makundi ya watu na watu binafsi katika mahusiano ya kijamii na asasi za kijamiii, na kuwazuia kushiriki kikamilifu katika shughuli za kawaida katika jamii wanamoishi. Utaratibu huu pia unahusiana na kutenga au kunyima watu fulani haki ya kupiga kura. Mara nyingi hahuhsiana na tabaka la mtu, hali yake ya elimu, uhusiano wake alipokuwa mtoto, hali ya maisha yake, na jinsi haya yote yanavyowenza kumwathiri kupata nafasi mbali mbali. Huhusisha pia walemavu, makundi tengwa (wake kwa waume) na watu wenye mielekeo tofauti ya kimapenzi na kijinsia.



*Picha 10: Jamii inayozingatia uhusishwaji.*

## MADA 2: VISABABISHI NA AINA ZA UTENGWAJI NA UTELEKEZWAJI

**Muda:** Dakika 40.

**Vitendea-kazi:** Ramani ya Kenya, picha, chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, nakala za katiba na nakala ya sera za uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kutambua sababu na aina za utengwaji na utekelezwaji.
- Washiriki wajaribu kutoa sababu na aina za utengwaji na utekelezwaji.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kutoa muhtasari wa maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

**Sababu za utengwaji na ukosefu wa usawa.**

#### 1. Kutengwa kimpango

Hii inarejelea kunyimwa kimpango haki za rasilmali na huduma. Pia, kunyimwa haki ya kushiriki, kwa namna iliyo sawa katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kimila, au kisia. Taratibu za kutengwa zinaweza kutokea katika ngazi tofauti tofauti – katika au mionganini mwa familia, vijijini, mijini na katika kaunti.

##### a. Hali za kihistoria

Katika muktadha wa nchi ya Kenya, hali za kihistoria ambazo zinachangia utengwaji kimpango ni kama zile athari za kujengwa kwa reli na serikali ya kikoloni na kuwepo kwa maeneo yaliyohifadhiwa walowezi wa kizungu pekee.

##### b. Kubaguliwa na Mashirika ya Nchi

Usawa ni muhimu katika demokrasia. Ili kuwe na jamii yenyewe uwiano, watu binafsi na jamii mbalimbali huhitaji kuhisi kuwa wanawea kushiriki kikamilifu katika ukuaji na maendeleo ya jamii na pia watendewe mambo kwa usawa bila ubaguzi. Serikali

inastahili kisheria na kimaadili kutoa huduma kwa watu bila kuzingatia jinsia, kabilia, umri, ulemavu, mapendeleo ya kimapenzi, dini au imani za kimila.

### c. **Ukosefu wa sera na sheria**

Serikali ikikosa kutambua na kutunga sheria na sera za kuendeleza usawa na kushughulikia aina yoyote ya ubaguzi na utekelezwaji utakaozaa hali ya kutokuwa sawa katika jamii, huzidisha pia utengwaji wa kimpango.

## **2. Hali za kimienendo.**

### a. **Kutokubalika kitaasisi au kiraia**

Kuna mielekeo na desturi fulani za kijamii ambazo husababisha hali ya kutengwa. Haya yanaweza kuwa ya kufahamika au kukosa kufahamika, ya kimakusudi au bila makusudi, ya wazi au yasiyo ya wazi. Kutokubalika kitaasisi au kiraia humaanisha kuwepo kwa "maadili, imani, matambiko na taratibu za kitaasisi ambazo hujiendeleza kimpango na kikawaida kwa manufaa ya watu na makundi fulani tu bila kujali wengine."

### b. **Uongozi mbaya**

Uongozi mbaya ni namna ambayo "viongozi hutumia rasilmali na nafasi kwa manufaa ya wachache wanaofikiria kuwa wanastahili". Hii huhusisha kubinafsisha nafasi fulani kwa misingi ya sifa za kundi kama vile mbari, lugha, asili ya jamii na dini. Taasisi za nchi husababisha utengwaji zinapobagua kimakusudi katika sheria , sera au mipango yao.

### c. **Utengwaji wa kijamii**

Utengwaji wa kijamii huhusiana na kutenga au kunyima watu katika jamii fulani haki ya kupiga kura. Mara nydingi inahusiana na tabaka, hali ya elimu na hali ya maisha, na jinsi haya yote yanavyoweza kuathiri upatikanaji wa nafasi mbali mbali. Yeyote anayekiuka kwa njia yoyote kaida za jamii anaweza kujipata katika hali ya kutengwa na jamii. Vile vile, jamii zinaweza kujitenga kwa kujitoa kihalisi kutoka katika kundi kubwa la kijamii.

### d. **Utengwaji wa kitamaduni**

Kuhakikisha kuwa watu wote wanashiriki katika shughuli za kitamaduni ni njia muhimu ya kuendeleza jamii iliyo jumuishi. Kushiriki katika shughuli za kitamaduni kunaweza kuwa muhimu katika kusaidia watu na jamii kwa ujumla kuukabili umaskini na utengwaji wa kijamii. Mfano mzuri ni ule wa vijana kushiriki katika michezo ya kuigiza na warsha mbalimbali. Kukabili tofauti za kitamaduni na ubaguzi kunaweza kuendelezwa kuititia kwa madarasa ya lugha au matumizi ya uigizaji na ngoma shulenii ili kusherehekea tamaduni mbalimbali.

## AINA ZA UTENGWAJI

Aina za utengwaji ambazo huathiri watu binafsi na makundi zinaweza kugawanywa kama ifuatavyo:

- a. Kutengwa katika bidhaa na huduma, zikiwemo bidhaa halisi na huduma kama vile elimu na matibabu;
- b. Kutengwa katika ajira kama vile kutoajiriwa, kuajiri watu wachache na kuajiriwa kazi zisizo imara na zenye malipo duni;
- c. Kutengwa katika ardhi, hali inayobainika kupitia ukosefu wa makao, nyumba, madai ya ardhi isiyomilikiwa na pia uskwota;
- d. Kutengwa katika usalama kama vile usalama wa watu na mali;
- e. Kutengwa katika utekelezaji wa haki za binadamu kama vile ubaguzi na kutokubalika katika mila za jamii kubwa;
- f. Kutengwa katika mikakati ya kuendeleza uchumi ambayo inaweza kuleta matokeo mabaya ya soko na uundaji upya wa sera. Katika nchi zinazoendelea, haya huweza kuyahusisha pia athari za marekebisho ya sera za kiuchumi; na
- g. Kutengwa katika kushiriki kwenye siasa na uundaji wa maamuzi.

### MADA 3: HATUA ZA KUENDELEZA USAWA NA UHUSISHWAJI

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Ramani ya Kenya, picha, chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, nakala za katiba na nakala ya sera za utangamano na uwiano wa kitaifa.

**Chemsha bongo:** Kushirikishana.

#### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze wahusika kutaja hatua za kuendeleza usawa na uhusishwaji.
- Wahusika wajaribu kutaja hatua hizo.
- Mwelekezi atumie hoja Kuu kuelezea maoni ya wahusika.



#### Vidokezo Muhimu

##### Hatua za Kuendeleza Usawa na Uhushishwaji

Hatua hizi ni kama:

- a. Maamuzi ya dhati – kubuni sera na mipango ambayo itawapa nafasi watu na vikundi vilivytengwa, kushiriki kikamilifu katika masuala husika kama vile alama za kuhitimu katika chuo kikuu zipunguzwe kwa wanawake na kwa makundi tengwa;
- b. Sheria – kutunga sheria ambazo zitajali masilahi ya watu na makundi tengwa;
- c. Kuhamasisha umma – kufahamisha umma kuhusu asili, athari na changamoto zinazohusu utelekezwaji;
- d. Usawa katika usambazaji wa rasilmali na nafasi kama vile hazina ya usawazishaji;
- e. Kutupilia mbali tamaduni duni kama vile umorani, ukeketaji wa wanawake, wizi wa mifugo , na kutafuta njia badala za maswala hayo; na
- f. Kutekeleza Katiba.

## MADA 4: MANUFAA YA USAWA NA UHUSISHWAJI

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Ramani ya Kenya, picha, chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala ya sera ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kutaja **manufaa ya usawa** na uhusishwaji.
- Washiriki wajaribu kutaja manufaa hayo.
- Mwelekezi atumie hoja Kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu.

#### Manufaa ya Usawa na Uhushishwaji ni kama:

- a. Kuimashwa kwa umoja wa kitaifa;
- b. Kuongezeka kwa utangamano wa kijamii na kiuchumi;
- c. Jamii na makundi yaliyotelekezwa kupata nafasi ya kuonyesha uwezo na vipawa vyao;
- d. Kuimashwa kwa maendeleo ya kitaifa;
- e. Watu waliohamasishwa
- f. Kuwezesha kwa jamii zilizotelekezwa na makundi mengine;
- g. Kuimarika kisiasa na kiuchumi;
- h. Kuendeleza uzalendo; na
- i. Uwazi na hadhi ya binadamu.



Picha 11: watu waliohamasishwa

**Marejeleo**

Centre for Research into Socially Inclusive Services – [www.crisis.hw.ac.uk](http://www.crisis.hw.ac.uk)

Joseph Rowntree Foundation – [www.irf.org.uk](http://www.irf.org.uk)

Oxfam (UK Poverty Programme) – [www.oxfamgb.org](http://www.oxfamgb.org)

Poverty Alliance – [www.povertyalliance.org](http://www.povertyalliance.org)

Regeneration Portal – [www.renewal.net](http://www.renewal.net)

Scottish Executive website –[www.scotland.gov.uk](http://www.scotland.gov.uk)

Social Exclusion Network – [www.socialexclusionunit.gov.uk](http://www.socialexclusionunit.gov.uk)

Social Justice site: [http://www.dmuuc.org/about/racial\\_timeline.html](http://www.dmuuc.org/about/racial_timeline.html)

## SOMO 12: UDHIBITI WA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanahitaji kuelewa umuhimu wa udhibiti wa uanuai wa kikabila na kitamaduni katika kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa.

### Utangulizi.

Somo hili linatoa habari muhimu kuhusu usawa na uhusishwaji. Linaangazia uhusiano uliopo kati ya usawa na uhusishwaji, pamoja na uwiano na utangamano wa kitaifa. Pia, somo hili linachunguza changamoto zilizopo katika kudhibiti uanuai wa kikabila na kitamaduni, pamoja na mikakati ya kuendeleza uanuai wa kikabila na kitamaduni. Somo linamalizia kwa kufafanua umuhimu wa kuwa na uanuai wa kikabila na kitamaduni.

## MADA 1: MAANA YA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI

**Muda :** Dakika 30.

**Vitendea-kazi :** Ramani ya Kenya, picha, chati, kalamu za wino, nakala za Katiba na nakala ya sera ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

- Mwelekezi aongoze washiriki kutoa maana ya ukabila na maneno mengine husika.
- Washiriki wajaribu kutoa maana za maneno hayo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo muhimu

**Maana za maneno :**

#### 1. Ukabila

Hii ni hali wazi au fiche ya kudhihirisha umoja, kujitolea, na kuunga mkono mawazo, maadili, kanuni na desturi za kundi la kinasaba. Pia inaweza kumaanisha hali ya kuwa na mshikamano wa kisiasa, kijamii au kiuchumi ambao hutumikia masuala ya kundi la kinasaba. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa kuna ukabila hasi na chanya. Ukabila chanya huendeleza majadiliano na mahusiano kati ya vikundi nao ukabila hasi hupuza maswala haya.

## 2. Kundu la Kikabila.

Kundi la kikabila huwa na watu ambao wanahusiana kinasaba na wenyе historia sawa, utamaduni sawa, lugha, matarajio na maono sawa. Katika baadhi ya sehemu za ulimwengu, makundi ya kikabila huishi katika maeneo fulani ya kijiografia, ilhali katika nchi nyingine, hujitambulisha kama watu wamoja.

## 3. Uanuai wa Kikabila

Uanuai wa kikabila ni hali ambayo makabila mengi huishi pamoja katika sehemu au eneo moja la kijiografia; Uanuai wa kikabila humaanisha kuwa makundi huwa na sifa za kipekee ambazo zinastahili kuheshimiwa; pia, inamaanisha kuwa hakuna kundi moja ambalo linajaribu kumeza lingine au kulilazimishia mapendeleo yake.

Uanuai wa kikabila usiwe kizuizi kwa amani ya taifa. Tom Mboya alisema kuwa: 'sisi ni wazawa wa makabila tofauti na hatuwezi kubadilika, lakini nakataa kuamini kuwa kwa sababu tuna asili tofauti kutokana na makabila, mila na tamaduni zetu, hatuwezi kujenga jumuiya au taifa moja la Kiafrika."

Wasomi wameeleza kuwa ukabila umetumiwa na viongozi wa kikabila kama mbinu ya kupata na kuhifadhi mamlaka, sawa na vile utamaduni unaweza kutumiwa kuwabagua watu wengine ambao si wa kundi hilo la kabilia au utamaduni.

## 4. Utamaduni

Huu ni mseto wa sifa maalum za kidini, kimali, kimawazo, na kihisia ambazo ni za kijamii au kundi la kijamii. Mbali na sanaa na fasihi, utamaduni unahu su pia mienendo ya maisha, mbinu za utangamano, mfumo wa kimaadili, desturi na imani. Kuheshimu na kutunza utamaduni ni mojawapo ya majukumu ya haki za kibinadamu. Utamaduni pia umeelezwa kama utaratibu wa mienendo, maadili, mawazo, na matendo yanayoshirikisha kundi la kijamii. Mambo ambayo hutofautisha kundi moja la watu na jingine katika jamii za kisasa ni maadili, ishara, tafsiri na mielekeo.

Kadhalika, utamaduni ni mwenendo ambao binadamu hujifunza kwa kuwa unahu su mseto wa mienendo, mitindo na sifa ambazo binadamu amejifunza. Hupatikana katika jamii kuititia mafundisho ya jamii hiyo. Huhusisha vielelezo vya kiishara, kidhana na kihisia. Huhusisha pia vitu vya kitamaduni kama vile chakula, mavazi, n.k. Utamaduni unahu ishara ushirika wa pamoja na hupitishwa na jamii. Huendelezwa na kuhifadhiwa kulingana na vile washiriki wa kundi hufasiri, kutumia na kutambua ishara za kitamaduni. Kwa mfano, kila mtoto hupitishwa katika mafunzo ya kitamaduni wakati anapokua.

## 5. Uanuai wa kitamaduni

Uanuai wa kitamaduni humaanisha kuheshimu haki za kimsingi kama vile uhuru wa mawazo, dhamiri na dini, uhuru wa maoni na kujieleza, na uhuru wa kushiriki katika harakati za kitamaduni kulingana na uchaguzi wa mtu binafsi.

### Mifano ya Uanuai wa Kikabila na Kitamaduni Nchini Kenya :

- a. **Mavazi** : Aina za mavazi zinaweza kutumika kutambulisha tamaduni mbalimbali kama vile vazi la Wamasai, buibui, leso, kanga na kondo.
- b. **Lugha** : Huu ndio utambulisho wa kitamaduni/kikabila unaojulikana sana katika kutambulisha jamii sana ya kubainisha jamii kwa mfano, Dholuo, Kimeru, Kitaita, Kiswahili, Kiteso, nk.
- c. **Majina** : Majina mengine hutambulisha makundi ya kikabila na badala ya kufurahikiwa, huweza kuwa sababu ya ubaguzi mf. Kamau, Atieno, Mohamed, Kipchoge, Farah, Amina, Nanjala, Wakesho, Etyang, Olesunkulu.
- d. **Chakula** : *Mukimo, firigisi, samaki, wali, mursik (maziwa), muthokoi*.
- e. **Nyimbo na ngoma** : *Isukuti, ramogi, akisuk, ohangla, taarab, esagasaga, mugithi, nyatiti, kilumi, sengenya*.
- f. **Nyumba** : *Manyata, Simba, digingira*.
- g. **Michezo** : Mapigano ya fahali, mapigano ya jogoo, ajwa, bao, miereka, kulenga shabaha, mchezo wa biladi (sherehe za maulidi).



Picha 11: Uanuai wa kitamaduni mionganini mwa jamii za Kenya

## MADA 2 : CHANGAMOTO KATIKA KUDHIBITI UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI.

**Muda :** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Ramani ya Kenya, picha, chati, kalamu za wino, nakala za Katiba na nakala ya sera za uwiano utangamano wa kitaifa.

**Mbinu :** Chemsha bongo, majadiliano ya vikundi.

### SHUGHULI :

- Mwelekezi aongoze washiriki kutaja changamoto katika kudhibiti uanuai wa kikabila na kitamaduni.
- Washiriki wajaribu kutaja changamoto hizo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo muhimu

#### Changamoto katika kudhibiti uanuai wa kikabila na kitamaduni.

Uanuai unaweza kuzua tataruki kati ya makundi mbali mbali – umri, jinsia, tabaka, n.k. Unaweza kupunguza ufanisi wa mawasiliano na kuzidisha mizozo nchini kutohana na tofauti za kikabila au kitamaduni. Uanuai unaweza kupunguza mshikamano na umoja kati ya wananchi wa taifa ikiwa hautatumiwa vizuri. Unaweza kusababisha usaliti wa maadili ya taifa na wananchi wasioridhika. Athari zinazohusiana na uanuai kama vile tatizo la kujitambua na ubaguzi, huweza kuzidisha tataruki katika makundi.

#### Changamoto katika uanuai wa kitamaduni na kikabila.

- a. Dharau;
- b. Ubaguzi;
- c. Dhana potovu;
- d. Mapendeleo;
- e. Mawazo ya kikabila;
- f. Kuelewa vibaya;
- g. Utelekelezaji;
- h. Misimamo mikali ya kidini;
- i. Misimimo mikali ya kitamaduni; na
- j. Utengwaji.

### MADA 3 : MIKAKATI YA KUENDELEZA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI

**Muda :** Dakika 30.

**Vitendea-kazi :** Ramani ya Kenya, picha, chati, kalamu za wino, nakala za Katiba na nakala ya sera za uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Majadiliano ya vikundi.

#### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kutaja mikakati ya kuendeleza uanuai wa kikabila na kitamaduni.
- Washiriki wajaribu kutaja mikakati hiyo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



#### Vidokezo muhimu

##### Mikakati ya kuendeleza uanuai wa kikabila na kitamaduni

- a. Kuiwezesha jamii;
- b. Mafunzo anuai na miradi ya uhamasishaji;
- c. Kujihusisha katika mipango ya kushirikiana na Mipango ya jamii mbali mbali kutembeleana;
- d. Ushauri;
- e. Kuhimiza ustahimilivu;
- f. Sherehe za kitamaduni kati ya pamoja za kitamaduni k.m. sherehe za muziki, kesha za jamii mbalimbali, kesha za kitamaduni k.m. *esagasaga, ramogi, mulembe, taarabu, sengenya, mugithi, kililimbi*;
- g. Kufanya maigizo ya pamoja ya kitamaduni wakati wa siku za kitaifa;
- h. Ndoa kati ya makabila;
- i. Kujenga vituo vya kitamaduni katika maeneo mbalimbali;
- j. Kuhimiza masomo ya uanuai wa kitamaduni shulen;
- k. Kuimarisha mazungumzo kati ya makabila;
- l. Kuhimiza mazungumzo ya dini mbalimbali;
- m. Kuwa na mazungumzo mionganoni mwa viongozi wa kidini;
- n. Kutambua mashujaa wa kitaifa kama vile Tom Mboya, Prof. Wangari Maathai, Dedan Kimathi, Kipchoge Keino, Mekatilili wa Menza, Mwang’acha Mwachof, Masinde Muliro, Dekha Ibrahim Abdi na kadhalika; na
- o. Kuunga mkono mifumo ya kitamaduni ambayo huendeleza uwiano wa kitaifa kama vile mabaraza ya wazee, *Njuri ncheke*, Viongozi wa Kaya, baraza la wazee la Wakikuyu, Waluo, Wakalenjin mionganoni mwa wengine.

## MADA 4 : UMUHIMU WA UANUAI WA KIKABILA NA KITAMADUNI

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Ramani ya Kenya, picha, chati za kugeuza, kalamu za wino, nakala za Katiba na nakala ya sera za uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Majadiliano ya vikundi.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kuchunguza umuhimu wa uanuai wa kikabila na kitamaduni.
- Washiriki wajaribu kuchunguza umuhimu wa uanuai wa kikabila na kitamaduni.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo muhimu

#### Umuhimu wa Utamaduni

Utamaduni ni muhimu katika maendeleo ya mtu binafsi na ya mahusiano ya kijamii. Tunategemea utamaduni kwa maana hatukuzaliwa na habari tunazohitaji ili kuishi. Hatufahamu jinsi ya kujivalisha, kujitunza, kula chakula, tuabudu Mungu gani au jinsi ya kutengeneza na kutumia pesa.

Ni sharti tujifunze utamaduni wetu kuititia maingiliano, kutazama na kuiga ili tushiriki kama wanachama wa kundi fulani. Kama vile utamaduni ni muhimu katika maendeleo ya watu, ni muhimu pia katika maendeleo ya jamii. Mfumo fulani wa kutunga na kutekeleza sheria ni muhimu katika jamii zote. Ili kuweza kuishi, jamii zinahitaji sheria kuhusu uraia na uvumilivu kwa wengine. Hatukuzaliwa na ujuzi wa kuonyesha wema au chuki kwa wengine.

#### Umuhimu wa Utamaduni katika Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.

1. Utamaduni huunda mazingira ya maingiliano ya jamii ya wanadamu, na hivyo basi kujenga mienendo ya watu ambayo inaweza kuleta amani au mafarakano.
2. Utamaduni ni mojawapo wa taratibu za kimaendeleo zilizotajwa katika dhana ya shirika la UNDP ya "kuzidisha uchaguzi wa watu binafsi". Kwa mtazamo huu,

utamaduni sio tu namna ya maisha ya watu katika kipindi fulani, lakini pia ni mbinu muhimu ya maendeleo endelevu.

3. Utamaduni kama mfumo, ndio unaojenga ukabila ambao umesalia kuwa changamoto katika uwiano wa kitaifa.

### **Umuhimu wa kuendeleza Uanuai wa Kitamaduni ili kudhibiti Uwiano wa Kitaifa**

Jamii ambazo zinaheshimu na kuthamini uanuai wa kitamaduni hupata manufaa yafuatayo:

- a. Mizozo hupungua na mahusiano huboreshwa;
- b. Kuboreka kwa utendaji na matokeo mema katika asasi na sehemu nyingine za jamii;
- c. Mbinu bora za kusuluuhisha matatizo kati ya jamii;
- d. Kuongezeka kwa nafasi za kibiashara ambazo hazipatikani katika biashara zinazoongozwa na kundi mahsusil la kitamaduni;
- e. Kuimarika kwa maingiliano na mabadilishano ya mawazo; na
- f. Kuimarika kwa uchumi.

### **Marejeleo**

Amutabi M.N., (1995) 'Challenging the Orthodoxies: The role of Ethnicity and Regional Nationalism in Leadership and Democracy in Africa,' Conference Paper, UNESCO Conference, Kericho, 28-31 May 1995.

Hall Stuart, (1996) 'Ethnicity: Identity and Difference' in Geoff Eley and Ronald Grigor Suny (eds) *Becoming National. A Reader.* Oxford, New York: Oxford University Press pp. 339-49.

KHRC, (1998) *Killing the Vote: State Sponsored Violence and Flawed Election in Kenya.* Nairobi: Kenya Human Rights Commission

Mafeje A., (1971). 'The Ideology of Tribalism,' *Journal of Modern Africa Studies*

Mamdani M. et al, (1988) 'Social Movements, Social Transformation and the Struggle for Democracy in Africa,' CODESRIA Working Paper

Manyasa Emmanuel Okoth, (2005) 'Ethnicity: An Opportunity or a Bane

in Africa's Development,' in Felicia Arudo Yieke (ed), East Africa: In Search of National and Regional Renewal. Dakar, Senegal: CODESRIA Publications pp. 67-79

Mazrui Ali, (1994) 'Development in a Multi-cultural Context: Trends and Tensions,' in Serageldin and June Taboroff (eds), Culture and Development. Washington DC: World Bank. pp. 127-136

Ndegwa Stephen, (1997) 'Citizenship and Ethnicity: An Examination of Two Transition Moments in Kenyan politics,' American Political Science Review Vol. 91 Issue no. 3

Nyong'o Anyang' P., (1993) The Challenge of National Leadership and Democratic Change in Kenya. Nairobi: Shrikan Publishers

Ochieng William, 'Independent Kenya (1963 – 1986)' in W. R. Ochieng (ed), A Modern History of Kenya 1895 -1980. Nairobi: Evans Brothers pp. 202 -218.

Ogot Bethuel (ed), (1996) Ethnicity, Nationalism and Democracy in Africa. Maseno, Kenya: Instituteof Researchand Postgraduate Studies, Maseno University College

Oyugi W.O and A. Gitonga (eds), (1987) Democratic Theory and Practice in Africa, Nairobi: Heinemann. pp. 49-70

Simala Inyani Kenneth, (1996) 'Ethnolinguistic Nationalism and Identity in Africa: Its Evolution and Implications to Nation-States,' in Bethwuel Ogot (ed), Ethnicity, Nationalism and Democracy in Africa. Kisumu: Institute of Research and Postgraduate Studies, Maseno University

## SOMO 13: NAFASI YA MAADILI NA KANUNI ZA UTAWALA KATIKA UWIANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanahitaji kufahamu nafasi ya maadili na kanuni za utawala katika ujenzi wa jamii yenyewe uwiano.

### Utangulizi

Somo hili linatoa maana na kueleza maadili ya kitaifa na kanuni za utawala zilizotajwa katika Ibara ya 4(2) na 10 ya Katiba ya Kenya (2010). Changamoto ambazo maadili na kanuni hizi zinajaribu kushughulikia zimeangaziwa, pamoja na mikakati ya kukuza maadili ya kitaifa. Somo linamalizika kwa kuangazia mchango wa maadili na kanuni za uongozi katika ukuzaji wa uwiano wa kitaifa.

### MADA 1: MAADILI, KANUNI ZA UTAWALA NA MANENO MENGINE

**Muda :** Dakika 10.

**Vitendea-kazi :** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala ya sera za uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu :** Chemsha bongo.

### SHUGHULI :

- Mwelekezi aongoze washiriki kutoa maana ya maadili na maneno mengine.
- Washiriki wajaribu kutoa maana za maneno hayo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kueleza maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

#### Maelezo ya Maana za Maneno

##### a. Maadili


Maadili ni kaida na mienendo ambayo hukubalika katika jamii, kundi au nchi. Maadili huongoza mtu, mkondo wa matendo au matokeo katika jamii. Maadili hueleza utambulisho wa watu, kama vile wao ni akina nani, wanaamini nini, wanasimamia nini na jinsi wengine wanavyowaona. Hivyo basi maadili ni muhimu.

### b. Wema

kwa upande mwingine, wema ni tabia zinazokubalika na ambazo huwezesha ustawi wa jamii. Kuishi maisha ya wema husababisha kuondolewa kwa maovu katika jamii na kuendeleza uwiano. Maadili ya kitaifa ni imani muhimu ya taifa ambayo huongoza matendo na mienendo ya wananchi na huathiri jinsi wananchi wanavyohusiana na kuhudumiana.

### c. Kanuni za Uongozi

Hizi ni kanuni ambazo hulazimisha nchi kutekeleza majukumu yake kwa njia ambayo huweza kuendeleza wananchi. Hivyo basi, ni kanuni ambazo zinahusiana na kazi ya nchi.



*Jedwali 12: Baadhi ya maadili ya kitaifa na kanuni za utawala*

## MADA 2: MAADILI YA KITAIFA NA KANUNI ZA UTAWALA KAMA ZILIVYO KATIKA KATIBA

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala ya sera za uwiano na utangamano.

**Mbinu:** Chemsha bongo.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kutaja maadili ya kitaifa na kanuni za utawala zilizopo kwenye Katiba.
- Washiriki wajaribu kutaja maadili ya kitaifa na kanuni za utawala.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala kama zilivyo katika Katiba ( Ibara 10)

#### 1. Uzalendo

Uzalendo ni upendo, utiifu na mtu kujitolea kwa nchi yake. Inahitaji mtu aunge mkono taifa lake licha ya changamoto zilizoko. Uzalendo unahu su huduma kwa taifa. Unahu su kujitambulisha kama Mkenya. Husaidia Kenya kupiga hatua katika kuleta maendeleo na ustawi wa taifa.

#### 2. Umoja wa kitaifa

Umoja ni uamuzi wa kuungana na wengine kwa minajili ya kutekeleza malengo ya pamoja. Ni uamuzi wa kufanya kazi kwa pamoja ili kukabili changamoto zinazokumba nchi. Ni nia ya kukubali mambo yanayotuunganisha na kutupilia mbali yale yanayotutenganisha. Kwa hivyo, ili kupata malengo yaliyomo kwenye Rajua ya 2030, kuna haja ya taifa kufanya kazi pamoja ili kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa .

#### 3. Ugavi na ugatuzi wa mamlaka.

Ugavi wa mamlaka unahu su mipangilio ya kisiasa ambapo makundi yanayopingana katika jamii hushiriki katika serikali. Mamlaka ya nchi hugawanywa kati ya vyama

mbalimbali, wala si kimoja tu. Kwa upande mwingine, ugatuzi ni usambazaji wa mamlaka na rasilmali kutoka kwa serikali kuu hadi mashinani.

#### **4. Utawala wa sheria**

Utawala wa sheria ni neno la kisheria ambalo linamaanisha kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria, na hakuna mtu anayeweza kuadhibiwa na serikali kabla hajakiuka sheria. Utawala wa sheria ni kinyume cha dhana kuwa mtawala yuko juu ya sheria. Utawala wa sheria unafuatwa wakati watu na serikali huamua kutii na kuongozwa na sheria wala si mambo yasiyo na mpango ya mtu au kundi la watu.

#### **5. Demokrasia na ushiriki wa watu**

Demokrasia ni mfumo wa kisheria ambapo kila mwananchi hushiriki moja kwa moja na kiusawa katika harakati za kuendeleza shughuli za nchi yake. Kwa upande mwingine, ushiriki ni desturi inayohusisha watu wote katika utoaji wa maamuzi ambayo huleta kuheshimiana na kukuza ugavi wa majukumu.

#### **6. Hadhi ya binadamu**

Hadhi ni neno linalotumika katika tabia, maadili na majadiliano ya kisiasa ili kuonyesha kuwa mtu ana haki ya kimsingi ya kuheshimiwa na kutendewa wema. Hadhi ya binadamu inamaanisha kuwa kila mtu anastahili kuonyeshwa upendo na heshima kwa kuwa yeye ni mtu, bila kuzingatia tabaka, mbari, jinsia, utaifa, mila, mielekeo yake ya kimapenzi, elimu, dini au kitu kingine chochote. Hadhi ya binadamu haistahili kutafutwa bali ni sehemu ya binadamu wote.

#### **7. Usawa**

Usawa unahu haki na ukosefu wa mapendeleo. Unahu haki na chochote ambacho ni cha haki. Ni sifa ya kutokuwa na mapendeleo, kuwa na umakinifu na haki katika maamuzi na matendo. Katika sheria, ni mfumo wa maarifa ya kisheria yenye msingi wa kanuni za mienendo ya haki. Huchukua nafasi ya sheria ya kawaida ambayo hupinga mapendeleo.

#### **8. Haki ya kijamii**

Haki ya kijamii inahu wazo la kubuni jamii au taasisi ambayo imejikita katika misingi ya kanuni za ulinganifu na mshikamano, ambazo huthamini haki za binadamu na kutambua hadhi ya kila mtu. Haki ya kijamii humaanisha usawa wa haki katika jamii ilhali 'haki' huzidi uongozi wa sheria. Haki ya jamii imejikita katika wazo la jamii ambalo hushughulikia watu na makundi kwa njia ya haki na ugavi wa manufaa ya jamii kwa njia ya haki.

## **9. Uhusishwaji**

Uhusishwaji ni hisia ya kuwepo, kuheshimiwa na kuthaminiwa vile ulivyo. Huhusu hisia kuwa watu wamejitolea kukusaidia. Utaratibu wa uhusishwaji unahusisha kila mtu na hufanya watu kuhihi kuwa wamethaminiwa na ni muhimu katika ufanisi wa kundi au shirika. Palipo na uhusishwaji, watu hufanya kazi kikamilifu, huhisi kuwa wamethaminiwa zaidi na huona kuwa wamehusishwa katika harakati za nchi yao.

## **10. Ulingano**

Ulingano ni hali ya kijamii ambapo watu wote katika jamii fulani huwa na hadhi sawa kwa njia fulani. Ulingano wa kijamii unahusu usawa wa haki chini ya sheria, kama vile usalama, kupiga kura, uhuru wa kujieleza na wa kujumuika, na pia haki ya kupata mali. Inahusu pia nafasi na majukumu sawa, na kwa hivyo hujumuisha jamii nzima. Ulingano unamaanisha ukosefu wa matabaka ya jamii na ubaguzi unaotokana na sifa za kutambulisha mtu ambazo haziwezi kubadilika, kama vile jinsia, umri, mielekeo ya kimpenzi, asili, tabaka, hali ya uchumi, lugha, dini, imani, maoni, afya au ulemavu. Yote haya hayastahili kusababisha ukosefu wa usawa chini ya sheria na hayastahili kupunguza nafasi ya mtu bila haki.

## **11. Haki za binadamu**

Haki za binadamu ni haki ambazo ziko kwa watu wote, bila kujali utaifa, makao, jinsia, kabilia, rangi, dini, lugha, au hali yoyote ile. Sote tunastahili kupata haki za kimsingi bila kubaguliwa. Haki hizi zote zinahusiana, zinategemeana na haziwezi kutenganishwa.

Haki zote za binadamu, ziwe za raia au za kisiasa, kama vile haki ya kuishi, usawa mbele ya sheria au uhuru wa kujieleza ; haki za kiuchumi, kijamii au kimila, kama vile haki ya kufanya kazi, usalama wa kijamii na elimu, au haki za jumla kama vile haki za maendeleo na kujitolea, haziwezi kutenganishwa. Zinahusiana na kutegemeana. Kuboreshwa kwa kila haki hurahisisha kuendelea kwa zile nyingine pia. Kadhalika, kudunishwa kwa haki yoyote kuna madhara makuu kwa zile nyingine.

Haki za binadamu zinahusu haki na wajibu. Nchi hufuata wajibu na majukumu yaliyo chini ya sheria za kimataifa; kuheshimu, kulinda na kutimiza haki za binadamu. Wajibu wa kuheshimu humaanisha kuwa nchi ni sharti ikatae kuingilia au kuzuia haki za binadamu. Wajibu wa kulinda hapa unahitaji nchi kulinda watu au makundi dhidi ya uvurugaji wa haki zao. Wajibu wa kutimiza unamaanisha kuwa taifa linapaswa kuchukua hatua mwafaka ili kurahisisha manufaa ya haki za kimsingi za binadamu. Kama vile katika kiwango cha mtu binafsi ni kupata haki za binadamu, tunastahili pia kuheshimu haki za binadamu wengine.

## 12. Kutobagua

Kutobagua humaanisha kuwa tuwatendee wengine haki bila mapendeleo, bila kuzingatia jinsia, kabilia, tabaka, dini, mbari, tofauti za kijografia au hata za kizazi.

## 13. Kulinda kundi lililotelekezwa

Kutekelezwa ni utaratibu wa kijamii wa kuwekwa au kushushwa hadi kwenye nafasi ya chini katika jamii. Kundi lililotelekezwa huwa limetengwa na jamii na hulazimishwa kuwa pembeni. Makundi yaliyotelekezwa kwa kawaida hayatambuliwi katika jamii.

## 14. Utawala bora

Utawala ni utaratibu wa kutoa maamuzi ya pamoja na kutekeleza maamuzi hayo. Utawala bora kwa upande wake humaanisha jinsi taasisi za umma zinavyoendeleza maswala ya umma na jinsi zinavyodhibiti rasilmali ili kuhakikisha kuwepo kwa haki za binadamu na maslahi ya kijamii. Katika mataifa mengi, wananchi huzipa taasisi za taifa wajibu wa kutoa na kutekeleza maamuzi ambayo yataboresha maslahi yao.

## 15. Uadilifu

Uadilifu ni dhana ya uthabiti wa matendo, maadili, mbinu, hatua, kanuni, matarajio na matokeo. Katika elimu ya maadili, uadilifu huelezwa kama ukweli na uaminifu katika matendo ya mtu. Uadilifu ni uwezo na ustawi wa tabia, hali ya uaminifu na ukweli kulingana na mshawasha wa matendo ya mtu. Uadilifu unahusu kuwa na nia ya kukataa matendo ya ujisadi, ya kutekezeza majukumu yasiyo maadilifu. Uadilifu unahitaji uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu. Kukubali uadilifu kutaruhusu Wakenya kuweka matendo yao katika misingi ya kanuni thabiti hata kama zitamdhuru mtu binafsi.

## 16. Uwazi na Uwajibikaji

Uwazi ni kuweka mambo dhahiri. Ni ukosefu wa kuweka mambo siri. Hali hii inahusisha kuwepo kwa habari zinazotakikana katika mashauriano, ushirikiano na maamuzi ya pamoja. Katika uwazi, kuna wajibu wa makampuni ya umma kuwajibika katika maswala ya fedha na majukumu ya kijamii, kwa wale waliowapa hayo majukumu.

Uwajibikaji wa umma huhitaji watu waliopewa rasilmali za umma kutunza kutoa maelezo kuhusu udhibiti wa rasilmali hizo na kuwajibika katika maswala ya fedha na udhibiti wa majukumu ya mipango waliyopewa. Uwajibikaji ni kusimamia matokeo, yaliyo au yasiyo na utaratibu, ambayo yamewakilishwa na hatua za ufanisi katika idadi na ubora.

## 17. Maendeleo ya kudumu

Maendeleo ya kudumu yaweza kuelezwu kama mfumo wa matumizi ya rasilmali unaolenga kutimiza mahitaji ya binadamu huku yakihifadhi mazingira ili mahitaji haya yatimizwe wakati uliopo na wa vizazi vijavyo. Inaweza pia kufafanuliwa kama maendeleo ambayo yanatimiza mahitaji ya sasa bila kudunisha uwezo wa vizazi vijavyo wa kutimiza mahitaji yavyo.

Maadili na kanuni hizo zote za utawala yametajwa katika Katiba ya Kenya kama ifuatavyo :

1. Ibara 132 (1c) inamhitaji Rais kutoa habari kwa taifa mara moja kila mwaka, kuhusu hatua zote zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa maadili ya kitaifa, yaliyotajwa katika Ibara 10;
2. Ibara 232 inataja maadili na kanuni zifuatazo kwa wafanyakazi wa umma:
  - a. Kiwango cha juu cha uadilifu wa kikazi.
  - b. Matumizi ya rasilmali yenyen ufanisi, faafu na makinifu;
  - c. Kutoa huduma kwa njia ya kuajibika, haraka, fanisi, yenyen kuzingatia usawa na bila mapendeleo;
  - d. Kuwahusisha watu katika michakato ya kutunga sera ;
  - e. Uwajibikaji katika matendo ya kiutawala ;
  - f. Kutoa habari za kweli kwa umma , kwa wakati na kwa njia ya wazi;
  - g. Kwa kuzingatia aya (h) na (i), kuwe na uzingativu wa mashindano ya haki na uhitimu kama msingi wa kuajiriwa kazi na kupanda cheo;
  - h. Uwakilishaji wa jamii anuui za Kenya; na
  - i. Kupata nafasi sawa na za kutosha za ajira, mafunzo na maendeleo katika viwango vyote vya utumishi wa umma, kwa-
    - (i) Wanaume na wanawake;
    - (ii) Watu wa makabila yote; na
    - (iii) Watu wenye ulemavu.

Bunge linatarajiwa kutunga sheria za kutekeleza kikamilifu Ibara hii.

3. Ibara 234 inahitaji kuwa Tume ya Huduma za Umma iendeleze maadili na kanuni zilizotajwa kwenye ibara 10 na 232 katika huduma zote za umma.
4. Ibara 249 inaeleza kuwa wahudumu wa tume na afisi huru walenge kudumisha demokrasia kuhusu kanuni na maadili katika mashirika yote ya serikali, mionganini mwa mengine.
5. Ibara 255 inaeleza kuwa Ibara 10 (2) (a) hadi (d) zinazotaja maadili ya kitaifa na kanuni za utawala, haziwezi kubadilishwa, ila kwa kupitia kura ya maamuzi.
6. Ibara 259 inaeleza kuwa Katiba ifasiriwe kwa njia itakayoendeleza malengo yake, maadili na kanuni zake.
7. Ibara 159 inataja kanuni zifuatazo za kuongoza mahakama na korti katika kutekeleza mamlaka:

- a. Haki itatendwa kwa wote bila kujali hali ya mtu;
  - b. Haki haitacheleweshwa ;
  - c. Njia m'badala za kusuluhiha migogoro kama vile upatanishi, usuluhishi na mbinu za kitamaduni zitaendelezwa, kutegemea kifungu cha 3; na
  - d. Haki itatekelezwa bila kufuata mifumo ya kitaratibu isiyo na sababu za kuridhisha; na Malengo na kanuni za Katiba hii zitalindwa na kuendelezwa.
8. Sehemu 23 ya Mpangilio wa Sita inaeleza kuwa Bunge litatunga sheria na taratibu za kuchunguza majaji na mahakimu ambao walikuwa mamlakani katika siku ya utekelezaji wa Katiba, waendelee kuhudumu kulingana na maadili na kanuni zilizobainishwa katika Ibara 10 na 159.

### MADA 3: CHANGAMOTO ZINAZOSHUGHULIKIWA NA MAADILI NA KANUNI ZA UTAWALA

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuzwa, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala za sera ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo, majadiliano.

#### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kutaja changamoto zinazoshughulikiwa na maadili na kanuni za utawala.
- Washiriki wajaribu kutaja changamoto hizo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



#### Vidokezo Muhimu

##### Changamoto zinazoshughulikiwa na maadili na kanuni za utawala

Baadhi ya changamoto kuu ambazo maadili ya kitaifa yatashughulikia ni kama vile:

1. Kuvurugika kwa familia kama msingi wa jamii;
2. Kutovumiliana kwa sababu ya tofauti za kijamii;
3. Kudorora kwa nidhamu ya kijamii;
4. Kuvunja sheria bila kujali.
5. Utengwaji;
6. Ufisadi na utawala mbaya;
7. Kupuuza mienendo ya uadilifu;
8. Kudunisha hadhi ya kitaifa;
9. Fujo katika jamii kama mbinu ya kusuluhisha mafarakano;
10. Kuvuruga haki za binadamu;
11. Kudorora kwa taasisi za kijamii;
12. Mienendo mibaya ya kazi;
13. Uongozi usiofaa;
14. Kupuuza uhitimu;
15. Kutozingatia usawa katika usambazaji wa rasilmali;
16. Umaskini;
17. Ubepari usiozingatia utu;
18. Ulokole wa kidini kupita kiasi.

## MADA 4: MIKAKATI INAYOSHIRIKISHA MAADILI YA KITAIFA NA KANUNI ZA UTAWALA

**Muda:** Dakika 30.

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala za sera ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo, majadiliano.

### SHUGHULI:

- Mwelekezi aongoze washiriki kutambua mikakati inayoshirikisha maadili ya kitaifa na kanuni za utawala.
- Washiriki wajaribu kutambua mikakati hiyo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo Muhimu

Mikakati inayoshirikisha maadili ya kitaifa na kanuni za utawala

- a. Mafunzo kwa raia kuhusu maadili ya kitaifa na kanuni za utawala;
- b. Kuyapa kipaumbele maadili ya kitaifa na kanuni za utawala katika mfumo wa elimu;
- c. Kutetea kanuni zenyе maadili kuitia vyombo vya habari;
- d. Kuyapa kipaumbele maadili ya kitaifa na kanuni za utawala katika sera za kitaifa;
- e. Kutambua na kutuza mabingwa wa maadili na kanuni za utawala;
- f. Kujenga ushirika baina ya mashirika ya umma na yale ya kibinafsi ili kuwezesha uendelezwaji wa maadili ya kitaifa na kanuni za utawala;
- g. Kufanya utafiti unaozingatia ithibati kuhusu maadili na kanuni za utawala; na
- h. Kushirikiana, kujenga mahusiano na kuiga desturi nzuri zaidi.

## **MADA 5: NAFASI YA MAADILI NA KANUNI ZA UTAWALA KATIKA KUENDELEZA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA .**

**Muda:** Dakika 30

**Vitendea-kazi:** Chati-za-kugeuza, kalamu za kutia alama, nakala za Katiba na nakala za sera ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

**Mbinu:** Chemsha bongo na majadiliano.

### **SHUGHULI:**

- Mwelekezi aongoze washiriki kutaja nafasi ya maadili na kanuni za utawala katika uendelezaji wa uwiano wa kitaifa na ushirikiano.
- Washiriki wajaribu kutaja nafasi hiyo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### **Vidokezo Muhimu**

#### **Nafasi ya maadili na kanuni za utawala katika kuendeleza uwiano wa kitaifa na ushirikiano.**

- a. Kufanya Kenya iwe taifa la mbele katika Jumuiya ya madola;
- b. Kuzipa harakati zote za kitaifa maana, umuhimu na mwelekeo, na kuimarisha utambulisho wa kipekee wa kitaifa;
- c. Kutoa mbinu za kutangamanisha mienendo ya kila shughuli za umma, huduma za jamii, kutekeleza udhibiti wa uongozi;
- d. Kuendeleza maslahi ya Wakenya;
- e. Kuiga desturi bora ambazo zinatafaa kufuatwa na kuthaminiwa na kila mtu; na
- f. Kuweka kipimo cha kutathmini na kukagua utendaji wa kila mtu na kutambua uhitimu wa kila mtu katika nafasi za kazi.

## Marejleo

- "Kalenjin." Countries and Their Cultures. Available online at  
<http://www.everyculture.com/wc/Japan-to-Mali/Kalenjin.html>
- "Kenya – Folklore". East Africa Living Encyclopedia Available online at  
<http://www.africa.upenn.edu/NEH/kfolklore.htm>
- "Kenya – Religion". East Africa Living Encyclopedia Available online at  
<http://www.africa.upenn.edu/NEH/kreligion.htm>
- "Luo": Countries and Their Cultures. Available online at  
<http://www.everyculture.com/wc/Japan-to-Mali/Luo.html>
- "MijikendaTribe" available At  
[http://www.enhols.com/kenya\\_safari/people/mijikenda/](http://www.enhols.com/kenya_safari/people/mijikenda/)
- African Studies Center--University of Pennsylvania. "Kenya – Ethnic groups". East Africa Living Encyclopedia.January 14, 2010).
- Ahmed Ali Jimale, 'The Somali Oral Tradition and the Role of Storytelling in Somalia' for the Minnesota Humanities Center.  
<http://mnhumanities.org/Resources/somalioraltradition.pdf>
- Allen James de V., (1982) "Shungwaya, the Mijikenda, and their Traditions", a Review of Thomas Spear, Traditions of Origin and their Interpretation: The Mijikenda of Kenya. Athens, Ohio: Ohio University Press
- Barret Antony, (1998) Turkana Iconography: Desert Nomads and Their Symbols. Kenya: Kijabe Printing Press
- Biikabku, 'Kalenjin Culture and Traditions,' available online at  
[http://www.biikabkutit.com/blog/view/id\\_32/title\\_Kalenjin-culture-and-traditions/](http://www.biikabkutit.com/blog/view/id_32/title_Kalenjin-culture-and-traditions/)
- Burke Cormac, (2007) Man and Values - a Personalist Anthropology.
- Finke Jens, 'The Traditional Music and Cultures of Kenya : Kamba – Fables and Legends - The Art of Story-telling' Available online at  
<http://www.bluegecko.org/kenya/tribes/kamba/stories.htm>
- Fontrodona Juan, (2004) Beyond Agency Theory: The Nature of the Firm from a Humanistic Perspective. Nairobi: Strathmore University Press
- Gakuru Wahome, (2006) Presentation to Media Owners - Kenya Vision 2030: Transforming National Development. Nairobi: National Economic and Social Council
- Gathogo Julius Mutugi, 'African Hospitality: Is it Compatible with the Ideal of Christ's Hospitality?' Part 1 Churchman pp. 39-56  
[http://www.churchsociety.org/churchman/documents/Cman\\_120\\_1\\_Gathogo.pdf](http://www.churchsociety.org/churchman/documents/Cman_120_1_Gathogo.pdf) online at <http://www.scribd.com/doc/3480381/Vision-2030-Popular-Version>
- Grossman M. J., 'People Profile: The Kalenjin Peoples of Kenya,'  
<http://strategyleader.org/profiles/kalenjin.html>

- Gyekye Kwame, (1996) African Cultural Values: An Introduction.  
 Philadelphia and Accra: Sankofa Publishing Company
- Hunter Lewis, (1991) A Question of Values Six Ways We Make The Personal Choices That Shape Our Lives. London: Harper Collins Publishers Moral Values: The Ongoing Youth Christian Education In Modern Kenya,' African Ecclesia Review (AFER) Vol. 6 pp. 361
- Kirwen C. Michael, (2005) African Cultural Knowledge: Themes and Embedded Beliefs. Nairobi: Maryknoll Institute of African Studies Books
- Kirwen Michael C., Ed. (2008) African Cultural Domains: Life Cycle of an Individual. Nairobi: Maryknoll Institute of African Studies Books
- Lagan Bruce, (1996) 'It's Goodbye to 'Virtues' and Hello to 'Values',' New Zealand Herald, 1 October
- Mimbi Paul, (2007) The Overlooked Factor: The Power of Being Fully Human. Nairobi: Strathmore University Press
- Mimbi Paul, (2009) The Sources of Effective Leadership. Nairobi: Strathmore University Press
- Miruka Okumba, (2001) Oral Literature of the Luo. Nairobi: East African Educational Publishers
- Ng'ang'a Wanguhu, (2006) Kenya's Ethnic Communities: Foundation of the Nation. Kenya: Gatundu Publisher
- Nomi Ron, (2004) "The Ogiek: Guardians of the Forest", Seattle Preparatory High School, African Studies. Available online at <http://www.ogiek.org/>
- Osogo John, (1965) Life in Kenya in the Olden Days: The Baluyia. Oxford: Oxford University Press
- Otieno Pireh, (2001) 'Values-Based Approaches to Community Water Education' in UN-HABITAT, Water Education in African Cities: Report of an Expert Group Meeting. South Africa: Johannesburg
- Patka Frederick, (1964) Value and Existence; Studies in Philosophic Anthropology. New York: Philosophical Library Economic Science, 2nd Ed., New York: New York University Press
- Sam Turner, 'People Profile: The Kikuyu People of Kenya,' available online at <http://strategyleader.org/profiles/kikuyu.html>
- Samper David E., 'Love, Peace, and Unity: Romantic Nationalism and the Role of Oral Literature in Kenya's Secondary Schools,' Folklore Forum 28/1 (1997) pp. 29-47
- Sobania Neal, (2003) Culture and Customs of Kenya. London: Greenwood Press

## SOMO 14: UKAGUZI NA UTATHMINI WA MIRADI YA UWIANO NA UTANGAMANO WA KITAIFA

**LENGO:** Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki wanahitaji kutumia mbinu za ukaguzi na utathmini wa miradi na shughuli za uwiano na utangamano wa kitaifa.

### Utangulizi

Somo hili linatoa maana ya ukaguzi na utathmini. Linataja pia utaratibu wa kufanya utathmini na ukaguzi wa miradi ya uwiano na utangamano wa kitaifa. Umuhimu wa ukaguzi na utathmini umeangaziwa huku mbinu na vifaa mwafaka vikitolewa.

### MADA 1: TOFAUTI KATI YA UKAGUZI NA UTATHMINI

**Muda :** Dakika 10.

**Vitendea-kazi :** chati, kalamu za wino, madaftari, kalamu, kanda za maelezo.

**Mbinu :** Chemsha bongo.

### SHUGHULI :

- Mwelekezi awaongoze washiriki kubainisha utathmini na ukaguzi.
- Washiriki wajadili maana za maneno haya.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki.



### Vidokezo muhimu

#### Ubainishaji:

##### 1. Ukaguzi.

Hali hii ni ya kila siku ya kufuatilia shughuli wakati wa kuzitekeleza ili kukagua maendeleo na kutambua kasoro. Ni ufuutilizi wa kila mara kwa nia ya kuhakikisha kuwa shughuli zinatikelezwa kama ilivyopangwa. Ukaguzi ni uchunguzi wa kila mara wa kunakili shughuli zinazoendelea katika mradi au mpango fulani. Ni utaratibu wa kutafuta habari kuhusu kila sehemu ya mradi. Uchunguzi pia unahu su kutoa ripoti

kuhusu maendeleo ya mradi fulani kwa watekelezaji, wale watakaofaidi na wadau wa mradi. Kutoa habari kunasaidia watekelezaji kutumia habari hiyo kuboresha mradi huo. Ukaguzi ni muhimu kwa sababu:

- Hufuatilia matumizi na matokeo;
- Hutambua na kushughulikia upungufu uliopo;
- Huhakikisha matumizi bora ya rasilimali;
- Huendeleza ubora katika utoaji wa huduma na elimu ili kuboresha shughuli na huduma;
- Hutoa nafasi za mafunzo na kuboresha utendaji;
- Huhudumu kama chombo cha kudhibiti mradi; na
- Hukusanya habari kuhusu shughuli zinazoendelea.

## 2. Utathmini

Utathmini ni utaratibu wa kutoa uamuzi wa thamani kuhusu kile ambacho mradi umepata hasa kuhusiana na shughuli zilizopangwa na malengo ya jumla. Unahu uamuzi wa thamani na kwa hivyo ni tofauti na ukaguzi. Utathmini pia ni uchunguzi wa matukio ya mafanikio na athari zake. Ni njia ya kitaratibu ya kujifunza kutoka kwa uzoefu ili kuboresha shughuli ibuka na kuendeleza miradi bora kwa shughuli zijazo. Imepangwa haswa kwa nia ya kuhusisha mabadiliko na mashauriano.

Utathmini ni muhimu kwa kuwa:

- Hubaini ufanisi, ufanifu, udumishaji, umuhimu na athari za miradi;
- Huimarisha matokeo na uwajibikaji wa kifedha;
- Huendeleza desturi ya mafunzo inayositisiza uboreshaji wa huduma; na
- Hueleza juu ya marudio ya mashauriano bora.

Ukaguzi	Utathmini
• Huendelea siku kwa siku	• Muda fulani: hatua kuu
• Hurekodi maendeleo	• Uchanganuzi wa kina wa mafanikio
• Husisitiza matumizi na matokeo	• Husisitiza matokeo na athari
• Hujuza wasimamizi matatizo	• Huwapa wasimamizi chaguo la mikakati na mbinu
• Hujichunguza	• Uchanganuzi wa nje

Jedwali 13: Tofauti kati ya Ukaguzi na Utathmini

## MADA 2: UTARATIBU WA UKAGUZI NA UTATHMINI

**Muda:** Dakika 10.

**Vitendea-kazi:** Chati ya kugeuzwa, kalamu za wino , madaftari, kalamu, kanda za maelezo.

**Mbinu :** Chemsha bongo.

### SHUGHULI :

- Mwelekezi awaongoze washiriki kuchunguza mchakato wa utathmini na ukaguzi.
- Washiriki wajaribu kuchunguza mchakato huo.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kuelezea maoni ya washiriki



### Vidokezo muhimu

#### 1. Utaratibu wa Ukaguzi na Utathmini

Ukaguzi na utathmini unahusu hatua zifuatazo:

- a. Kutafuta habari ya kimsingi kuhusu hali ya sasa (uchunganuzi wa hali);
- b. Kutayarisha matokeo na malengo katika hatua ya kupanga;
- c. Kuchagua viashiria vya matokeo vitakavyochunguzwa;
- d. Kuweka shabaha maalum za kutekelezwa na muda wa makataa wa kuzingatiwa;
- e. Kukusanya habari kila wakati ili kuchunguza ikiwa shabaha zilizowekwa zinafikiwa; na
- f. Kuchanganua na kuripoti matokeo.

#### 2. Kushiriki katika Ukaguzi na Utathmini.

Ukaguzi na utathmini wa shughuli za uwiano na utangamano wa kitaifa huhusisha wahusika mbali mbali. Wahusika hawa ni kama Wizara inayohusika na uwiano na utangamano wa kitaifa, Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa, wizara nyingine husika, tume nyingine, asasi za kidini, washirika wa maendeleo, asasi za kielimu na jamii kwa jumla.

Majukumu yanayopaswa kutekelezwa na wahusika mbalimbali ni kama:

- a. Kufanya ukaguzi na utathmini;
- b. Kuchanganua habari;
- c. Kutangaza matokeo ya utathmini;
- d. Kupitia mipango ya uwiano kulingana na matokeo; na
- e. Kutoa msaada wa kiujuzi, kifedha na kiuongozi kwa ukaguzi na utathmini.

### **3. Ukaguzi na Utathmini shirikishi**

Ukaguzi na utathmini shirikishi ni utaratibu ambao wadau mbali mbali wanahusika pamoja katika utaratibu wa ukaguzi na utathmini kwa kutumia mwelekeo wa chinijuu. Kanuni kuu ya ukaguzi na utathmini shirikishi ni kuwahusisha wale watakaonufaika.

### **4. Manufaa ya Ukaguzi na Utathmini shirikishi**

- a. Huwezesha uwajibikaji kati ya wahusika na kudumisha matokea halali na ya kutegemewa;
- b. Ufahamu wa pamoja wa matatizo na utambuzi wa masuluuhisho: ukaguzi shirikishi husaidia wadau kuelewa pamoja matatizo yanayokabili jamii au miradi (asili, uzito na athari zake);
- c. Hunufaisha makundi lengwa na kuwezesha uwajibikaji: ushiriki katika ukaguzi huhakikisha kuwa walengwa ndio wanaonufaika;
- d. Huongeza uhamasishaji wa haki za watu ambazo huwafanya kulinda rasilmali za miradi dhidi ya ufujaji;
- e. Hujumuisha uwezo wa pamoja na kupunguza matumizi mabaya ya nguvu; na
- f. Ukaguzi na utathmini shirikishi huwezesha ubora wa maamuzi, hivyo basi kuboresha utendaji wa miradi.

### MADA 3: UMUHIMU WA UKAGUZI NA UTATHMINI

**Muda:** Dakika 10

**Vitendea-kazi:** Chati ya kugeuzwa, kalamu za wino, madaftari, kalamu, kanda za maelezo.

**Mbinu :** Chemsha bongo.

#### SHUGHULI :

- Mwelekezi awaongoze washiriki kuchanganua umuhimu wa ukaguzi na utathmini.
- Washiriki wajaribu kuchanganua umuhimu na changamoto za ukaguzi na utathmini.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kueleza maoni ya washiriki.



#### Vidokezo muhimu

##### 1. Umuhimu wa Ukaguzi na Utathmini

- a. Kupima ubora wa shughuli za uwiano wa kitaifa na hatua za kuchukuliwa, na iwapo zinatimiza malengo yaliyowekwa;
- b. Kuangazia mabadiliko katika mazingira ambayo huathiri utekelezaji wa mipango ya uwiano wa kitaifa;
- c. Kutambua desturi nzuri, kupata mafunzo kutoka kwa uzoefu wa shughuli hiyo na kusaidia kuboresha utendaji;
- d. Kuendeleza ufanyaji kazi wa pamoja, kukuza uwazi na kuwezesha uwajibikaji kwa wadau husika;
- e. Husaidia wahusika kukadiria athari za shughuli za uwiano na utangamano wa kitaifa;
- f. Kuhakikisha kuna utaratibu wa kuripoti;
- g. Kuwasilisha matokeo kwa wahusika na watakaonufaika;
- h. Kutoa habari kwa ajili ya kufanya maamuzi bora; na
- i. Kuhakikisha ugavi bora wa rasilimali.

**2. Ukaguzi unaofaa hujibu maswali yafuatayo :**

- a. Je, tunapata tunachokusudia? Vipi? Kwa nini au kwa nini hatupati?
- b. Vizuizi vya utekelezaji ni vipi?
- c. Tunaratibu vilivyo?
- d. Kasoro za utekelezaji ni zipi? Tutazishughulikia vipi?

**3. Utathmini unaofana hujibu maswali yafuatayo:**

- a. Tulifanya nini?
- b. Tulifanya vipi?
- c. Tulipata kile tulichotarajia?
- d. Tulileta athari gani?
- e. Tumejifunza nini?
- f. Tunashughulikia masuala makuu? Ikiwa sivyo, kasoro ni zipi?
- g. Mradi huo unaweza kurudiwa kwingineko?

**4. Changamoto za Ushiriki katika Ukaguzi**

- a. Gharama za awali za juu: kushiriki katika ukaguzi kunahitaji rasilmali kama vile wakati, usafiri na marupurupu. Ni utaratibu wenye gharama ya juu na unaweza kuathiri asasi.
- b. Ukaguzi unahitaji kukusanya, kurekodi na kubadilishana habari. Haya huhitaji ujuzi mbali mbali ambao wahusika wanaweza kuukosa katika viwango mbalimbali.

## MADA 4: MBINU NA ZANA ZA UKAGUZI NA UTATHMINI

**Muda:** Dakika 40

**Vitendea-kazi:** Chati ya kugeuza, kalamu za wino, madaftari, kalamu, kanda za maelezo.

**Mbinu :** Chemsha bongo.

**SHUGHULI :**

- Mwelekezi awaongoze washiriki kutaja mbinu na zana za ukaguzi na utathmini.
- Washiriki wajaribu kutaja mbinu na zana za ukaguzi na utathmini.
- Mwelekezi atumie hoja kuu kueleza maoni ya washiriki.



Chemsha bongo

### Vidokezo muhimu

#### 1. Mbinu na Zana

Uthibitishaji wa matokeo ya ukaguzi na utathmini hubainishwa kuitia kwa matumizi ya viashiria. Kiashiria ni sifa ambayo inaweza kupimwa ili kubaini mabadililiko katika hali ya uwiano na utangamano wa kijamii. Viashiria ni sharti viwe halisi, vya kupimika, vya kweli na kutegemewa. Viashiria ni vibainishi vya aina za mbinu na zana zitumiwazo katika ukaguzi na utathmini. Kuna zana na mbinu kadha ambazo zinaweza kutumiwa kukusanya habari. Hizi zinahusisha:

- a. Hojaji;
- b. Mahojiano;
- c. Utafiti wa kimsingi;
- d. Miongozo ya uchunguzi;
- e. Ripoti za matukio; na
- f. Majadiliano elekezi ya vikundi.

Muundo katika jedwali 4 unaweza kutumiwa kupima utendakazi wa miradi katika viwango mbali mbali.

*Jedwali 14 a: Kupima utendakazi wa mradi*

<b>Kupima Utendakazi wa Mradi</b>			<b>Kutathmini matokeo na athari za uwiano wa kitaifa</b>	
<b>Mahitaji</b>	<b>Utaratibu</b>	<b>Mazao</b>	<b>Matokeo</b>	<b>Athari</b>
Watu Fedha Wazo Utafiti Taratibu za sera Msaada wa kitaalamu	Kutumia rasilmali za kifedha katika kupanga ; Mafunzo Mikutano Ushawishi Mawasiliano Ununuizi	Mbinu za uratibu Maendeleo katika ushirikishaji Watu kufunzwa Huduma kutolewa	Ongezeko la uhamasishaji Ongezeko la kupata haki Ongezeko la kimaeneo	Ukuza ji wa hali ya uwiano wa kitaifa Kuwezesha kijamii na kiuchumi
Viashiria vya mahitaji	Viashiria vya utaratibu	Viashiria vya utaratibu	Viashiria vya matokeo	Viashiria vya athari

## **2. Muundo wa Ukaguzi na Utathmini katika Harakati za Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.**

Muundo wa ukaguzi na utathmini hutekelezwa katika viwango vya mahitaji, mazao, matokeo na athari, kama ilivyoashiriwa kwenye jedwali 5.


*Jedwali 14 b: Kupima utendakazi wa mradi*

<b>Kiwango</b>	<b>Maelezo</b>	<b>Idadi ya Marudio</b>
<b>Mahitaji</b>	Rasilmali zinazohitajika kwenye mradi. Husababisha mazao.	Kila wakati
<b>Mazao</b>	Huduma au shughuli ambazo kampeni zinakusudia kutoa. Mazao husababisha matokeo	Baada ya miezi mitatu
<b>Matokeo</b>	Mabadiliko katika tabia kutokana na shughuli zilizotekelawa. Matokeo yanatazamiwa kuleta athari.	Miaka 2-3 (kipindi kifupi au wastani)
<b>Athari</b>	Mabadiliko yanayopimika ya hali ya uwiano, yaani kupungua kwa athari za mafarakano. Matokeo ya athari husababishwa na kuingilia kati ili kubadilisha mambo.	Miaka 3-5 ( kipindi kirefu)

### 3. Ukaguzi na Utathmini wa Kimatokeo

Ukaguzi na utathmini wa kawaida hulenga katika mahitaji, matendo na mazao. Changamoto za mwelekeo huu ni kuwa haulengi matokeo ya mashauriano ambayo yanatekelezwa. Hatari zake ni kuwa mafunzo mengi, desturi bora na uzoefu wa baada ya mashauriano, yote hupotea. Mwelekeo huu huitwa ukaguzi wa kiutekelezaji.

Ili kuzuia haya, mwelekeo wa kimatokeo hutumika. Huu hulenga kuona jinsi ufanisi wa miradi unaendelezwa na kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kwa hivyo, ukaguzi na utathmini wa kimatokeo huzingatia sehemu ya utekelezaji na pia huchanganua matokeo pamoja na athari za miradi.



*Mchoro 5: Mwelekeo wa Ukaguzi na Utathmini unaozingatia Matokeo*

#### Mfano wa Muundo wa Ukaguzi na Utathmini

Ili kuzingatia mwelekeo wa kimatokeo wa ukaguzi na utathmini, muundo ufuatao unaosisitiza kupata shabaha fulani kwa ajili ya viashiria maalum, umependekezwa.

*Jedwali 15: Mfano wa muundo wa ukaguzi na utathmini.*

Kiashiria	Msingi na Shabaha					Upataji habari			
	MS	Mwaka1	Mwaka2	Mwaka3	Mwaka4	Ratiba	Chanzo cha habari		Majukumu
1.									
2.									
3.									

#### **4. Mikakati ya Ukaguzi na Utathmini kwa ajili ya Miradi na Shughuli za Uwiano na Utangamano wa Kitaifa**

Ili kupata mikakati inayofana ya ukaguzi na utathmini, mambo yafuatayo yapaswa kufuatwa:

- a. Kubaini malengo ya mbinu za ukaguzi na kupima mahitaji ya habari;
- b. Kuhakikisha mashauriano ya uwiano wa kitaifa yana malengo, mazao na viashiria dhahiri;
- c. Kuweka kwa mpangilio mzuri zana za kuripoti;
- d. Kubaini mbinu za kupata habari juu ya viashiria;
- e. Kuwapa watu majukumu ya kukusanya habari, kubaini wakati, idadi ya marudio katika kupata habari, na kugawa rasilmali; na
- f. Kuweka mbinu za kupashana habari na kuhusisha matokeo katika mipango ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

#### **Marejleo**

Bozeman B. and Feeney M. K., (2007) 'Toward a Useful Theory of Mentoring: A Conceptual Analysis and Critique,' *Administration & Society* Vol. 39 Issue no. 6 pp. 719–739

DuBois David L. and Michael J. Karcher, (2005) *Handbook of Youth Mentoring* Thousand Oaks, California: SAGE Publications Ltd.

Parsloe E. and Wray M. J., (2000) *Coaching and Mentoring: Practical Methods to Improve Learning*. Kogan Page.

